ULINGANISHI WA KIDHAMIRA WA NYIMBO ZA BONGO FLEVA NA HADITHI FUPI ZA MAGAZETI YA UDAKU

Na

Felister Julius Mtey

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii inayoitwa **“Ulinganishi wa Kidhamira wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi zaMagazeti ya Udaku”** na anapendekeza kwamba inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi za Jamii katika Fasihi ya Kiswahili.

……..

Prof. J.S. Madumulla

(Msimamizi)

Tarehe……..

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi, **Felister Julius Mtey**, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi, na kwamba haijawahi kuwasilishwa, katika Chuo chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada nyingine yoyote.

Saini……..

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kuzalisha, kunakili, ama kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

SHUKURANI

Shukrani jazila nazitoa kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa imetimia tasnifu! Yeye ndiye wa kushukuriwa zaidi, kwa sababu amenipitisha salama katika tesi za ulimwengu katika kipindi chote cha masomo ya darasani na wakati wa uandishi wa tasnifu hii. Ama kwa hakika, kidole kimoja hakivunji chawa, walipata kunena wahenga. Kamwe siwezi kujidai kuwa yote niliyofanya ili kazi hii itimie nimeyafanya kwa urazini ama ujanja wangu tu, ila ni kwa nguvu na jitihada za watu mbalimbali walionipa msaada na ushirikiano wakati wa mchakato wa kuandika tasnifu hii. Wote ninawashukuru sana. Mtima wangu unawiwa kuwataja wote kwa majina yao, lakini orodha yao ndefu inabinywa na uchache wa karatasi. Lakini kwao wote ninasema, “Ahsante sana”.

Baada ya kumshukuru Rabuka kwa jamala na uhai na vyote, sichelei kumtaja msimamizi wangu, Prof. J.S. Madumulla. Huyu ni mwalimu ambaye nawiwa mfano madhubuti wa kumfananisha naye. Kwake nimejifunza mambo mengi mazuri kama mwalimu, kiongozi, na mzazi. Hakika, yeye ni mfano wa kuigwa. Alinifaa sana kwa msaada wake adhimu na maelekezo yake aushi aliyonipatia katika kipindi chote cha utafiti wangu. Hata pale nilipohisi kukata tamaa, kutokana na changamoto mbalimbali zilizoniandama, alinitia moyo. Aliniamrisha na kunitia ari ya kusonga mbele na kwa hiyo, kwa mwongozo wake hakuna ambacho kilikwenda tofauti. Namshukuru kwa fikra na mawazo yake kuhusu mada yangu ya utafiti, sina cha kumpa ila nasema ahsante sana na Mungu akupe maisha marefu hapa duniani yenye nguvu, amani na upendo ili uendelee kuwasaidia na kuwaongoza wengine.

Shukrani zangu nyingi ziwaendee wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mafunzo mazuri waliyonipatia katika kiwango hiki cha Umahiri. Sina

budi kuwataja baadhi yao katika tasnifu hii: Prof J.S Madumulla (msimamizi na mwalimu wangu), Dkt. Elias M. Songoyi, Dkt. Mohamed S. Khatib, Dkt. R.Y. Sebonde, na Dkt. S.A. Ponera. Hawa walinisaidia vema kuukwea mlima huu wa elimu. Pia, siwezi kuwasahau wote ambao tulikuwa nao darasani katika mihadhara na tamrini, maktabani na kwingineko. Tulisaidiana katika furaha na karaha zetu, huku tukioneana huruma na kutiana moyo katika yote tuliyoyafanya. Nawataja wachache kuwakilisha wengine. Hawa na sahiba zangu Arafa Jumanne, Asia Yassin, Upendo Mdaha, Doroth Elisa, Magreth Mjale, Joyce John, Prosister Tarimo, Neema Victor, Neema Tandiko, Daniel Mollel, Adam Jumbe, Meshack Mwigulu, Ally Shabani, Peter Ngongolo, Said Amour, Yusuph Mohamed na Lawi Lechipya. Maisha yangekuwa magumu sana chuoni kama hawa wote wasingekuwepo.

Nawashukuru watu wote walionisaidia huko uwandani wakati wa utafiti huu. Kipekee, nawashukuru sana Bw. Oscar Ndauka, Bi Irene Ndauka Bw. Ally Mbetu, wanachuo wa vyuo vikuu vya UDOM, UDSM na Ustawi, wanafunzi wa sekondari, mashabiki wa nyimbo za Bongo Fleva na wasomaji wa hadithi fupi za Magazeti ya Udaku.

Ninawashukuru wadogo zangu wapendwa wa kike Jescar, Monica, Mwanaidi, na Lea na wadogo zangu wa kiume Abasi, Mrisho, Anchilaus, James na Mohamed kwa kuwa walinitia moyo katika safari yangu ya masomo. Pia napenda kuwashukuru kaka zangu Adinani Mabaraza, Mohamed Walele, Gilbert Kafunafu na Burhan Msaka, pamoja na familia zao. Hawa waliniwezesha kutimiza ndoto zangu kwa kunitia moyo na kunipa ushauri wakati wa masomo yangu.Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa mama yangu mdogo, Bi. Upendo Msuya na familia ya Bw na Bi Julius Mtunda, Peter George, Kaisi Mwakibete, Hamis Mfuko na Juma

Katema, kwa upendo wao, ushauri na maombi yao mpaka kufikia hapa nilipo, ahsanteni sana, na Mungu awabariki. Pia nawashukuru wanangu wapendwa Nusrath, Kamran, na David kwa kunivumilia muda mrefu ambao sikuweza kukaa na nyie. Mungu awatangulie, mkue katika misingi ya dini.

Pia nawashukuru wazazi wangu wapendwa Bw na Bibi Julius Mtey kwa kuwa taa yangu maishani. Ninajivunia kuwa mwanenu, nawapenda sana. Maana mlinitoa tongotongo za ujinga kwa kunipeleka shule. Mlipofanya ibada kamwe hamkunisahau. Mliniombea nipate kufanikiwa katika maisha yangu. Juhudi zenu za kupigania ustawi wangu wa kesho ndizo zimenifikisha katika kiwango hiki cha elimu, ndiyo maana hamkusita kuendelea kunitunza hata pale nilipoweza kujitegemea, kwani mliendelea kunilea kama mtoto mdogo ambae nahitaji kila kitu kutoka kwenu! Nawapenda sana, Mungu awape maisha marefu zaidi duniani yenye nguvu, baraka, upendo na amani daima ili sisi nasi siku moja tuje tulipe fadhila japo kidogo tu, maana hatuwezi kulipa kile mlichotutendea katika dunia hii.

TABARUKI

Kwenu wazazi wangu wapendwa Bw na Bibi Julius Mtey, nawashukuru sana kwa upendo wenu usio na kikomo. Nawashukuru sana kwa kunilea, kuniombea na kunipeleka shule na harakati za kunisaidi hiki na kile, ilimradi tu nitimize malengo yangu. Yote haya nayakumbuka kwa sababu yalinipa moyo na kuniongezea juhudi zaidi ya kusonga mbele. Sikuwa na wasi wasi hata kidogo kwa kuwa nilijua siku zote mko nyuma yangu kwa lolote lile na kuniongoza kusonga mbele kukamilisha kazi hii. “Nashukuru sana”.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza suala la **Ulinganishi wa Kidhamira wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku,** kwa kutumia nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi zilizomo ndani ya Magazeti ya Udaku. Mtafiti alipata wazo la kufanya utafiti huu kutokana na watafiti wengi kujikita katika lugha, matatizo yanayowakumba wanamuziki, na katika hadithi; kuchunguza athari za dhamira, hadithi za makabila, na hadithi fupi za Kiswahili. Lakini hakuna aliyelinganisha dhamira za muziki na hadithi. Kipengele cha ulinganishaji wa dhamira hakikupewa kipaumbele kutokana na kujikita zaidi katika kuchunguza vitu viwili kwa wakati mmoja. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya Upokezi/mwitikio wa msomaji katika kuyafikia malengo yake. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kulinganisha dhamira za nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, ili kuona kama dhamira hizo zinafanana au kutofautiana katika jamii.

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba dhamira zilizopo ndani ya Muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana, zinafanya kazi sawa na zina lengo moja katika jamii.

Vile vile utafiti huu umeweza kuonyesha wazi, kuwa muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku vina mchango mkubwa katika jamii, kwani vinaelimisha, vinaburudisha, vinakosoa na kutoa muongozo katika jamii. Hivyo, watu wasivipuuze na kuona ni vitu visivyofaa na visivyokuwa na thamani katika jamii, au kuona ni vya kihuni na vinawahusu vijana tu. Bali watunzi na waandishi wazingatie zaidi tamaduni za Kiafrika, katika kuimba na kuandika kazi zao, pia katika uchapishaji wa magazeti hayo ya udaku na uvaaji wa wanamuziki vijana.

YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ..... **ii**
IKIRARI NA HAKIMILIKI ..... **iii**
SHUKURANI ..... **iv**
TABARUKI ..... **vii**
IKISIRI ..... **viii**
YALIYOMO ..... **ix**
ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU ..... **xiii**
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVOTUMIKA ..... **xvi**

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA UTAFITI **1**
1.0 Utangulizi **1**
1.1 Usuli wa tatizo **1**
1.2 Tamko la tatizo la utafiti **3**
1.3 Malengo ya Utafiti **3**
1.3.1 Lengo la Jumla **3**
1.3.2 Malengo Mahususi **3**
1.4 Maswali ya Utafiti **3**
1.5 Umuhumu wa Utafiti **4**
1.6 Mkabala wa Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data za Utafiti **4**
1.7 Msingi wa Nadharia ya Upokezi/mwitikio wa Msomaji **5**
1.7.1 Jinsi Nadharia Hii Ilivyotumika **10**
1.8 Mipaka ya Utafiti **11**
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza **11**

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO **12**
2.0 Utangulizi **12**
2.1 Maandiko Kuhusu Historia ya Muziki wa Bongo Flava **12**
2.2 Historia ya Hadithi Fupi **15**
2.3 Muundo wa Hadithi Fupi **16**
2.3.1 Sifa za Hadithi Fupi **17**
2.3.2 Maudhui **18**
2.4 Maandiko Kuhusu Magazeti ya Udaku **18**

2.5 Mapitio Kuhusu Magazeti ya Udaku **20**
2.5.1 Magazeti ya Udaku **20**
2.6 Mapengo Yaliyojitokeza **24**
2.6.1 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa **24**

SURA YA TATU: USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI 25
3.1 Mpango wa Utafiti **25**
3.2 Eneo la Utafiti **26**
3.3 Walengwa wa Utafiti **26**
3.3.1 Wago Tafutiwa **27**
3.3.2 Sampuli ya Watafitiwa **27**
3.4 Ukusanyaji Data **28**
3.4.1 Njia na Zana za Kukusanya Data **29**
3.4.1.1 Udurusu wa Kimaktaba **29**
3.4.2 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Uthibiti Wake **29**
3.5 Uchanganuzi wa Data **30**
3.6 Uhalali na Uthibiti wa Matokeo ya Utafiti **30**
3.7 Vikwazo vya Utafiti na Utumizi Wake **31**

SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ... 32
4.1 ..Msukumo wa Watunzi wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti Ya Udaku. **32**
4.1.1 Msukumo wa Watunzi wa Nyimbo za Bongo Fleva **32**
4.1.2 Nyimbo Teule za Wanamuziki wa Muziki wa Bongo Fleva **34**
4.1.2.1 Wimbo wa Linex – Mama Halima **34**
4.1.2.2 Wimbo wa Diamond - Safari **35**
4.1.2.3 Wimbo wa Lady Jay Dee - Nasimama **36**
4.1.2.4 Wimbo wa Nikki wa Pili akishirikiana na Ben Pol – Sitaki Kazi **36**
4.1.2.5 Wimbo wa Professa Jay aliyemshirikisha Juma Nature na Babu Ayubu – Ndiyo Mzee **37**
4.1.3 Msukumo wa Watunzi na Waandishi wa Hadithi Fupi wa Magazeti ya Udaku **37**
4.2 Wateuzi Teule na Watunzi wa Hadithi Fupi katika Magazeti ya Udaku **40**

4.2.1 Hadithi ya Godoro la Mtumba, iliyotungwa na kuandikwa na Irene Mwamfupe Ndauka. **40**
4.2.2 ..... Hadithi ya Kutoka Uchungaji Mpaka Ukuu wa Wachawi, iliyotungwa na kuandikwa na Ally Mbetu **42**
4.2.3 Kubainisha Dhamira Zinazopatikana katika Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku. **44**
4.2.3.1 a) Wimbo wa Lady Jay Dee, Nasimama **44**
4.2.3.1b) Wimbo wa Diamond, Safari **47**
4.2.3.1c) Wimbo wa Nikki wa Pili na Ben Pol, Sitaki Kazi **49**
4.2.3.1d) Wimbo wa Professor Jay na Juma Nature, Ndio Mzee **51**
4.2.3.2 Kubainisha Dhamira Zinazopatikana katika Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku **53**
4.3 ... Ulinganishaji wa Kidhamira katika Nyimbo za Bongo Fleva na Hadidhi Fupi za Magazeti ya Udaku **74**
4.3.1. Mwongozo wa Usaili kwa Watu wa Makamo, Viongozi wa Dini na Wanasiasa **74**
4.3.2 Mwongozo wa Usaili kwa Wanafunzi na Wanachuo **75**
4.3.3 ..... Mwongozo wa Mjadala wa Vikundi kwa Washabiki wa Muziki wa Bongo Fleva na Wasomaji wa Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku. **76**
4.4. Jinsi Dhamira za Muziki wa Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku Zinavyofanana **78**
4.4.1 ... Dhamira za Muziki wa Bongo Fleva Zilizojitokeza, Kutoka kwa Wanamuziki Teule **78**
4.4.2 Dhamira za Hadithi Fupi Zilizojitokeza, katika Magazeti ya Udaku za Waandishi Teule **79**
4.4.3 ..... Ulinganishi wa Kidhamira wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku **81**
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne **81**

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 82
5.1 Muhtasari **82**
5.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika **82**

5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu **83**
5.5 Hitimisho **84**
MAREJELEO **86**
VIAMBATANISHO **89**

ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU

Sehemu hii inaelezea baadhi ya dhana ama istilahi muhimu ambazo zinahusiana na mada tuliyoitafiti.

Maana ya Bongo Fleva

Neno bongo linatokana na neno ubongo ambapo kwa lugha ya mtaani, linamaanisha akili. Vijana wengi wa mtaani hasa kutoka Dar es salaam wanauita mji wa Dar es salaam bongo wakimaanisha ni mahali ambapo lazima akili itumike ili kuishi katika mji huo. Hivi sasa neno bongo limepata mashiko kwa vijana wengi wa Tanzania kiasi kwamba linatumika kumaanisha Tanzania, kwa maana ya kuwa, ili uishi maisha mazuri katika Tanzania unatakiwa kufikiri, au kutumia akili.

Neno ‘fleva’ limetokana na neno la Kiingereza “flavor” (Englert.2003.75) lenye maana ya ladha. Hivyo basi neno, Bongo Fleva linamaanisha ladha za bongo, au tunadiriki kusema, midundo motomoto ya Tanzania.

Maana ya hadithi

Hadithi ni Fasihi yenye kusimulia (*narrate)* habari fulani. Ni masimulizi ambayo yanatumia lugha ya mjazo au nathari na mtiririko wake huwa mwepesi au sahili. Urefu wa hadithi hutofautiana kutoka kipera kimoja hadi kingine.

Hadithi Fupi

Dhana ya hadithi fupi imefafanuliwa na Wamitila (2002:68) kuwa ni utungo mfupi wa kinathari unaojishughulisha na suala fulani kuu, wenye wahusika ambao hawakuzwi kwa kina na unaotumia mbinu za kimaelezo za kibanifu, zenye uelekezi wa kiwango cha juu na athari kuu moja. Madumula (2009:108) anafafanua dhana ya

hadithi fupi kwa namna mbili, ufafanuzi wa kwanza, ni aina ya kazi ya sanaa inayotumia lugha ilioandikwa kwa nathari. Hadithi ya aina hii husimulia tukio moja au matukio mawili na inatumia mawanda yasiyo mapana sana, haina mchanganyiko mkubwa wa matukio. Hadithi fupi hutumia wahusika wachache sana ukilinganisha na wale wa riwaya, hutendeka kwa muda mfupi na ina mtiririko wa kiupeo. Ufafanuzi wa pili, ni masimulizi mafupi ya kubuni yaliyo katika mtindo wa nathari, yakisawiri maisha ya mtu wa wakati maalum, mahali maalum na kwa madhumuni maalum. Senkoro (2011:58) anasema hadithi fupi kuwa ni utanzu wa fasihi ambao hutumia wahusika wachache na huwachukulia wahusika hao kwa kiwango cha jumlajumla mno cha kuwakilisha tabia, mienendo na matendo na huzungumzia mambo kwa ufupi (si kwa upana).

Aidha Songoyi na Masele (2013:33) wanasema kuwa hadithi fupi ni utanzu wa kinathari ambao hutumia muundo rahisi, hutumia wahusika wachache, aghalabu mmoja, ambaye hubeba maudhui ya hadithi; huwa na jambo moja linalozungumziwa na hutumia lugha kwa ubanifu sana na huwa lugha rahisi ambayo ina ubunifu ndani yake.

Kwa ufafanuzi wa wataalamu hawa, tunaweza kusema kuwa hadithi fupi ni utanzu wa Fasihi unaotumia lugha ya kinathari na hutumia wahusika wachache katika kuzungumzia jambo moja linaloikumba jamii.

Maana ya dhamira

Dhamira, ni wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya Fasihi. Wazo au mawazo hayo anakuwa nayo msanii au mwanafasihi katika kuwasilisha au kusana kazi yake ya Fasihi ambayo ameikusudia ifike kwa jamii husika.

Magazeti ya Udaku

Hushughulikia habari ambazo ni za kiumbeaumbea na ambazo, kwa kawaida, haziendani sana na urasmi. Gazeti la namna hiyo inadaiwa kuwa halisomwi sana na waungwana, bali ni uga maarufu wa watu wa kawaida, na hasa vijana, tena wasio wasomi.

Udaku

TUKI, (1981:293), wanafafanu neno udaku kuwa ni tabia ya kutafuta na kutaka kujua habari za watu. Kwa mujibu wa utafiti huu udaku litatumika kuelezea magazeti yale ambayo yanaandika sana mikasa ya watu. Magazeti haya huandika habari za watu zikiambatana na picha zao hivyo huwavutia wasomaji hasa wale wanaopenda kufuatilia habari za watu. Kwa kifupi udaku ni kufuatilia habari za watu.

Dhana zilizofafanuliwa hapo ni muhimu katika kuzungumzia dhamira zilizomo ndani ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya udaku. Utafiti huu umezitumia baadhi ya dhana hizi katika uhakiki, na uchambuzi wa kazi zilizoteuliwa kwa lengo la kukamilisha utafiti, na kuwapa fursa wasomaji wa kazi hii ya kuifahamu vema dhamira zilizopo ndani ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, na kuona kwamba zinafanana na zina lengo moja kaika jami

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVOTUMIKA

Prof:	Profesa.
Dkt:	Daktari wa Falsafa.
TUKI:	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
BAKITA:	Baraza la Kiswahili la Taifa.
Uk:	Ukurasa.
UDOM	Chuo Kikuu cha Dodoma.
UDSM	Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
Bw.	Bwana.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, ambayo jamii hutumia kama kioo katika maisha kwa kutatua matatizo, kuiga au kujifunza yaliyo mema kupitia wanamuziki na waandishi mbalimbali katika jamii inayowazunguka. Vipengele muhimu kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahususi, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti, vimeelezwa.

1.1 Usuli wa tatizo

Sanaa ina matawi mengi na Fasihi ni moja wapo kati ya hayo. Fasihi nayo imegawanyika katika matawi makuu mawili; Fasihi simulizi na Fasihi andishi. Katika utafiti huu tutajikita katika Fasihi Andishi, hususani, nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Nyimbo za Bongo Fleva zimewekwa katika Fasihi Andishi na siyo Fasihi Simulizi kwa kuwa waandishi au watungaji wa nyimbo hizi huziandika kwanza ndipo huziimba. Hivyo, ndiyo maana nyimbo hizi zimewekwa katika Fasihi Andishi na siyo Fasihi Simulizi.

Muziki wa Bongo Fleva ni aina ya muziki ambao umetokana na utamaduni wa hip hop. Aina hii ya muziki inapambanuliwa na vipengele vya msingi vinne vya kimtindo ambavyo ni kughani (rapping), ufundi wa kusugua santuri wakati wa kupiga muziki (*DJing/scratihing*), usanisi (*sampling synthesis*), na mdundo (*beat boxing*). Kwa upande wa hadithi za Magazeti ya Udaku ni hadithi ambazo zinaandikwa na waandishi mbalimbali zikihusiana na mapenzi, uchawi, na upelelezi.

Kwa jumla hadithi nyingi za magazeti ya udaku na nyimbo nyingi za Bongo Fleva zinahusu mapenzi.

Kwa hiyo watu wengi hasa watu wazima, viongozi wa kidini na serikali wanachukulia kuwa muziki wa Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku kuwa ni vitu visivyokuwa na maana wala maadili mema katika jamii ya Kitanzania na hupotosha vijana na watoto, na husababisha kukua katika misingi mibaya isiyokuwa na maadili ya Kitanzania. Baadhi ya matatizo ni kama vile kutamani kuwa na wapenzi katika umri mdogo na kusababisha kufanya tendo la ndoa mapema mno; kujihusisha na uvutaji bangi; kukataa kuendelea na shule na kujiingiza katika muziki huo kwa kuona kuwa ni njia moja wapo ya kuwafanya wawe na utajiri wa haraka.

Utafiti uliofanyika juu ya kipera hiki umechunguza njia mahususi za namna Bongo Fleva ilivyoenea, ilivyopokewa, ilivyoendelezwa na mabadiliko iliyoyapata katika mazingira mbalimbali na kwa muda tofauti (Kraidy, 1999; Frimpong, 1999).

Watanzania wengi, hasa watu wa makamo, viongozi wa dini na wanasiasa hawatoi kipaumbele katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi za magazeti ya udaku kwa kuwa wanaona siyo vya muhimu sana katika jamii ya Kitanzania. Mtafiti ameona achunguze kulingana au kutofautiana kwa dhamira za nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za magazeti ya udaku. Ili kuwaondolea watanzania mawazo ya kuwa muziki wa Bongo Fleva na hadithi za magazeti havina umuhimu katika jamii; mtafiti ameona alinganishe dhamira zake ili kupata tofauti au kufanana kwao na kuweza kupata sababu ya msingi au siyo ya msingi ya kutopewa kwao kipaumbele katika jamii.

1.2 Tamko la tatizo la utafiti

Asilimia kubwa, hasa watu wazima, viongozi wa siasa na kidini hawapendi muziki wa Bongo Fleva na magazeti ya udaku na wanaona muziki huu na magazeti haya havina maana yoyote katika jamii ya Kitanzania. Mtafiti ana lengo la kulinganisha dhamira za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku ili aone kama kweli dhamira zake hazina thamani katika jamii. Wanataaluma, waandishi na wachunguzi mbalimbali wamejitokeza kushughulikia muziki wa kizazi kipya, ukiwemo muziki wa Bongo Fleva kwa makusudi ya kuachana, lakini si katika kulinganisha dhamira zake na kazi nyingine za kifasihi.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya udaku kidhamira ili kuona umuhimu wao katika jamii.

1.3.2 Malengo Mahususi

a) Kubaini msukumo wa watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi katika magazeti ya udaku.

b) Kubainisha dhamira zinazopatikana katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya udaku.

c) Kulinganisha dhamira za Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya udaku.

1.4 Maswali ya Utafiti

a) Ni msukumo upi wanaoupata watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi katika Magazeti ya Udaku, na, je, dhamira zao zinafanana au kutofautiana?

b) Ni kwa vipi dhamira zinapatikana katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku?

c) Ni kwa namna gani dhamira za (wanamuziki) muziki wa Bongo Fleva na (waandishi wa) hadithi fupi katika Magazeti ya Udaku zinafanana au kutofautiana?

1.5 Umuhumu wa Utafiti

Utafiti huu unalenga kuleta mabadiliko ya kimtazamo na kifikra juu ya muziki wa Bongo Flava na hadithi za Magazeti ya Udaku. Lakini pia Utafiti huu unalenga kutoa mchango katika nyanja mbalimbali: Kwanza, Utafiti huu unalenga katika kuchunguza ulinganishi wa kidhamira kati ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku ili kuzielewa na kubainisha kufanana kwao au kutofautiana kwao. Hivyo, kazi hii itaibua mjadala juu ya ulinganishi wa kidhamira kati ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Pili, utasaidia wasomaji wa tasnifu hii kufahamu kufanana au kutofautiana kwa dhamira kati ya Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Mdaku. Tatu, tasnifu hii itakuwa ni chachu ya wataalam ili kuangalia kwa jicho la ziada au pevu mapengo na mianya iliyopo katika utafiti na kuchunguza kwa makini dhamira zinazotumika katika nyimbo na hadithi zote kwa jumla. Nne, kuondoa dhana iliyoenea katika jamii, hasa kwa watu wazima na viongozi wa dini na serikali kuwa muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku ni vya kihuni na vinawahusu wahuni au vijana tu, hivyo havina michango wala faida yoyote katika jamii.

1.6 Mkabala wa Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data za Utafiti

Katika uchambuzi wa data, kuna nadharia mbalimbali ambazo hutumika katika uchanganuzi wa kazi za kifasihi. Miongoni mwa nadharia hizo ni nadharia ya

Umarksi, Ufeministi, Usosholojia, Umuundo, Upokezi wa hadhira na nyinginezo nyingi.

Nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. (*Wafula na Njogu* 2007,)

Nadharia ni mwongozo unaomwelekeza mpokezi wa kazi ya Fasihi kuifahamu kazi ya Fasihi kwa undani zaidi. Nadharia inaweza kuundwa kutokana na tajiriba ya mtu binafsi au juhudi za kikundi cha watu. Nadharia huwasaidia wapokezi wa kazi ya kifasihi katika juhudi za kuziweka kwenye mizani kwa lengo la kutathimini ufanisi wa fanani. Vilevile nadharia ni kama dira inayowapa wapokezi vigezo sawa au mwongozo wa kuzithamini kazi za Fasihi.

Kila mtafiti hutumia nadharia moja au mbili kulingana na malengo ya utafiti wake. Hivyo, katika utafiti huu nadharia ya upokezi/mwitikio wa msomaji imetumika.

1.7 Msingi wa Nadharia ya Upokezi/mwitikio wa Msomaji

Nadharia ya upokezi/mwitikio wa msomaji, ni nadharia inayomlenga moja kwa moja msomaji; inayomuweka msomaji katikati ya uhakiki wa Fasihi. Hushughulikia uhusiano uliopo kati ya fanani na kazi ya fasihi, msomaji wa kazi husika, mchakato wa usomaji pamoja na maana za matini. Ni nadharia iliyoanza miaka ya sitini na sabini ya karne ya ishirini, hasa kule Marekani na Ujerumani. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), miongoni mwa washadidiaji wa nadharia hii ni Wolfgang Iser (1974; 1978), Stanley Fish (1980), James Thompkins (1980), na Haus Robert Jauss (1982). Kuzaliwa kwa nadharia hii ni matokeo ya msuguano wa kifikra uliodumu muda mrefu kuhusu dhana ya ujenzi wa maana ya matini ya kifasihi. Wahakiki wa fasihi, kwa muda mrefu, wamekuwa wakivutana kuhusu ama kazi ya fasihi huwa na maana moja tu au huwa na maana tofauti.

Nadharia hii kwa upande wake, inaamini kuwa ukweli au maana ya kazi ya fasihi haina umbo wala sura moja iliyo maalum. Imani hii ya wanaupokezi inatokana na hoja inayochukulia kazi ya fasihi kama umbo lisilotimia daima. Hali hiyo ya kuwa au kutokuwapo kwa utimilifu katika matini za fasihi haiwezi kuchanganuliwa kwa kutumia seti ya kanuni za kimaabara kama ifanyavyo kwa dhana mbalimbali za sayansi asilia. Fasihi siyo kipengele cha sayansi asilia; ni sanaa ya maneno. Hapo ndipo litokeapo wazo muhimu la kumhitaji sana mtumiaji (hadhira) ili alikamilishe umbo la kazi ya fasihi. Hivyo, wao humweka msomaji katikati ya fanani na maana ya matini ya fasihi ili akamilishe maana. Hufanya hivyo kwa kuamini kuwa msomaji huwa na mawazo ya awali kuhusu matini anayopitia. Mawazo haya hutokana na tajiriba ya kimaisha, hususani ya usomaji wa matini mbalimbali kwa nyakati maalum, na kwamba, kwa namna moja au nyingine, msomaji wa kazi ya fasihi huathiri maana ya matini hiyo (Wamitila, 2002;Mushengyezi, 2003; Wafula na Njogu, 2007). Iser (1974) na Fish (1980) ambao wamenukuliwa na Wamitila (2002) wanadai kuwa kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hulazimika kuyajaliza. Kwa hiyo, msomaji hulazimika kutunga matini mpya ambazo hutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa. Mushengyezi (2003) kutokana na umuhimu wa msomaji katika upataji wa maana za matini za fasihi, ni vema msomaji kusaidiwa kuyajua majukumu na mikakati ya usomaji. Majukumu na mikakati hiyo ya usomaji ni pamoja na ufahamu na uzingatiaji wa misingi ya kiisimu na kifasihi pamoja na duara ya ki-Heminitiki.

Nadharia hii ya upokezi yaweza kubainishwa katika makundi matatu, wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji, kama vile C.S Lewis (1961) na, Stanley Fish (1967). Kisha kuna wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalum cha wasomaji, kama vile Reuven Tsur (1974), Richard Gerrig na

David Miall (1981). Na hatimaye wale wanaochukulia kwamba wasomaji wote wataipokea kazi ya Fasihi kwa njia sawa, kama vile Wolfgang Tser (1976) na Haus Robert Jauss (1978).

Hata hivyo, Stanley Fish (1980) anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi ili kuonyesha ujuzi uliofanikiwa au ujuzi ambao haujafanikiwa. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007:85-86) watetezi wa nadharia ya upokezi, huuliza maswali ambayo misingi ya nadharia hii imejengeka. Maswali haya ni pamoja na:

a) Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?

b) Je, kila kazi ya Fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia?

c) Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za Fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine?

d) Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Adena Rosmarin katika (Murfin 1991) anadai kuwa kazi ya Fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika, na kwa hivyo, mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kwamba:

Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Tser na Fish (1976) wanadai kwamba kazi ya Fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hulazimika kuyajaliza.

Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za Fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji mbalimbali hufasiri athari hizi kupitia njia mbalimbali:

a) Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.
b) Namna matini inavyoelekeza au kutatiza mwitikio wa msomaji. Sifa inayozua mwitikio mzuri au mbaya wa kazi inayohusika.

Wanadharia hawa wanashikilia kuwa kuna njia mbili za kusoma kazi za Fasihi ambazo ni:

- Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejulikana na kutambuliwa na msomaji.
- Kuwasilisha kazi za Fasihi kimafumbo ili kumchochea msomaji kujitaftia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi anayoisoma.

Usomaji ni tendo linalofanyika na kutekelezwa kwa wakati maalum, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo. Fish anadai kuwa wasomaji wanapaswa kufanya mikataba ya aina fulani na matini hizi katika miktadha mbalimbali.

Msomaji anayetumia mikakati ya mwitikio kusoma kazi ya sanaa hufuata hatua tatu katika waledi wa kazi za Fasihi.

a) Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.

b) Hubainisha jinsi miktadha ya matini inayohusiana moja kwa moja na maandishi, inayoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji.
c) Hudhihirisha kuwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.

Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi. Huck (1976) anadai kuwa lengo kwa hapa ni kuwabainisha wasomaji, kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji. Hivyo, ni muhimu kuepuka kulazimisha kasumba au misimamo fulani ya jinsi watu wanavyopaswa kuipokea kazi fulani ya Fasihi.

Baadhi ya wahakiki wa kisasa wanadai kwamba uhakiki kwa mujibu wa nadharia ya upokezi, umekosa kutambua kuwa matini ina uwezo wa kupanua welewa wa msomaji. Aidha, wanadai kwamba nadharia hii imewaruhusu wasomaji kufasiri matini/kazi ya Fasihi jinsi wapendavyo. Hivyo, maoni yale ya Tser (1976) yanaafikiwa, aliposisitiza kuwa msomaji hana budi kuzielewa mbinu, kaida na kanuni zinazotumiwa katika kazi fulani ya Fasihi ili kuweza kuisoma kikamilifu. Kwa hivyo, nadharia hii ingali muhimu katika uhakiki wa kazi za Fasihi kwa jumla.

Hivyo, nadharia ya usomaji itatumika kuchunguza usomaji katika kazi za wasanii wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya udaku kwa kuzingatia hatua zifuatazo: Kwanza kusoma kazi za waandishi teule na kukisia maana zake kutokana na fikra binafsi na uzoefu wa mtafiti kuhusiana na hadithi na nyimbo mbalimbali alizowaihi kuzisoma na kusilikiza maishani. Pili, kuhusisha na mikitadha mbalimbali iliyomo katika kazi za waandishi teule na mikitadha inayohusisha mifumo ya kiuchumi, kijamii, kijiografia, kisiasa na kihistoria iliyojiri kabla, wakati na baada ya utunzi. Tatu, kutoa maana inayoendana na ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku katika kazi hii. Ni matumaini ya mtafiti

kuwa kinadharia hii itafaa katika uchambuzi na utafiti huu kwa sababu msingi wake mkubwa umejikita katika namna mbalimbali za ujengaji wa maana kutoka katika matini. Matumizi ya nadharia hii yatazingatia pia maoni ya kiukosoaji kutoka kwa baadhi ya wahakiki wa kisasa wanaodai kwamba nadharia ya upokezi huwaruhusu wasomaji kufasiri kazi ya fasihi kadri wapendavyo; hali ambayo huweza kusababisha ‘fujo’ ya kimaana. Uwamuzi wa kuitumia nadharia hii unajikita katika msisitizo wa Iser (1976) ambaye amenukuliwa na Mushengyezi (2003) kuwa msomaji hana budi kuzielewa na kuzingatia mbinu, kaida na kanuni zinazotumiwa katika usanaji wa kazi ya fasihi ili kuweza kuisoma vema.

Ukusanyaji wa data na uchambuzi wa data na uwasilishaji wake umefanyika kwa kuzingatia mhimili wa nadharia hii ambao ni upokezi/mwitikio wa msomaji, kwa uchunguzi wa kidhamira katika nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Kwa kuzingatia nadharia ya upokezi/mwitikio wa msomaji imetumika katika utafiti huu kwa kuwa huuliza maswali yaliyomsaidia mtafiti kuhoji kwa wahojiwa na hivyo kusababisha wahojiwa kugundua kwa haraka dhamira zilizopo katika kazi hizo za kifasihi.

1.7.1 Jinsi Nadharia Hii Ilivyotumika

Tulitumia nadharia hii ya upokezi/mwitikio wa msomaji katika kuchunguza dhamira zilizopo ndani ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Upokezi huu ulilinganishwa na hali za kijamii, na jinsi nyimbo na hadithi hizo zinavyoashiria uhalisia katika jamii kutokana na dhamira zake. Vile vile nadharia hii ilituongoza kuangalia nyimbo na hadithi hizo kama njia maalum ya kuchunguza dhamira hizo, Pia nadharia hii ilituongoza kuonesha kuwa dhamira zilizopo ndani ya

nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana kutokana na kuwa na sifa zinazofanana.

1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, hususani, zile za wasanii “Lady Jay Dee, Diamond, Linex, Nick wa Pili na Professor Jay” na waandishi “Irene Ndauka na Ally Mbetu”. Zimetumika kazi zao mojamoja katika kuchunguza kwa jicho la jumla katika kutafuta muhamala au ithibati zaidi kuhusu dhamira mbalimbali zilizotumika katika kazi zao kuwa zinafanana au kutofautiana.

1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imeangalia mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti wetu. Nayo ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti huu, na umuhimu wa utafiti huu kwa jamii na wataaluma. Pia imeelezwa namna nadharia ua upokeze/mwitikio wa msomaji na mwisho kuna mipaka ya utafiti huu. Masuala ya mapitio ya maandiko kuhusiana na mada ya utafiti tutaona katika sura ya pili.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO

2.0 Utangulizi

Sura hii inabainisha mapitio mbalimbali yanayohusu muziki wa kizazi kipya. Mapitio haya yanatoa mwanga juu ya mtazamo katika nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku hususani katika dhamira zilizopo ndani ya nyimbo hizo na hadithi hizo. Sura hii inajumla ya sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu machapisho yanayozungumzia chimbuko na maendeleo ya muziki wa Bongo Fleva, historia ya hadithi fupi na Magazeti ya Udaku. Sehemu ya pili machapisho yanayoelezea dhana ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi. Mwisho ni mapengo yanayopaswa kuzibwa.

2.1 Maandiko Kuhusu Historia ya Muziki wa Bongo Flava

Hip hop ilianza kusini mwa Bronx katika jiji la New York katika miaka ya 1970. Wakati mwingine neno Rap hutumika katika kumaanisha muziki huu huu wa hip hop au Bongo Fleva.

Muziki huu una historia ndefu, ama kuanzishwa kwake kunahusishwa na Wamarekani weusi wa huko Bronx, New York, Marekani miaka ya 1970. Muziki wa Rap ni moja kati ya element nne za mwanzo za utamaduni wa hip hop, ambapo element tatu za mwanzo ni graffit ambayo ni maandishi au michoro inayochorwa sehemu za wazi kama vile ukutani; u – DJ ambao ni kuchagua na kupiga muziki katika redio, santuri na n.k; na mabreka (breakdancing) ambazo ni mtindo wa kucheza muziki mbele ya hadhira kwa kujinyonganyonga na kushika sehemu mbalimbali za mwili. Element hizi za utamaduni wa hip hop zilikuwa zikijitokeza

kwa hawamu, yaani moja ilipofifia, iliibuka nyingine. Ilianza sanaa ya graffit ikafuatiwa ya u-DJ halafu rap.

Wamarekani weusii wana asili ya Afrika ambapo babu zao walichukuliwa kwenda Marekani kama watumwa (Toop, Rose, 1994; Southern, 1997; Mitchel, 2001; Yassin, 2001) Mizizi hasa ya muziki wa rap ni Afrika kwani mbali ya kuanzishwa na Wamarekani weusii, muziki wa rap una sifa mbalimbali za kifasihi za Kiafrika ikiwa ni pamoja na matumizi ya midundo na mahadhi ya kuvutia, usimulizi, kiitikio na majigambo. (Omari 2004: 69: 73).

Wamarekani weusi walikuwa na dhamira za element zao kama vile; utamaduni wao katika malazi, mavazi, na makazi, mapambano, nguvu za dola. Wanamuziki wa Kitanzania waliiga baadhi ya dhamira hizo za Kimarekani; na baadae waliamia katika dhamira zilizoonekana katika jamii yao ya Kitanzania kama vile, utamaduni wao katika mavazi, malazi na makazi, mapambano, dola na nguvu zake, ukosefu wa ajira na athari zake, madawa ya kulevya, siasa, nafasi ya mwanamke katika jamii, mapenzi, umasikini na mengineyo.

Kuingia kwa muziki wa hip hop hapa Tanzania kumeelezwa na watu kwa namna mbalimbali. Wanataaluma na waandishi hawa wanaiona historia ya muzuki wa hip hop kuwa ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Chachage (2002) na Mangecho (2003) wamesema kuwa hapa Tanzania muziki wa hip hop au Bongo Fleva uliingia mnamo mwishoni mwa miaka ya 1980. Vijana walianza kuimba wakiwa ufukweni na baadaye katika sherehe mbalimbali. Ulianza kusikika redioni mwaka 1995; Sherehe zinazorejelewa hapa ni zile za kuwakaribisha

ama kuwaaga wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Nne, Tano na Sita na sherehe za ufukweni (beach parties).

Baadae, vijana wa Dar es salaam walianzisha matamasha mengi yaliyokuwa yakihusisha vijana wenye vipaji vya kurap na kuimba. Vijana wengi wa Kitanzania walitumia muziki huu kuelezea matatizo yao ya kila siku kama vile ukosefu wa ajira na athari zake, dola na mambo yake, masuala ya mahusiano ya kimapenzi na nyinginezo.

Hapo zamani nyimbo ziliimbwa kwa kuwaiga wasanii wa Kimarekani kuanzia lugha hadi maudhui. Kwa mfano, Saleh Sabir mwanzoni mwa miaka ya 1990 katika kanda yake iitwayo Swahili Rap, alitumia mapigo ya muziki wa wasanii wa Kimarekani kama vile Vamilla Ice, Kriss Kross na Naught by Nature. Hali kadhalika, alitumia baadhi ya maneno na sentensi kutoka katika mashairi ya nyimbo hizo (Rernes 1998:320).

Mwishoni mwa miaka 1990, wanamuziki wengine wa Bongo Fleva walijitokeza kwa kasi. Baadhi ya wanamuziki waliomfuatia Salehe Jabiri ni Joseph Mbilinyi (Sugu), Joseph Haule (Prof J), Ballozi Dulla So, Nigger One, n.k. Maudhui ya maneno na sentensi zilizotumika zilitungwa na mwanamuziki wa Kitanzania. Kuanzia hapo uigaji wa maudhui, maneno na sentensi kutoka kwa wanamuziki wa Kimarekani kama vile kuigiza namna ya maisha yao magumu, ya kifukara, kujionyesha kwenye kivazi chao na chakula chao na hata malazi na makazi yao. Zaidi, ukajionyesha hata kwenye mapambano yao na nguvu za dola. Hali hiyo ikaakisi utamaduni wao wa kimapambano kwa wakati ule. Ukiangalia “graffit” kwa mfano, yalikuwa ni mapicha kwenye kuta, hususani kwenye njia za chini za reli (mafichoni), mapicha yaliyoelekezwa kwa tabaka tawala ulipungua. Muziki huu haukupokelewa vizuri na

Watanzania hasa watu wazima ambao waliuona ni muziki wa kihuni, kwa kuangalia uhusiano wake na Wamarekani weusi ambao uvaaji, uongeaji na hata uchezeji.

Joseph Haule (Professa J) akiwa na kundi lao "Hard Blasters" aliupa picha chanya muziki wa hip hop au Bongo Fleva na kubadilisha mitazamo ya baadhi ya watu baada ya kutoa wimbo uitwao "Chemsha Bongo" na hasa nyimbo zake mbili za "Ndiyo Mzee" na "Siyo Mzee" ambazo zilibadili sana mtazamo wa kuwa muziki huu hauongelei mambo ya kuwapotosha vijana, bali una hoja nzito zinazohusu jamii nzima.

Miaka ya hivi sasa muziki wa Bongo flava umekuwa na heshima kubwa katika jamii, kwani umekuwa ukitoa heshima kubwa katika jamii kwa kutoa mchango mkubwa katika kuwapatia ajira vijana. Vile vile umekuwa ukitumika katika kutoa elimu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu jamii kama vile kupinga rushwa, elimu ya UKIMWI, mapenzi na elimu kuhusu misingi ya uongozi bora.

2.2 Historia ya Hadithi Fupi

Utanzu wa hadithi fupi unahusishwa na mtunzi na mhakiki wa Kimarekani anayefahamika kama Edgar Alan Poe. Poe na Blander Mathew, wanasadikiwa kuwa ndio waasisi wa hadithi fupi. Blander inasadikiwa kuwa ndiye mtu wa mwanzo aliyetumia neno la Kiingereza la 'short story' (hadithi fupi) kwa mara ya kwanza. (Wamitila, 2002:66)

Mulokozi (1996:181) anasema hadithi fupi (visa) za Kiswahili zilivyochapishwa kwa lugha ya Kiswahili ni mkusanyiko wa hekaya na ngano kwa mfano Hekaya za Abunuwas (1928). Hadithi hizi zilikuwa ni za kimapokeo na ziliingiliana na fasihi simulizi. Anaendelea kusema hadithi fupi (visa) halisi za kwanza katika lugha ya Kiswahili zilianza kuandikwa kwenye magazeti kama vile Mambo leo, Mwafrika,

Nyota ya Afrika na Kiongozi katika miaka ya 1950 na vilianza kuchapishwa vitabuni miaka ya 1960 mfano *Mapenzi Kikohozi* kilichochapishwa na Longman 1994, Ruhumbika, G, *Parapanda* EALB 1974. Baadaye watunzi wengine walijitokeza kuandika hadithi zao magazetini kama Agoro Anduru na Eddie Ganzel.

Siku hizi kuchipuka kwa Magazeti ya Udaku kumeongeza wasomaji wengi wa hadithi fupi, hivyo watunzi pia kuongezeka kwa mfano, Erick Shigongo, Irene Ndauka, Ally Mbetu, Nyeno Chilongani kwa kuwataja wachache. Kwa hiyo utanzu huu umeendelea kukua sana kupitia magazeti ambayo husomwa kila siku na watu tofauti tofauti.

2.3 Muundo wa Hadithi Fupi

Hadithi fupi huundwa kwa sehemu kuu tatu ambazo ni mwanzo, sehemu kuu na mwisho.

Mwanzo

Kwa sababu utanzu huu una sifa ya ufupi, hivyo mwandishi hana uhuru wa kuandika mambo mengi. Katika sehemu hii mwandishi huelekeza moja kwa moja kwenye msuko wa hadithi. Mwandishi huandika maneno yale tu anayoyaona kuwa yanaweza kukuza dhamira kuu ya hadithi. Pia katika sehemu hii mwandishi anaweza akatoa uelekezi wa jumla wa hadithi yake. Kwa hiyo basi sehemu ya mwanzo ni mbegu ya hadithi nzima kama alivyowahi kusema mtaalamu wa fasihi Wamitila.

Sehemu kuu

Katika sehemu hii mwandishi huendeleza kwa upana dhamira ya hadithi yake. Hadithi fupi huwa na maneno ya muhimu tu ili kukuza dhamira kuu. Katika kupanua dhamira mwandishi hueleza kisa au tukio linalobeba hadithi yake ili kuwafanya

wasomaji waelewe nini mwandishi anakusudia wapate kupitia hadithi hiyo. Katika hehemu hii ndio ujumbe muhimu hupatikana.

Mwisho

Sehemu ya mwisho mwandishi hudhihirisha wazi wazi funzo lake. Ufumbuzi au utatuzi wa tatizo kuu katika msuko wa hadithi fupi unapatikana katika sehemu hii. Katika sehemu hii mwandishi hujaribu kutumia maneno machache kuhitimisha hadithi yake.

2.3.1 Sifa za Hadithi Fupi

Madumulla (2009:89) ananukuu sifa za hadithi fupi za Kiswahili kama alivyozitaja Mbunda Msokile kama ifuatavyo;

- Ni masimulizi ya kadhia (kisa/tukio/tuko) moja lililowekwa katika mazingira ya utamaduni wa lugha ya Kiswahili.
- Kadhia hiyo ielezwe kwa ufupi na isitumie wahusika wengi; mara nyingi mmoja au wawili.
- Hadithi fupi iwe na masimulizi ya kubuni, maana ya kubuni si kusema uongo, hadithi fupi ya kubuni ni kiwakilishi cha kisanaa kwa kutumia lugha.
- Hadithi fupi ya kubuni si picha ya maisha halisi, bali ni maisha yaliyosanifiwa, yaliyorembwa au kutiwa chumvi kwa shabaha maalum.
- Hadithi fupi ya Kiswahili inatakiwa iwe na msuko wamatukio tofauti na hadithi za kingano. Maelezo na mawazo muhimu yawe yamepangwa vizuri.
- Hadithi fupi ya Kiswahili haipaswi kuwa na mawanda mapana kwa namna yoyote ile.

- Hadithi fupi ya Kiswahili haina mchanganuo wa masimulizi na mandhari huwa si mapana.

Kwa ujumla naweza kusema kuwa sifa kuu ya hadithi fupi ya Kiswahili ni kusimulia jambo moja kwa kutumia maneno machache tofauti na riwaya na hutumia wahusika wachache. Kulingana na sifa hizi humfanya hata mwandishi au mtunzi kuwa na sifa ya ubanifu wa mawazo yake ili aweze kuufikisha ujumbe kwa wasomaji wake.

2.3.2 Maudhui

Hadithi fupi za Kiswahili hubeba maudhui sawa na yale ya tanzu zingine za Kiswahili kama vile kuburudisha, kuelimisha, kuonya na kuhifadhi amali za jamii. Hivyo basi hadithi fupi hujaribu kuzungumzia karibu matatizo yote yanayohusu mwanadamu. Mulokozi (1996: 182) anasema dhamira ambazo zinazojitokeza zaidi katika hadithi fupi za magazetini ni kuhusu mapenzi, matatizo ya ndoa, uhalifu, matatizo ya maisha ya mijini na vijijini, mgongano wa tamaduni na mara chache siasa na falsafa.

2.4 Maandiko Kuhusu Magazeti ya Udaku

Karugendo aliandika makala yake katika gazeti la Raia Mwema kuhusu Magazeti ya Udaku na jinsia. Katika makala hiyo mwandishi anaeleza namna watu wavyobeza Magazeti ya Udaku na anasema watu wanayabeza kwa kisingizio kuwa yana sifa mbalimbali, ikiwamo kutangaza uongo na hata umbeya. Anaendelea kusema pamoja na ukweli kwamba magazeti ya aina hii nchini yanasomwa na watu wengi, bado tunayadharau na kufikiri kwamba yanasomwa na watu wasiokuwa makini. Kuyabatiza magazeti haya kuwa ya udaku ni lengo zima la kutoa ujumbe kwamba haya ni magazeti ya umbea na uzushi.

Karugendo anasema katika makala hii kuwa karibia magazeti yote ya udaku kurasa zake za mbele zinapambwa na masuala ya jinsia. Mifano ya magazeti haya na habari zinazoandikwa ni nyingi, inahusu wanasiasa kushiriki ngono; mafumanizi, ufuska wa kupindukia na nyingine nyingi. Ingawa hapa ninatoa mfano wa habari katika magazeti machache tu, ukweli ni kwamba karibia magazeti yote ya udaku yanaandika mambo ya jinsia na yaliyo tofauti. Hakuna gazeti linalorudia yale yaliyoandikwa na gazeti jingine. Kila gazeti linajitahidi kuibua kitu kipya; Ukitaka kufahamu hali ya jinsia ilivyo katika taifa letu la Tanzania, soma Magazeti ya Udaku. (http://www.raiamwema.co.tz/magazeti-ya-udaku-na-jinsia#sthash.G07sCtnq.dpuf)

Hata hivyo, watu wengi wamekuwa na mwamko wa kuandika hadithi mbalimbali kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma. Hii pia inatokana na kuwapo kwa uwezekano wa kuchapishwa kazi za waandishi. Zamani uchapishaji ulikuwa ni wa mashaka. Maendeleo katika teknolojia, hasa matumizi ya ngamizi kwa upande mmoja, na kushamiri kwa biashara katika soko huria, kumesababisha wafanya biashara kujiingiza katika eneo hili la utoaji, uuzaji na usambazaji wa maandishi. Leo hii kuna wachapishaji wengi wa vitabu na magazeti. Katika magazeti, kuna zaidi ya magazeti 71 ambayo huandika hadithi fupi na mashairi. Baadhi ya hadithi fupi huwa na mfululizo wa matoleo ambao kwa kila toleo la gazeti kuna mwendelezo wa hadithi ileile. Hadithi fupi hujadili mambo ya muda mrefu na visa na mikasa ambayo imekuwapo katika jamii kwa kipindi kirefu. Hivyo waandishi mashuhuri na wengine wamejitokeza katika mfululizo wa aina hii, kama Eric Shigongo, Irene Ndauka na Faki A.Faki, Ally Mbetu ili kuhamasisha watu kubadilika kutoka katika fikra fulani ya kimaisha na kuhamia katika fikra fulani.

2.5 Mapitio Kuhusu Magazeti ya Udaku

2.5.1 Magazeti ya Udaku

Hushughulikia habari ambazo ni za kiumbeaumbea na ambazo, kwa kawaida, haziendani sana na urasmi. Gazeti la namna hiyo halisomwi sana na waugwana, bali ni uga maarufu wa watu wa kawaida, na hasa vijana.

Magazeti mengi ya udaku mara nyingi hayaandiki habari za maana zinazotakiwa na wasomaji wao, mara nyingi huandika habari zisizokuwa na ukweli na hata zikiwa na ukweli huziongezea chuku sana juu yake. Na mara nyingine magazeti haya utengeneza bifu au ugomvi katika jamii na kuwagombanisha watu hao maarufu na wapenzi wa kazi zao au wao kwa wao, au na jamii yao inayowazunguka.

Utafiti huu unalenga kuibua na kuweka bayana ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku katika jamii.

Sehemu hii inabainisha picha ya jumla kuhusu machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada hii.

Mandula (2008) alifanya utafiti juu ya matatizo yanayowakumba wanamuziki wa Bongo Fleva katika harakati zao za kujikwamua kutoka katika tatizo la ukosefu wa ajira. Yeye anauona muziki wa hip hop kama ni chanzo cha ajira halali kinachowasaidia vijana wa Tanzania kujikwamua kutoka katika tatizo hilo la ukosefu wa ajira.

Hata hivyo, utafiti wake umetofautiana na utafiti huu kwani utafiti huu, unachunguza ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku. Mandula amefanya utafiti juu ya wanamuziki wa Bongo Fleva katika

harakati za za kujikwamua kutoka katika tatizo la ukosefu wa ajira lakini hakuangalia nyimbo wanazotunga zinadhamira gani katika jamii.

Chachage (2002), ameandika juu ya utandawazi na migogoro ya kitamaduni Tanzania, na kusema kuwa wanaodhani muziki wa hip hop unaharibu utamaduni ni wa potofu wa mawazo, kwani utamaduni katika jamii ni mwingiliano wa mambo mengi kutoka ndani na nje ya nchi husika. Yeye anasema kuwa Fasihi ya Kiafrika na mtindo wake wa muziki vinaathiri hip hop. Alitoa mfano wa matumizi ya utani (*satire*) na misimu (*slang*) katika kuzungumzia maswala mbalimbali ya kijamii, kisiasa katika jamii.

Vile vile Fenn na Perrulo (2000) walifanya utafiti juu ya uchunguzi wa lugha unaofanywa na wanamuziki wa hip hop: Wao wanasema kuwa hali ya sasa ya mabadiliko ya kiuchumi na kijamii imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya muziki wa hip hop. Wanatumia Kiingereza na Kiswahili ili kufikisha ujumbe kwa hadhira pana: Kiingereza kinachukuliwa kama ni lugha ya kisiasa ya Kimataifa na Kiswahili kama lugha ya Taifa. Kutokana na malengo yao hawakuangalia kipengele cha dhamira, jambo ambalo mwandishi wa utafiti huu unakusudia kulifanya katika utafiti huu, hususani kwa kulinganisha dhamira za nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku.

Kwa upande wake, Mangesho (2003) alifanya utafiti wa muziki wa hip hop wa kisosholojia uliokuwa ukichunguza mambo yaliyochangia muziki wa Bongo Fleva kusambaa na kupata umaarufu miongoni mwa wakazi wa Dar es salaam. Utafiti ulionyesha kuwa mambo mengi yamechangia hilo kama vile kurekodi kwa kutumia ngamizi, kuanzishwa kwa vituo vya Redio vya FM ambavyo vilikuwa chanzo cha kurusha nyimbo hizo. Mathalani Radio One, Uhuru FM, Clouds, Times FM, nk.

Kumeanzishwa na kusambaa kampuni za kurekodi muziki kama vile Wananchi Stores, Bongo records, nk. Utafiti wa maegesho umesaidia kutupa historia ya muziki wa hip hop wa Tanzania lakini ulijikita zaidi katika mambo ya kisosholojia.

Zaidi ya hao, Omari (2001) anajadili kuhusiana na matumizi ya misimu katika muziki wa Bongo Fleva (BF) na anasema kuwa moja kati ya sifa zinazotofautisha Bongo Fleva na aina nyingine za muziki wa Kitanzania ni matumizi ya misimu. Anasema kwamba misimu ni lugha ya kificho inayozungumzwa na kundi fulani la watu katika jamii, kundi lenye watu wa kuwatenga au kuwafanya watu wengine wasielewe wanachotaka kukizungumza. Misimu inabadilika kulingana na wakati, kwahiyo kundi fulani la watu kwa wakati fulani wanazalisha aina fulani ya misimu yao.

Omari ameigawa misimu hiyo katika makundi sita, ambayo ni misimu inayohusu ulevi (*drug and alcohol slang),* misimu inayowahusu wanawake na sehemu zao za mwili (*woman and body part slang*), misimu ya mapenzi (*sexual and love slang*), misimu ya mavazi (*dress slang*), misimu inayohusu fedha (*money slang*), misimu inayohusu UKIMWI na ya kiume na kike ya kujikinga na magonjwa ya zinaa na ukimwi (*Aids and Condom slang*).

Utafiti wa Omari umetupa mchango mkubwa katika kuielewa hip hop ya Tanzania. Kupitia kazi hiyo tulipata mwanzo mzuri wa kuelewa lugha iliyotumika katika muziki wa hip hop na sababu zake.

Perullo (2003), alifanya utafiti juu ya aina ya muziki inayopatikana katika miji ya Tanzania, muziki kama vile taarabu, hip hop, ragae, mchiriku na ngoma. Yeye alifanya mahojiano na watu mbalimbali kama vile DJs, wanamuziki, watengenezaji,

na wasambazaji. Alikuwa na lengo la kutaka kujua njia wanazotumia katika kuwarekodi, kuzalisha, kusambaza, kuuza na kucheza muziki. Aligundua kuwa kuna njia mbalimbali zinazotumiwa na watu hao ili kukabiliana na mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa Tanzania. Kati ya njia hizo kuna utumizi wa rushwa, uchawi, wizi na ushirikina kati yao na ndugu, jamaa na marafiki.

Gitonga na Onesmus (2011) wamefanya utafiti katika tasnifu ya hadithi kwa kuchunguza athari ya dhamira katika uteuzi wa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Wametumia diwani nne za mwaka wa 2007. Diwani hizo ni *Damu Nyeusi, Likizo ya Mauti, Kurudi Nyumbani, Alidhani Kapata* na hadithi nyingine. Malengo ya tasnifu hii yalikuwa ni kuainisha maswala yanayoshughulikia waandishi wa hadithi fupi za 2007 katika diwani zao, kudhihirisha dhamira katika hizo hadithi, kubainisha ni vipi dhamira hizo zinavyouathiri uteuzi wa mitindo wanayoitumia kuziwasilisha, na mwisho kuangalia jinsi ambavyo mazingira huathiri utunzi wao.

Joseph L.Mbele (1999), alifanya uchunguzi katika lugha ya Kimatengo kwa kujumuisha tafsiri za hadithi kumi alizorekodi katika miaka ya sabini. Kila hadithi imefuatiwa na uchambuzi, ambao aliandika ili kufafanua yaliyomo na kueleza undani wa hadithi na umuhimu wake.

A.K Mulewa (2011), amefanya utafiti katika hadithi fupi za Kiswahili. Ametumia diwani tatu za hadithi fupi, *Kicheko cha Ushindi* (1978), *Pendo la Heba* (1996), *Mayai Waziri wa Maradhi* (2004) pamoja na hadithi nyingine. Malengo ya tasnifu hii yalikuwa ni kuchunguza sifa za wahusika wa hadithi fupi, kuonyesha na kuelezea mbinu za usawiri wa wahusika katika hadithi fupi na kukadiria ni kwa kiasi gani mbinu hizi zinavyoweza kuwasawiri wahusika katika ukamilifu wao.

2.6 Mapengo Yaliyojitokeza

Katika mapitio yetu, tumeona kuwa kuna waandishi na wataalamu mbalimbali wa Fasihi na walioandika kuhusiana na muziki wa Bongo Fleva na hadithi, hususani katika masuala mbalimbali ambayo yanahusu jamii na muziki huu wa Bongo Fleva na hadithi. Wapo walioandika kuhusu matatizo yanayowakumba wanamuziki wa Bongo Fleva, wengine wameeleza juu ya utandawazi na migogoro ya kitamaduni kama alivyofanya Chachage. Wapo walioandika juu ya uchanganuzi wa lugha unaofanywa na wanamuziki wa Bongo Fleva, kama vile Fenn na Perollo. Wapo waliofanya utafiti wa kisosholojia uliochangia muziki wa Bongo Fleva kusambaa, kama vile Mangesho. Omari alifanya juu ya matumizi ya misimu katika muziki wa Bongo Fleva, aidha wapo waliofanya juu ya aina ya muziki inayopatikana katika jamii ja Tanzania. Kwa upande wa hadithi, wapo waliofanya kwa kuchunguza athari ya dhamira katika uteuzi wa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili; wapo waliofanya juu ya uchanganuzi katika lugha ya Kimatengo kwa kujumuisha tafsiri za hadithi kumi zilizorekodiwa. Ila, miongoni mwa mapitio yetu, hakuna hata moja linalojihusisha na ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku.

2.6.1 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa

Katika tafiti zote zilizofanyika hapo awali kuhusu nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku hakuna utafiti ambao uliwai kufanywa kuchunguza kwa kina kuhusu ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku hususani katika tungo zao, kwa wasanii teule na waandishi teule ambae tulidhamiria kuwazamia katika kipengele hicho. Pia tulidhamiria katika utafiti huu kuchunguza ulinganishi wa kidhamira katika nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku kama unafanana au kutofautiana katika kazi zao.

SURA YA TATU

USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sehemu hii inafafanua mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, zana na mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data, mchakato wa kukusanya data pamoja na mbinu zilizotumika katika uchambuzi wa data.

3.1 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika, uwandani na maktabani kwa njia na maelezo au ufafanuzi; uwandani watafitiwa walipewa hojaji zilizowaongoza kunukuu data kwenye makabrasha (Baradyana na Ame, 2007: 65). Mbinu iliyotumika katika mchakato wa kukusanya data ni mahojiano na mapitio mbalimbali ya vitabu kutoka maktaba, pamoja na nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku. Data zilikusanywa kutoka katika maandiko mbalimbali yanayoelezea muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Vilevile nyimbo hizo na hadithi hizo zilipatikana kutoka kwenye nyimbo za **Diamond, Lady Jay dee, Linex, Niki wa pili** na **Professa J** na Magazeti ya Udaku yanayoandika hadithi za **Irene Mwamfupe Ndauka na Ally Mbetu** kama vile **Uwazi, Ijumaa, Risasi** na **Kiu**. Niliwachagua wanamuziki hao kwa sababu wanafahamika katika jamiii na kazi zao nyingi zinapendwa na wanajamii wengi na wana mashabiki wengi katika jamii na nimetumia nyimbo moja tu kutoka kwa kila mwanamuziki katika nyimbo zao, ili kuona tofauti za dhamira zao katika jamii. Vile vile nilichagua hadithi za Irene Mwamfupe Ndauka na Ally Mbetu kwa kuwa ni waandishi maarufu hapa Tanzania na wametunga hadithi nyingi zenye visa mbalimbali. Data mbalimbali zilizozokusanywa zimehakikiwa, kuchanganuliwa na hatimaye kufafanuliwa kwa kina. Mwelekeo wa utafiti huu ni wa kiufafanuzi hivyo, haukujihusisha kabisa na

taarifa za kitakwimu. Aina hii ya utafiti wa kiufafanuzi ambao aghalabu hutumia mbinu za maelezo, ulinganisho, pamoja na uhusishaji wa data zake na kutolea matokeo. Hivyo, ukusanyaji, uchanganuzi wa data, pamoja na utoaji matokeo ya utafiti huu uliegemezwa katika mbinu hii. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu zilitarajiwa kuwa ni za maktaba na kuzihusisha na taarifa za uwandani.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ambao, kwa kiasi kikubwa, ni wa kimaktaba ulifanyika katika jiji Dar es salaam, hasa kuhusiana na data za uwandani. Data za maktabani zilipatikana katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Maktaba ya Taifa iliyoko jijini Dar es salaam. Sababu za kuchagua mji wa Dar es salaam ni kutokana na kuwepo kwa wanamuziki hawa teule wote na waandishi wengi wa hadithi walipatikana katika mji wa Dar es salaam ambao wameweka makazi yao ya kudumu katika mji huu. Hali kadhalika, kuna soko la uhakika wa kazi zao, kumbi za kisasa, wasomaji wengi wa Magazeti ya Udaku, kuwepo kwa matukio mengi ya kijamii na kuwepo kwa vyombo vingi vya habari, wahariri na wachapaji wengi, pamoja na studio mbalimbali za kisasa kwa ajili ya kurekodi kazi zao za muziki na sehemu nyingi za uchapaji wa hadithi hizo.

Vilevile mji huu mkubwa nchini Tanzania una wasikilizaji, wachambuzi, waandishi na wahakiki wengi wa muziki wa Bongo Fleva, wakiwemo na watangazaji, waandaaji wa vipindi mbalimbali vya redio, televisheni na magazeti vinavyohusu muziki huu wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku.

3.3 Walengwa wa Utafiti

Utafiti huu umegawanywa katika makundi manne ambayo ni nyimbo za Bongo Fleva, hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, mashabiki wa nyimbo za Bongo Fleva, na

wasomaji wa hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Hawa walitoa taarifa mbalimbali kuhusu Bongo Fleva na dhamira zake katika jamii na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku na dhamira zake katika jamii.

3.3.1 Wago Tafutiwa

a) Nyimbo mbalimbali za muziki wa Bongo Fleva, ya Diamond, Lady Jay Dee, Linex, Nick wa Pili na Professor Jay na hadithi za Magazeti ya Udaku zilizotungwa na waandishi Irene Mwamfupe Ndauka na Ally Mbetu. Hizi zilisaidia kuchunguza ulinganishi wa kidhamira katika nyimbo hizo na hadidhi hizo.

b) Wananchi wa Dar es salaam wa marika na jinsia mbalimbali (ambako kwa kiasi kikubwa muziki huu ndio unasikilizwa na magazeti hayo ndiyo yanayosomwa kwa wingi). Hawa walitarajiwa kutoa taarifa za ulinganishi wa kidhamira kati ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku katika tungo za wasanii teule na waandishi teule.

3.3.2 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa. Hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi wa kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti wake (Barayana na Ame, 2007; Kothari, 2009; Mason, 2010). Wawakilishi hao walichaguliwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti huu na walichaguliwa kutoka katika makundi yote. Vigezo vikubwa vilivyotumika katika kuwapata ni vitatu:

a) Nyimbo tano za Bongo Fleva, kutoka kwa Diamond, Lady Jay Dee, Linex, Nick wa Pili na Professor J. Na hadithi mbili kutoka Magazeti ya Udaku (***Kiu na Uwazi***). Nyimbo hizi zilipatikana kutoka kwenye nyimbo zao walizotunga

tofautitofauti na kuandika mmoja na hadithi zilipatikana kwenye Magazeti ya Udaku. Zilichungunzwa kwa namna ya jumla kwa lengo la kutaka kujua kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa ulinganishi wa kidhamira katika kazi hizo. Sifa zilizosababisha wasanii hao kuteuliwa ni kutokana na kazi zao na uzoefu wao katika muziki wa Bongo Fleva, pamoja na utunzi wa nyimbo zao kwa vipindi tofauti, pia magazeti hayo ya udaku yalianza siku nyingi kuandika hadithi za vichwa vya habari mbalimbali. Mwandishi alichunguza hadithi za miaka ya hivi karibuni ili kuendana sawa na nyimbo za hivi karibuni, kwakuwa hadi leo nyimbo nyingi na hadithi nyingi hazina mashiko kwa baadhi ya watu kama vile viongozi wa dini, wanasiasa na watu wa makamo.

b) Wasikilizaji wa nyimbo za Bongo Fleva na wasomaji wa hadithi za magazetini. Watu hawa walipatikana kwa njia ya mahojiano, na taarifa zilizohitajika kwao ni jinsi gani wanaupokea muziki wa Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku na dhamira zake ni zipi haswa katika jamii. Kulikuwa na idadi ya watu 40, watu wazima kumi(10), vijana kumi(10), wanafunzi sita(6) na viongozi wa dini na wakiserekali wa nne(4).

c) Wanachuo mbalimbali (10) waliosoma na kusikiliza kazi mbalimbali za wasanii na waandishi wa hadithi fupi.

3.4 Ukusanyaji Data

Sehemu hii inaelezea njia na zana mbalimbali zilizotumika kukusanyia data, pamoja na mchakato wa kukusanya data.

3.4.1 Njia na Zana za Kukusanya Data

Njia kuu zilizotumika kukusanya data za utafiti ni udurusu wa maktabani, magazeti na usikilizaji wa siidii, usaili na mjadala wa vikundi. Zana zilizotumika ni mwongozo wa udurusu, mwongozo wa usikivu, mwongozo wa usaili, mwongozo wa mjadala wa vikundi, madaftari, kalamu na kinasa sauti.

3.4.1.1 Udurusu wa Kimaktaba

Ni utaratibu ambao unahusisha kwenda maktabani kudurusu na kupitia maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti. Miongoni mwa maandiko yaliyopatikana maktabani kwaajili ya udurusu ni kama vile tasnifu mbalimbali zinazohusu dhamira zilizopo ndani ya muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku, majarida, miziki, magazeti pamoja na vitabu vinavyohusiana na mada ya utafiti.

3.4.2 Mchakato wa Ukusanyaji Data na Uthibiti Wake

Utafiti huu ulizingatia maadili yaongozayo mchakato wa utafiti. Masuala kama vile uombaji wa ridhaa ya watafitiwa, utanzu wa siri za taarifa na ufichwaji wa majina ya watoa taarifa. Mwongozo huu ulitumika katika kusoma magazeti na kusikiliza muziki. Data zilikusanywa kwa njia tatu ambazo ni usaili, mjadala wa vikundi, usomaji hadithi magazetini na usikilizaji wa nyimbo za Bongo Fleva.

Mwongozo wa usaili ulitumika kuwasaili wasomaji wa hadithi fupi na wasikilizaji wa muziki wa Bongo Fleva. Njia hii ya usaili, kama asemavyo Kothari (2009), hurahisisha upataji wa data kutoka kwa watu hata kama hawawezi kusoma na kuandika katika mziki wa Bongo Fleva. Pia, huruhusu upatikanaji wa taarifa za kina kutokana na kumruhusu mtafiti kusaili vipengele vya nyongeza. Mwongozo wa mjadala wa vikundi ulitumiwa kwa watu wa rika zote. Mtafiti aliongoza mjadala kuhusu mziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti (namna waichukuliavyo

na dhamira zake) katika jamii. Mwongozo wa usomaji hadithi magazetini na usikilizaji wa nyimbo za Bongo Fleva ulifanyika kwa kusoma kipengele cha hadithi na kusikiliza muziki wa Bongo Fleva. Daftari na kalamu zilitumika kunukuu data zilizopatikana katika mahojiano na wakati wa kudurusu katika uchambuzi wa data. Pia, magazeti, siidii, na kinasa sauti vilitumika kuwarekodi wasailiwa na kupiga picha na vielelezo mbalimbali vihusianavyo na utafiti huu.

3.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya upokezi/mwitikio wa msomaji. Data zilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ambayo yamebainishwa hapo awali kuhusu utafiti huu. Data zilizopatikana uwandani kupitia njia za usaili na majadiliano ya vikundi zilichanganywa na kuwianishwa na zile zilizopatikana kutokana na udurusu wa kimaktaba kisha kupimwa na kutadhiminiwa. Baada ya uchanganuzi huo, matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ambayo yalitumika kwa kiasi kikubwa.

3.6 Uhalali na Uthibiti wa Matokeo ya Utafiti

Ponera (2014) anafafanua kuwa uhalali wa utafiti maana yake ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Nakuhusu uthabiti wa utafiti, ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayoendanana ikiwa utafiti utafanyika katika wakati mwingine, mahali pengine, au na mtu mwingine. Ni vigumu kwa utafiti kuwa na matokeo thabiti ikiwa uhalali utakosekana (Kothari, 2009). Uhalali wa matokeo ya utafiti huu ulitarajiwa kuthibitishwa kwa kutumia mbinu zifuatazo: Kwa kuweka bayana malengo na mipaka ya utafiti. Pili, kwa kutumia lugha nyepesi na yenye kueleweka katika kukusanya data ili sampuli isipate taabu kuelewa kinachotafitiwa; na hivyo kutoa

majibu yanayohusiana na malengo ya utafiti huu. Tatu, kwa kutumia njia nne za kukusanyia data (hojaji, usikivu, udurusu pamoja na mjadala wa vikundi lengwa). Kwa kutumia mbinu hizi matokeo yamekuwa na kiwango kikubwa cha udhibiti. (Ponera, A 2014).

3.7 Vikwazo vya Utafiti na Utumizi Wake

a) Upungufu wa fedha za kugharimia shughuli mbalimbali kama vile ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data, uunganishaji, uandishi wa ripoti, uhariri wa ripoti na usambazaji wa matokeo ya utafiti. Kikwazo hiki kimetatuliwa kwa kuomba mkopo kutoka asasi ya kifedha.

b) Ugumu wa watafitiwa kutoa taarifa. Kikwazo hiki kimetatuliwa kwa kuwaelimisha watafitiwa umuhimu wa kutoa taarifa sahihi za utafiti na faida za utafiti walioupata wao binafsi na jamii kwa jumla.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni kubaini msukumo wa watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, kubainisha dhamira zinazopatikana katika kazi hizo na kulinganisha dhamira za Bongo Fleva na hadithi fupi za magazedti ya udaku, na mwisho, ni muhtasari wa sura.

4.1 Msukumo wa Watunzi wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti Ya Udaku.

4.1.1 Msukumo wa Watunzi wa Nyimbo za Bongo Fleva

Katika utafiti huu, inaonyesha kuwa watunzi wengi wa nyimbo za Bongo Fleva wanapata misukumo mingi kutoka katika jamii inayowazunguka ama huguswa na hisia fulanifulani katika jamii zao, au matatizo yanayozikumba jamii zao hadi kufikiwa kutunga nyimbo hizo. Asilimia kubwa ya nyimbo wazitungazo zinahusu mambo au matatizo yanayojitokeza katika jamii kwa jumla, kama vile mapenzi, siasa, chuki, fitina, umasikini, majanga ya kijamii na hata ushirikina. Lakini misukumo hii imebebwa na dhana kuu nne, ambazo ni fedha, mapenzi, siasa na majanga:

a) **Fedha**

Suala la fedha au pesa limeonekana kuwa ni msukumo mkubwa sana kwa wasanii wengi. Wasanii wengi wanajitokeza katika fani hii au katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za Bongo Fleva kama ajira yao ya kujipatia kipato cha kila siku kinachowawezesha kujikimu na maisha ya kila siku. Ndiyo maana vijana wengi wamejikita katika muziki huu ili kujipatia kipato. Wengine

huonekana kutunga nyimbo zenye maudhui mepesi au ujumbe mchache katika maisha, ili tu hatimaye wajipatie fedha ijapokuwa kidogo.

b) Mapenzi

Suala lingine linalotoa msukumo mkubwa kwa watunzi katika kutunga na kuimba nyimbo ni suala la mapenzi. Suala la mapenzi limetawala sana katika dunia ya leo, ambapo kila kukicha watu wanazungumzia mapenzi: si wazee, si vijana, wala watoto; kila mtu huzungumzia juu ya mapenzi. Mapenzi hayo nayo wameyagawanya katika sehemu kuu mbili, yaani mapenzi ya dhati na mapenzi ya udanganyifu.

i) Mapenzi ya dhati

Mapenzi ya dhati ni mapenzi ya kweli ya kutoka moyoni, huwa hayaangalii mali, elimu, fedha, dini wala kabila. Watu hupendana wao kama wao na siyo kwa sababu ya kitu fulani. Lakini watunzi wachache sana huwa wanazungumzia mapenzi haya ya dhati, maana hutokea kwa watu wachache sana katika jamii zetu.

ii) Mapenzi ya udanganyifu

Haya ni mapenzi yasiyo ya dhati; yamejaa chuki, tamaa, fitina, kejeli, dharau na masimango. Haya ni mapenzi ambayo watu wanapendana kwa sababu ya kitu fulani kama vile mali, fedha ama elimu. Pia, ni mapenzi ambayo yanakuwa na ahadi nyingi, lakini mwishowe zile ahadi hazitekelezeki na huishia njia panda; ni mapenzi ambayo hayana malengo. Mapenzi ya udanganyifu ndiyo yametawala sana katika jamii zinazotuzunguka na ndiyo huimbwa sana na watunzi na waimbaji wengi wa nyimbo za Bongo Fleva.

c) Siasa

Suala lingine linaloonekana katika jamii kuwapa msukumo wasanii wengi katika kutunga na kuimba nyimbo zao ni lile la siasa. Swala hili pia linaonekana katika nyimbo za wasanii, japo kuwa siyo kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya wasanii wameguswa na wanasiasa katika kampeni zao na hata ahadi zao zisizo na ukweli kila siku katika jamii kwa njia ya kujinufaisha wao wenyewe na familia zao tu. Hivyo, huamua kutunga nyimbo zinazowagusa na kuwafungua macho wananchi juu ya viongozi hao.

d) Majanga

Haya ni baadhi ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii, kama vile, umasikini, maradhi, ukame, ushirikina, ukosefu wa ajira, ugumu wa maisha, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi, kutokupendana na kuwekeana chuki kati ya mtu na mtu, kati ya mtu na watu, na kati ya jamii na jamii. Mambo haya pia yanaonekana kugusa jamii tunayoishi, hivyo huwapa msukumo watunzi na waimbaji wa nyimbo za Bongo Fleva katika kutunga kazi zao.

4.1.2 Nyimbo Teule za Wanamuziki wa Muziki wa Bongo Fleva

4.1.2.1 Wimbo wa Linex – Mama Halima

Mtunzi na mwandishi wa wimbo huu anaonekana aliutunga kuhusu mapenzi yaliyojaa udanganyifu na usaliti. Msanii anaonyesha kuwa walikubaliana na mpenzi wake kutokana na ugumu wa maisha aende akatafute ili akipata arudi waje waoane. Lakini alipoondoka kwenda kutafuta mpenzi wake alipata mwanaume mwingine na kuwa naye kimapenzi, jambo lililosababisha huyo mpenzi wake kushika ujauzito. Wakati yeye anafika, alikuta mpenzi wake amemsaliti na tayari ni mjamzito.

> *“Nilivyokuacha na nilivyokukuta ni tofauti tofauti kabisa, sitaki kugombana na wewe niambie nini kilikukuta inaonyesha na iko wazi una mimba ya miezi sita; kama unavyojua sijawahi kutembea na wewe kama unavyoelewa lakini mpaka nikuoe, mi kwako ulinidanganya utanipenda kwa moyo wote. Mama Halima wee umesahau ahadi ni deni”*

Mtunzi anaonekana alipata msukumo wa mapenzi ya udanganyifu, akaamua kutunga wimbo huu unaohusu mapenzi ya udanganyifu.

4.1.2.2 Wimbo wa Diamond - Safari

Mtunzi wa wimbo huu alitunga kutokana na msukumo wa mapenzi ya dhati. Katika jamii zetu kuna watu wenye mapenzi ya dhati, ila wanakabiliwa na changamoto ya umasikini katika mapenzi yao au familia zao. Hivyo, mwandishi alisukumwa kwa kuangalia mapenzi haya na kuonyesha suluhisho la umasikini na kutaka kuieleza jamii kuwa inawezekana katika familia kukaa chini kama wapenzi na kuamua jambo litakalosaidia familia hapo baadaye. Kwa suala la mapenzi ya dhati msanii ameonyesha

> *“Unapoenda kama ukifika salama utukumbuke na sisi, usisahau kama mkeo na wana umetuacha na dhiki. Hilo usijali, ila naomba chunga sana ogopa na marafiki wakikulaghai hata kwa mbegu za mtama, waambie sidanganyiki”*

Inaonyesha mapenzi ya dhati maana kila mmoja anamsihi mwenzake asifanye baya litakalohatarisha mapenzi yao. Na katika umaskini mwandishi anaonyesha kipengele cha;

> *“Ahh vipi mizigo ushaweka tayari, nisije chelewa nikajaachwa na gari, basi jikaze usilie mpenzi mi nitarudi niombee kwa Mwenyezi, aaaa zile taabu na njaa msimu mzima, mavuno hakuna huwa nakosa raha pale mnapokosa cha kutafuna roho yangu inaniuma sema nitafanya nini na pesa sina na kuonea na huruma bora niende mjini kusaka Tumaa”*

Mtunzi anaonyesha kuguswa na swala la umasikini katika familia lakini pia anaonyesha ufumbuzi wa tatatizo hilo.

4.1.2.3 Wimbo wa Lady Jay Dee - Nasimama

Msanii wa wimbo huu anaonekana kuguswa au kusukumwa na mambo yanayojitokeza katika jamii kama vile chuki, fitina, masimango na umbea katika jamii. Kuna watu ambao hawapendi kuona maendeleo ya wengine, hawapendi kuona watu wakipendana, wengine wanajifanya wema kwa watu kumbe ni wanafiki wamejaa chuki, fitina na masimango kwa wengine. Hivyo msanii anatoa angalizo kwa jamii kuwa makini na watu wanaozunguka watu wengine, maana huwezi kumjua mwema.

> *"Ukitazama kwa macho yako huwezi kumjua mwema mateso yako furaha yao tena mengi watasema, moyo wa mtu kichaka mengi yalofichika, naye mdhania mwema kumbe mchawi kwako"*

Msanii ameguswa pia na kuamini Mungu yupo na hakuna chochote kitakachoshindikana kwake.

> *"Nasimama na mola kwa kila jambo lile ntendalo"*

4.1.2.4 Wimbo wa Nikki wa Pili akishirikiana na Ben Pol – Sitaki Kazi

Msanii wa wimbo huu amepata msukumo wa kupambana na maisha au wa kuondoa dhana ya vijana wengi wanaosubiri kuajiriwa na serikali au shirika ndipo wajipatie kipato. Anawaeleza kuwa siyo mpaka waajiriwe ndipo waweze kujikimu kimaisha, wanatakiwa kugundua vipaji vyao na kujiajiri wenyewe kwa kutumia vipaji hivyo. Anaona kuajiriwa ni kuwa kama mtumwa maana lazima ufanye yale bosi au mkuu wako anayotaka tu, na siyo vinginevyo. Anaonyesha kuwa yeye amesoma na ana Shahada ya Uzamili, lakini amejiajiri maana hawezi maisha ya kitumwa. Anawashangaa vijana wanaosubiri kuajiriwa tu huku wana elimu nzuri, vipaji na nguvu.

> " *Utamaduni wangu nikuuliza why why why why; Nimekataa kuwa mtumwa najituma, eeee form six degree hadi masters sitaki kazi, elimu sio vyeti nachoma, sitaki kazi. Wana vyeti mtaani vijana, hawana kazi. Natengeneza ajira mtaa niupe kazi"*

Anasisitiza kuwa hata walioajiriwa kila siku wana wasiwasi na maisha yao huenda wakafukuzwa kazi wakati wowote, lakini yeye aliyejiajiri mwenyewe hana mashaka.

4.1.2.5 Wimbo wa Professa Jay aliyemshirikisha Juma Nature na Babu Ayubu – Ndiyo Mzee

Wimbo huu ni wakisiasa. Msanii ameguswa na wanasiasa na vibaraka wao wanaowafanyia kampeni ili washinde katika chaguzi zao. Msanii ameonyesha ni jinsi gani wanasiasa wanavyotumia nafasi zao vibaya katika kuwadanganya wananchi wao kwa kutoa ahadi nyingi zisizo na ukweli wowote na mwishowe wanashindwa kuzitekeleza.

> *"Okk naitwa ndugu Joseph haule nadhani nimeletwa niokoe hiki kizazi mimi ni mwanasiasa niliyebarikiwa na Mungu, nimeletwa kwenu ili niwapunguzie machungu"*.

Anaonyesha jinsi wanasiasa wanavyojua kujinadi katika majukwaa, lakini si watekelezaji. Pia anaonyesha jinsi wananchi wanavyotakiwa wawagundue wanasiasa wa aina hiyo na kuwanyima kura, maana ni waongo na wadanganyifu, na wanataka kujinufaisha wao wenyewe na familia zao tu.

> *"Nyie ndugu zangu huyu msimpe uongozi sio mzuri muongo tu mnafiki na kiburi si mzuri, anaongopea sana".*

4.1.3 Msukumo wa Watunzi na Waandishi wa Hadithi Fupi wa Magazeti ya Udaku

Katika utafiti huu, inaonyesha kuwa watunzi wengi wa hadithi fupi wa Magazeti ya Udaku wanapata misukumo mingi katika jamii inayowazunguka ama huguswa na hisia fulanifulani katika jamii zao, au matatizo yanayozikumba jamii zao hadi

kufikia kutunga nyimbo hizo. Asilimia kubwa ya hadithi hizi wazitungazo zinahusu mambo au matatizo yanayojitokeza katika jamii kwa jumla, kama vile, siasa, chuki, fitina, umasikini, majanga ya kijamii, na hata ushirikina. Lakini misukumo hii imebebwa na dhana kuu nne, ambazo ni fedha, mapenzi, siasa na upelelezi.

a) Fedha

Waandishi wengi wa hadithi fupi na ndefu, wanaonekana kujituma sana katika uandishi kwa ajili ya kujipatia kipato au fedha ili kukidhi mahitaji yao. Suala la fedha limekuwa changamoto kubwa katika jamii, hivyo kila mtu anajituma awezavyo ili kujipatia kipato katika maisha. Hivyo suala hili limeibua waandishi wengi katika tasnifu hii, ili tu kujipatia kipato cha kukidhi mahitaji ya kila siku.

b) Mapenzi

Suala la mapenzi limechukua nafasi kubwa sana katika jamii. Hivyo, linasababisha waandishi wengi kujikita sana katika uandishi wa suala la mapenzi, na kusahau mambo mengine yaliyomo katoka jamii. Suala hili limegawanyika katika makundi mawili, yaani;

i) Mapenzi ya dhati

Mapenzi ya dhati, haya ni mapenzi ya uaminifu na ya kutoka moyoni. Hayaangalii sura, umri, kabila wala kipato. Ni mapenzi yanayojali utu na siyo kitu, mapenzi haya hutokea mara chache sana na kwa watu wachache.

ii) Mapenzi ya udanganyifu

Haya ni mapenzi ya kimaslahi zaidi, hayaangali sura ya mtu bali yanaangalia una nini mfukoni. Ni mapenzi yaliyojaa chuki, fitna, kejeli, na masimango. Waandishi

wengi hupenda sana kuandika mapenzi haya, kwa kuwa ndiyo yaliyotawala katika jamii zetu.

c) Siasa

Waandishi wa Magazeti ya Udaku, pia wameonekana kuguswa na suala hili la siasa katika jamii. Wamejaribu kufichua masuala mengi yanayojitikeza ndani ya siasa, na kuonyesha baadhi ya wanasiasa wanavyojali maslahi yao wao na familia zao na kusahau maslahi ya jamii. Japo sio wengi sana wanaozungumzia sana maswala ya siasa.

d) Majanga

Suala la majanga, pia limeonekana kushika mashiko makubwa kwa waandishi wa hadithi fupi katika Magazeti ya Udaku. Mambo haya ya umasikini, ushirikina, ukame, maradhi na chuki yameonekana kuandikwa sana na waandishi wengi wa hadidhi fupi katika Magazeti ya Udaku, kwa kuwa ni mambo ambayo yapo na yanayosumbua sana jamii.

e) Upelelezi

Hili ni suala lingine linalowapa msukumo waandishi na watunzi wa hadithi fupi katika masuala ya uandishi. Kumezuka mambo mengi ya kivita, kijambazi na kutekwa katika jamii nyingi mbalimbali, na swala hili limekuwa kero katika jamii nyingi na kusababisha mamia ya watu kupoteza maisha, kupoteza baadhi ya viungo vya mwili, kupoteza watoto, ndugu, jamaa na marafiki, ambapo watoto hubaki yatima na wengine kufungwa na kuteseka bila sababu.

4.2 Wateuzi Teule na Watunzi wa Hadithi Fupi katika Magazeti ya Udaku

4.2.1 Hadithi ya Godoro la Mtumba, iliyotungwa na kuandikwa na Irene Mwamfupe Ndauka.

Hii ni hadithi fupi inayogusa maisha ya wanadamu au ya jamii kwa jumla, ni vitu ambavyo vinatokea katika jamii tunazoishi. Hadithi hii inaitwa **"Godoro la Mtumba"**. Ni hadithi yenye kusisimua na yenye mafundisho ndani yake, kuhusu mapenzi. Mapenzi ni dhamira kubwa sana iliyojitokeza katika kitabu hiki, na ni kitu kizuri katika maisha ya binadamu, ila kikitumika vibaya kinaweza kuleta madhara makubwa sana kwa wapenzi, rafiki, ndugu, jamaa na jamii kwa jumla.

Hadithi hii inahusu ndugu wawili waliojikuta wakiingia katika swala la mahusiano ya kimapenzi na kusahau kuwa wao ni ndugu wa karibu sana. Mjomba msafiri aliamua kumshawishi na kumlaghai mjomba wake Zuwena ili wawe wote kimapenzi baada ya kumuona Zuwena amekua na anavutia kimapenzi. Pia aliamua kumuacha mpenzi wake Zuhura Chachandu ili wapate muda wa kuwa pamoja na Zuwena. Zuwena ni mtoto wa dada yake Msafiri. Zuwena baada ya kumaliza darasa la Saba katika Shule ya Msingi Usagara alikosa nafasi ya kuendelea na masomo, ndipo mjomba wake alipomchukua kwa nia ya kumuendeleza. Alimchukua mwaka mmoja mbele baada ya kutengana na mke wake. Alimtafutia sekondari ya binafsi iliyopo maeneo ya Ubungo Kibangu na kuanza masomo. Mjomba wake alikuwa na kazi nzuri yenye maslahi makubwa, hivyo aliajiri msichana wa kazi na mlinzi, lakini baada ya muda aliwaondoa watu hao na kujikuta wakiishi yeye na Zuwena tu katika nyumba hiyo.

Zuwena alipofika Kidato cha Tatu, ndipo mjomba Msafiri alipoamua kuvunja ukimya na kumshawishi Zuwena kuingia katika mahusiano ya kimapenzi.

Alifanikiwa kumteka kiakili kwa kuwa alikuwa ni binti mdogo na hakuwahi kukutana na mwanaume yeyote kimwili toka atoke tumboni mwa mama yake. Zuwena alipoingia katika mchezo huo, akajikuta ananogewa. Jina la mjomba likafa, na kujikuta akimuita mjomba wake majina ya kimapenzi kama vile mpenzi, honey, baby, sweet, na mengineyo. Uwezo wake darasani ulipungua na kujikuta akiingia tena katika mahusiano na walimu wa kiume na wanafunzi kwa lengo la kusaidiwa kimasomo na kuwafahamu wanaume wengine zaidi. Walinogewa na mapenzi na kujikuta wakati mwingine Zuwena haendi shule, wala Msafiri haendi kazini.

Mama yake Zuwena alikuwa akiota ndoto mbaya juu ya Zuwena na mdogo wake Msafiri. Hivyo, aliamua kufunga safari kutoka Tanga kwenda Dar es Salaam kuwatembelea. Baada ya kufika huko, aligundua kuwa kuna mchezo unaoendelea kati ya Zuwena na Msafiri. Aliamua kuendelea kukaa na kufuatilia kwa kina nyendo zao, na baada ya muda alipata ukweli. Zuwena na Msafiri walinogewa na mapenzi na kutojali kuwa mama Zuwena yupo. Zuwena alikuwa akitoroka usiku kutoka chumba alicholala na mama yake na kwenda kwa mjomba wake. Mama alimtafuta mara kadhaa, lakini walimdanganya kwa maneno mengi. Waswahili wanasema, za mwizi ni arobaini. Hatimaye, siku hiyo mama Zuwena aliwakuta wakiwa kitandani kwa Msafiri, tena watupu kama walivyozaliwa.

Baada ya fumanizi hilo walikosa cha kujitetea tena. Mama baada ya kupata ukweli, aliamua kuondoka na kuwaachia maneno makali ya laana juu yao na pia akaenda kuwaambia ndugu. Huku nyuma, Zuwena na Msafiri waliendelea na mapenzi, huku Zuwena akitaka wafunge ndoa ili wawe mke na mume kama Msafiri alivyomuahidi siku za nyuma. Dakika za mwisho, waligundua walichokifanya siyo kizuri kwa ndugu na hata kwa jamii kwa jumla. Waliamua waende Tanga kuomba msamaha.

Lakini kutokana na mawazo na mwendo kasi wa Msafiri ,walijikuta wakipata ajali na Msafiri kupoteza maisha papo hapo, na Zuwena kujikuta hospitali na mama yake akiwa pembeni.

4.2.2 Hadithi ya Kutoka Uchungaji Mpaka Ukuu wa Wachawi, iliyotungwa na kuandikwa na Ally Mbetu

Hii ni hadithi fupi inayogusa maisha ya wanadamu au ya jamii kwa jumla, ni vitu ambavyo vinatokea katika jamii tunazoishi. Hadithi hii inaitwa **"Kutoka Uchungaji Mpaka Mkuu wa Wachawi"**. Ni hadithi yenye kusisimua na yenye mafundisho ndani yake, na inahusu imani katika dini ya Kikristo. Inaonyesha jinsi baadhi ya viongozi wa dini wasivyokuwa na imani au wana imani haba na vitu wavifanyavyo, na kukosa imani na Mungu na kuamua kujiingiza katika imani za kishirikina ili kupata sifa zaidi ya kile wanachokifanya.

Hadithi hii inamuhusu Mchungaji anayeitwa Joshua, aliyepewa karama kubwa na Mungu ya kuhubiri na kuombea wenye matatizo mbalimbali katika maisha, au katika jamii inayomzunguka na jamii nyingine. Mchungaji Joshua aliifanya kazi yake kwa moyo, akiamini ni kipawa alichopewa na Mungu. Alianza katika mazingira magumu ya kutokuwa na kanisa na waumini wachache. Lakini kutokana na kipawa chake cha kuombea watu wakapona magonjwa na mapepo kutoka, jina lake lilikuwa kwa kasi na kusababisha kila kukicha waumini wazidi kuongezeka kwenye Kanisa Lake. Ongezeko hilo lilisababisha ongezeko la pesa na zawadi nyingi kutoka kwa waumini wake. Kitendo hicho kilisababisha kununua kiwanja na kujenga kanisa kubwa sana litakalopokea waumini wengi zaidi, ila katika huduma yake ya kiroho hakukosa majaribu ila kwa uwezo wa Mungu aliyashinda.

Mchungaji Joshua aliwaombea wagonjwa, na wakapona, wenye shida wakafanikiwa. Hivyo akafahamika kila kona ya nchi, maana alifanya huduma ndani na nje ya nchi. Siku moja, mwanawe aliumwa akiwa safarini na aliporudi alimfanyia maombi ili apone kwa masaa kadhaa lakini haikusaidia. Aliamua kumpeleka hospitali, lakini kwa bahati mbaya alifariki dunia. Kitendo kile kilihuzunisha sana familia. Baada ya miezi michache mwanawe wa kiume tena aliugua ghafla. Yeye na wachungaji wenziwe wakamfanyia maombi, lakini ilishindikana. Walipompeleka hospitali, alifariki dunia. Alipoteza imani kwa Mungu na kujiuliza kwanini kwake kunabomoka kila siku na kwingine kukizidi kuimarika, wakati ni yeye ndiye anayefanya kuimarike. Hivyo akaona Mungu amemuacha na ameamua kumpa mapigo makali sana. Baadhi ya watu walisema kuwa anatoa watoto kafara ili aweze kuonekana Mchungaji mwenye kipaji cha kuombea, kuponya na kutatua matatizo ya watu. Baada ya siku chache, mkewe aliugua na kupoteza fahamu. Alimuombea, lakini haikusaidia. Alimpeleka hospitali, lakini hali ikawa mbaya zaidi.

Siku moja akiwa ofisini kwake, alitembelewa na wazee wawili wakidai wamekuja kumponya mke wake kwa dawa za kienyeji. Alikataa, lakini baadaye ushawishi wa waezee ulimshinda nguvu Mchungaji Joshua na kujikuta akikubaliana nao. Wazee wale walikuwa wachawi na walitumwa na mkuu wao kuja kumshawishi ili aingie katika nguvu hizo maana anamaliza watu wao kwa kuokoka, na wao ndio waliohusika na vifo vya wanawe na ugonjwa wa mkewe. Walimwagiza vitu vya kichawi vya kumponya mke wake na hatimaye alipona, na yeye wakafanikiwa kumuingiza kwenye kundi lao la uchawi na kumpa cheo kikubwa kuwa mkuu wao wa wachawi. Pia walimpa masharti ya kutoa vitu vyote vinavyohusiana na dini nyumbani kwake na kumuamuru yeye na familia yake waache kusali. Walimpatia vitu vya kichawi vitakavyomuwezesha kutenda miujiza zaidi atakapokuwa kanisani,

hadi kufufua watu. Pia walihitaji sadaka ya damu. Hivyo, Mchungaji alikuwa anaua watu na kupata damu na vichwa vyao kuviweka mbele ya madhabahu (mahali ambapo Mchungaji anasimama kuhubiri). Jina la Mchungaji likazidi kukua, na miujiza yake kuzidi kutokana na uchawi. Na aliye mkashifu tu kwa njia yoyote ile alipoteza uhai wake.

Maisha yaliendelea na mke wake akashiriki katika ushirikina huo na vifo vya watoto wake vikaisha. Siku moja alitakiwa kumtoa mtoto wake sadaka kwa kiongozi wao wa kichawi ambaye haonekani. Mchungaji Joshua alipata wakati mgumu sana kumtoa mtoto sadaka, na cha kusikitisha mtoto alimlalamikia baba yake kwa kumtoa sadaka. Alitakiwa amchinje kwa mkono wake, ila alishindwa na mwisho, mtoto alifariki. Hapo Mchungaji na familia yake walilia sana na kuona kumbe hata huko kwa shetani hakuna msaada. Ndipo mke wake alipomshawishi wapige magoti chini na kumrudia Mungu. Walitubu kwa Mungu na kwa waumini wote na kuanza maisha mapya ya kiroho tena, ijapokuwa mwishowe alipelekwa polisi kujibu tuhuma za mauaji. Kutokana na kutubu kwake na kesi kukosa ushahidi, aliachiwa huru na kuhama sehemu ile na kwenda sehemu nyingine kufanya huduma ya kiroho.

4.2.3 Kubainisha Dhamira Zinazopatikana katika Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku.

4.2.3.1Kubainisha Dhamira Zinazopatikana katika Nyimbo za Bongo Fleva

4.2.3.1 a) Wimbo wa Lady Jay Dee, Nasimama

Nasimama ni wimbo ambao unahusu maisha ya watu kwa ujumla na jinsi watu waishivyo katika jamii inayowazunguka, wimbo huu unaonyesha jinsi mtu anavyoweza kujifanya mwema sana kwako kumbe ni mbaya. Pia unaonyesha imani

ya mtu au tegemeo la mtu kwa Mungu, ni wimbo mzuri wenye kufunza na kumuongoza mtu. Wimbo huu unadhamira zifuatazo;

i) Imani

Mwandishi anaamini kuwa kila kitu kinapangwa na Mungu. Hivyo, hata mambo yote yamtokeayo mtu anaamini kuwa ni mipango ya Mungu pekee. Anazidi kusisitiza na kusema kuwa anasimama na Mola kwa kila kitu akifanyacho na si mwanadamu, maana aliumizwa sana ila ameshasahau yote yaliyopita.

> *"Aliyepanga ni manani shida na riziki zangu, aliyezitupa gizani shida na tabu zangu. Nasimama na Mola kwa kila jambo lile nitendalo, maneno ya watu bakora yalinichapa nikaumia".*

ii) Unafiki

Msanii anaonyesha kuwa katika maisha ya kila siku tunakutana na watu mbalimbali, ila watu hao sio wote ni wazuri. Wengine machoni wanakuchekea kumbe moyoni wanakung'ong'a au wanachuki na wewe, hivyo yatupasa kuwa makini na watu hao maana si wote ni wema.

> *"Ukitazama kwa macho yako huwezi kumjua mwema aaa, mateso yako furaha yao tena mengi watasema. Moyo wa mtu kichakaa mengi yalofichika, naye mdhania mwema kumbe mchawi kwako.*

iii) Elimu

Kwa jumla, wimbo huu unatoa elimu katika jamii, kwamba yatupasa kumtegemea Mungu kwa kila jambo na si mwanadamu, kwani Mungu ni Muweza wa yote. Pia unafundisha kuhusu maisha kwa jumla, kuwa makini zaidi na watu tunaoishi nao katika jamii, maana wote si wema. Mwingine unamwambia shida yako ukijua ni rafiki au ndugu wa kweli, lakini kumbe moyoni anakucheka au anakwenda kuhadithia kwingine na watu, wanabaki kukunyooshea vidole tu. Vile vile

mwandishi anatuonyesha kuwa tusishindwe kufanya jambo sababu ya mtu au watu, maana mtu ukishamjua hawezi kukupa taabu.

> *"Nlishaambiwa zamani kinyago ukichongacho hakikutishi ng'oo, ndo maana nasimama nalia kwako"*

b) Wimbo wa Linex, Mama Halima

Mama Halima ni wimbo unaohusu mapenzi ya udanganyifu. Mwandishi anatuambia kuwa alikuwa na mpenzi wake ambaye wanapendana, lakini kutokana na ugumu wa maisha wakakakubaliana kuwa yeye akatafute maisha au pesa sehemu nyingine, ili akipata arudi ili aje waoane. Na wakati anaondoka hakuwahi kutembea naye ila walipanga hadi wafunge ndoa ndipo wakutane kimwili. Lakini, cha ajabu na kusikitisha, siku aliporudi kutoka kutafuta riziki, alimkuta huyo mpenzi wake na mimba ya miezi sita. Wimbo huu una dhamira mbalimbali:

i) Usaliti

Wimbo huu unaonyesha dhamira ya usaliti ndani yake. Mama Halima amemsaliti mpenzi wake kwa kumpa ahadi ya uongo na kushindwa kuitimiza. Walikubaliana na mpenzi wake kutokana na ugumu wa maisha, mpenzi wake aende akatafute maisha ili akipata arudi waje wafunge ndoa. Lakini baada ya mpenzi kuondoka, Mama Halima alimsaliti mpenzi wake kwa kuwa na mpenzi mwingine mpaka akapata ujauzito.

> "*Mama Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima wee umesahau ahadi ni deni. Umevunja ahadi yetu tulopanga mimi na wewe, kwamba mimi nikatafute hata nikikosa nije nikuoe. Mama Halima wee, umesahau ahadi ni deni"*

ii) Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati yanaonekana kwa mwanaume wa kwanza aliyekuwa na Mama Halima. Alimpenda Mama Halima kwa moyo wake wote na kwa nguvu zake zote. Ndiyo maana hakumgusa. Walikubaliana hadi wafunge ndoa ndipo wakutane kimwili; na alijitoa kwenda kutafuta maisha kwa ajili ya wote wawili. Pia, hata aliporudi na kumkukuta Mama Halima ana mimba ya miezi sita, hakutaka kugombana naye, bali alimpa nafasi ya kujitetea na alimuuliza maswali tu. Hayo ni mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo mwanaume huyo.

> *"Nilivyokuacha na nilivyokukuta ni tofauti tofauti kabisa, sitaki kugombana na wewe niambie nini kilikukuta, inaonyesha na iko wazi una mimba ya miezi sita. Kama unavyojua cjawai kutembea na wewe, kama unavyoelewa lakini paka nikuoe. Mi kwako ulinidanganya utanipenda kwa moyo wote, maisha hayataki haraka Mungu amekuponza wee"*

iii) Migogoro

Wimbo huu unaonyesha kuwa kulikuwa na migogoro ya nafsi kwa mpenzi wa kwanza wa Mama Halima baada ya kumkuta mpenzi wake amemsaliti na ana mimba ya miezi sita. Pili, kulikuwa na mgogoro wa nafsi kwa Mama Halima baada ya kukutwa ni mjamzito na mpenzi wake wa kwanza ambaye walipeana ahadi na baada ya kuachwa na mpenzi wa pili aliyempa ujauzito. Mgogoro mwingine unaonekana kati ya wazazi wa Mama Halima na Mama Halima, baada ya kutaka kumfahamu baba wa mtoto.

> *"Nyumbani kwenu wanataka kujua baba wa mtoto, Yule bwana uliyempenda kageuka moto"*

4.2.3.1b) Wimbo wa Diamond, Safari

Wimbo huu unahusu maisha ya ndoa kwa jumla. Mwandishi anaonyesha jinsi familia hii inavyoishi kwa upendo na amani ndani ya nyumba. Wakiongea na kushirikiana mambo mengi ndani ya familia; baba na mama wanapendana na wanaelewana, na wako tayari kusaidiana na kusikilizana wakati wote. Ila wanakabiliwa na changamoto moja tu ya hali ngumu ya maisha. Hivyo, wanaamua kukaa chini na kufikia muwafaka kuwa baba aende mjini akatafute riziki ili akipata waje watumie wote. Wimbo huu una dhamira zifuatazo;

Mapenzi ya dhati

Mapenzi ya dhati ni dhamira mojawapo inayoonekana katika wimbo huu, ambapo wanandoa hawa wanashirikiana mambo mengi, kama vile kulea watoto pamoja, kulima pamoja, kuchota maji pamoja na katika mambo mengine ya kujenga familia.

> "*We unajua kwamba na sina roho nitakuwa na wasiwasi iii ubaki na moyo utajaa wasiwasi iii napokuwa nakwenda shambani hafu nipo peke yangu honey, napokuja kuona majirani nitaumia pale napotoka kisimani ama nipo na kuni kichwani sina wa kunitua nyumbani nitaliaa.*
>
> *Maneno yako yanafanya nakosa raha na mawazo, hata mwenzio sijawahi kufika dar huu ndo mwanzo ooo, pili nakwenda nasijui pakukaa wala mavazi ohhh; we niombee niepushwe na balaa na maradhi ooo eee.*

i) Nafasi ya Mwanamke katika jamii

Hii pia ni dhamira nyingine inayojitokeza katika wimbo huu. Katika jamii yetu ya Kitanzania tumezoea kuona kina mama wakijihusisha na mambo mengi katika familia. Katika wimbo huu mwanamke anaonekana kama mtu mwenye wajibu wa kumwandalia mwanaume mizigo yake wakati anasafiri:

> "*Ahhh vipi mizigo umeshaweka tayari, nisije chelewa nikajaachwa na gari, basi jikaze usilie mpenzi, mi nitarudi niombee kwa Mwenyezi*".

Pia mwanamke ameonekana kama mlezi wa watoto; tunaona pale baba anapoenda kutafuta maisha anamuachia mama jukumu la kutunza familia.

> *“Kama watoto wakinililia waambie kesho nitarejea, wadanganye kwa vibagia waambie pipi nitawaletea. Kama watoto wakinililia waambie kesho nitarejea, usichoke kuvumilia na kila siku kuniombea, nirudi salama.*

ii) Umasikini

Umasikini ni dhamira nyingine inayojitokeza katika wimbo huu, tunaona wanajishughulisha na kilimo lakini mavuno hakuna. Wanashindia ugali na dagaa. Hivyo, wanakaa chini na kuamua baba akatafute maisha mjini, na mama aendelee kulea watoto.

> “*Basi jikaze usilie mpenzi, mi nitarudi niombee kwa Mwenyezi, zile taabu na njaa msimu mzima mavuno hakuna huwa nakosa raha pale mkikosa cha kutafuna roho yangu inauma sema ntafanya nini na pesa sina na kuonea na huruma bora niende mjini kusaka Tumaa”*

Swala lingine la umasikini linajitokeza pale mwanaume anapoondoka kuelekea Dar es Salaam, ambako anakwenda huku hajui pa kukaa, wala mavazi.

> “*Maneno yako yanafanya nakosa raha na mawazo, hata mwenzio sijawahi kufika dar huu ndo mwanzo ooo, pili nakwenda nasijui pakukaa wala mavazi, ohhh; we niombee niepushwe na balaa na maradhi ooo eee”*

4.2.3.1c) Wimbo wa Nikki wa Pili na Ben Pol, Sitaki Kazi

Wimbo huu unahusu kazi. Mwandishi wa wimbo huu anaona kama kazi ya kuajiriwa ni ya kitumwa. Haoni sababu yoyote ya kusubiri kuajiriwa maana ana kipaji. Hivyo, anapenda kujiajiri mwenyewe ili aje aajiri na wengine wanaotafuta kazi. Yeye haoni umuhimu wa kutafuta kazi ijapokuwa ana Shahada ya Uzamili. Pia anawashauri vijana kugundua vipaji vyao na kujiajiri wenyewe, siyo mpaka wasubiri kuajiriwa na serikali au na mashirika binafsi. Wimbo huu una dhamira nyingi katika jamii:

i) Ajira ya kujitegemea

Mwandishi ana mtazamo wake kuwa siyo lazima ukimaliza Chuo au mafunzo usubiri kuajiriwa na serikali au na mashirika binafsi. Kila siku anajiuliza kwanini vijana kila kukicha wanalalamika kuwa hakuna ajira na uwezo wa kujiajiri wanao? Anajiuliza kuwa na maisha mazuri ni hadi uajiriwe na serikali au kwenye shirika tu, Anawataka vijana kujituma ili kufanikiwa, na siyo kusubiri tu kuajiriwa.

> *"Utamaduni wangu nikuuliza why why why why why why x2*
> *Nimekataa kuwa mtumwa najituma eee eee eee*
> *Kataa kuwa mtumwa jitume eee eee eee*
>
> *Form six degree hadi masters staki kazi, elimu sio vyeti nachoma sitaki kazi, wana vyeti mtaani vijana, hawana kazi. Natengeneza ajira myaa niupe kazi"*

ii) Kujitegemea

Muandishi anatoa mwongozo kwa vijana ili waweze kujitegemea, maana kuajiriwa ni kazi ya kitumwa. Anawashauri kugundua vipaji vyao ili kuachana na mashaka au wasiwasi katika kazi; mtu afanye kazi kwa uhuru wake mwenyewe na siyo kuongozwa, kulazimishwa au kufanya kazi kwa maslahi ya wachache tu. Hivyo, anawashauri vijana kujiajiri kuepukana na bughudha.

> "*Uko na wasiwasi mtu bila nafsi umeajiriwa shirika la mtu binafsi, sina wasiwasi mtu mwenye nafsi sijaajiriwa nimeajiri yangu nafsi. Mishaara imejaa makato biashara mjini ndo zimejaa mapato, ajira itakulinda toa vyeti siitaji kulindwa mimi sio mtoto wa geti kali, kazi ni mpaka wa akili yako, mpaka ufukuzwe kazi ndo ugundue kipaji chako. Ajira ya mkeo chini ya boss we ni house girl pekee ndiyo anakuita boss, sivai tai sikatai utamaduni wangu mi nikuuliza why? Elimu bongo imekosa plani ya pili ahufundishwi kuwa tajiri"*

iii) Migogoro

Katika wimbo huu, kuna dhamira nyingine iliyojitokeza ya migogoro. Vijana wana migogoro na serikali kwa kukosa ajira. Na mwandishi ana mgogoro na Wizara ya Elimu. Anaona kuwa Wizara ya Elimu ingefundisha njia mbalimbali za kujipatia

kipato, tofauti na masomo ya darasani tu yakusubiri mtu kuajiriwa peke yake. Hivyo, wimbo huu pia ni changamoto kwa serikali yetu kwa kufikiria njia mbadala ya kuwawezesha wanachuo na wanafunzi kujiingizia kipato licha ya kusubiri ajira rasmi.

"*Elimu bongo imekosa plani ya pili ahufundishwi kuwa tajiri*"

4.2.3.1d) Wimbo wa Professor Jay na Juma Nature, Ndio Mzee

Wimbo huu unahusu siasa. Unaonyesha jinsi wanasiasa na vibaraka wao wanavyokuwa na maneno mengi na matamu wakati wa kuomba kura. Lakini mwishowe wakishapata wanachokitaka hawatimizi ahadi zao, na huwaacha wananchi wakiteseka kama kawaida, na wenyewe kuendelea kujinufaisha wao wenyewe na familia zao. Pia, unaeleza kuwa yatakiwa kuwa makini na kuwagundua wanasiasa matapeli wanaojinufaisha wao wenyewe na familia zao na kuwanyima fursa ya kuingia katika uongozi serikalini. Wimbo huu una dhamira kama vile;

i) Siasa

Dhamira ya siasa inajitokeza katika wimbo huu ambao, mwandishi anaonyesha jinsi kibaraka wa mgombea anavyomnadi mgombea kwa wananchi kwa lengo la kuvuta usikivu wao ili wamsikilize mgombea huyo na kumpa kura yake ya ndio:

> "*Naam ndugu wananchi mc wenu babu Ayubu nawaleeteeni habari japo kwa ufupi, kuhuusiana na huyu ndugu yetu Joseph Haule mpeni kura zenu za ndio. Kwasababu yeye ni mpenda watu, mpenda amani na mtu mwenye huruma kwa wananchi wote. Kwahiyo basi ninawaomba wananchi mumpe kura yake ya ndiyo, hivyo basi wananchi tafadhali namkaribisha mgombea mtu ndugu Joseph Haule ili aweze kuzungumza na wananchi"*

Baada ya kibaraka wake kumnadi, mgombea anasimama mbele ya hadhara na kumwaga sera zake nyingi zisizokuwa na ukweli wowote katika jamii. Anajinadi

kuwa yeye ameletwa aokoe hiki kizazi kwa ahadi nyingi za uongo, ili mradi tu apate kura za wananchi:

> "*Ok ok naitwa Joseph Haule nadhani nimeletwa niokoo hiki kizazi, mimi ni mwanasiasa niliyebarikiwa na Mungu nadhani nimeletwa niokoe hiki kizazi. Nimeletwa kwenu ili niwapunguzie machungu mimi ni mteule tangu enzi za sahara ndiyo maana nimetunukiwa hii zawadi, na hekima kuliko Mfalme Suleimani. Msiwe na wasi na hii itafahamika pindi mtakaponipa nafasi, actually nimedhamiria kuwasaidia Taifa lenye nguvu liwe Tanzania, jamani makofi basi tafadhali. Ni mambo madogo tu nadhani nitarekebisha mkinipa visiku vichache, uchumi utapanda ghafla bin vuu, nataka mpaka matonya afundishe Chuo Kikuu nchi ya Tanzania itang'ara kishenzi na nitahakikisha kila baamedi anamili benzi"*

ii) Umasikini

Umasikini ni dhamira nyingine inayojitokeza katika wimbo huu, ambao wananchi wanaonekana kuitikia kila jambo wanaloambiwa na mgombea. Umasikini umewatawala wananchi na kujikuta wanaitikia hata vitu ambavyo kwa hali ya kawaida unaona hapa mgombea anadanganya kabisa. Hivyo, kutokana na umasikini wa kimaisha wanajikuta wakichagua mgombea ambaye hana sifa za oungozi.

"Si mtafurai watanzania jamani "Ndyio mzee"
Si kweli inakubalika jamani "Ndiyo mzee"
Basi mie mkombozi wenu jamani "Ndyio mzee"
Na nitafuta shida zenu zote "Ndyio mzee"
Hivi ni nani ni vijimambo tu "Ndyio mzee"
Na vinanikera kwelikweli "Ndyio mzee"
Basi hali itabadilika sawa "Ndiyo mzee"
Na hatamu tutaishika ok "Ndiyo mzee""

iii) Migogoro

Kutokana na ahadi nyingi zisizo za kweli za wanasiasa, wanajikuta wakiingia katika mgogoro mkubwa na wananchi kwa kushindwa kutekeleza ahadi walizoahidi wakati wa kuomba kura. Maana wakati huo wa kuomba kura huwa na maneno mengi yanayopitiliza na yasiyoweza kutekelezeka kama wanavyodai. Hivyo husababisha

kuingia kwenye mgogoro na wananchi wanaoona mbali zaidi na ambao hawahitaji kudanganywa:

> *"Nyie ndugu zangu huyu jamaa msimpe uongozi siyo mzuri muongo tu mnafiki na kiburi, si mzuri. Anaongopea sana cjui kazaliwa muda gani alfajiri au alasiri au wakati wa mvua zile za kipindi kile. Amepitapita school lakini mambo yake si mazuri, waala tusimtetee atatuangamiza".*
> *"Wananchi mmesikia "Ndiyo Mzee"*
> *Kuwa jamaa hatufai "Ndiyo Mzee"*
> *Na inafaa kumchukia "Ndiyo Mzee"*
> *Hatumtaki aondoke zake "Ndiyo Mzee"*
> *Tusifuate maneno yake "Ndiyo Mzee"*
> *Tunahakikisha hatumchagui"Ndiyo Mzee"*
> *Kwasababu jamaa ni mnafiki"Ndiyo Mzee"*
> *Asitufanye tuwe na dhiki "Ndiyo Mzee"*

4.2.3.2 Kubainisha Dhamira Zinazopatikana katika Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku

4.2.3.2a) Dhamira Zilizojitokeza katika Hadithi Fupi ya Godoro la Mtumba na Irene Mwamfupe Ndauka.

Hadithi hii imebebwa na dhamira kubwa ya mapenzi, ndiyo iliyotawala katika kitabu hiki. Ikifuatiwa na dhamira nyingine ndogondogo kama vile wivu, migogoro, nafasi ya mwanamke katika jamii, unyanyasaji wa kijinsia, kutokujitambua na starehe.

a) Mapenzi

Katika kitabu hiki tunaona, kuwa kuna mapenzi ya dhati na mapenzi ya ulaghai.

i) Mapenzi ya dhati

Mama kwa Zuwena

Yanajitokeza kati ya Mama Zuwena na mwanae Zuwena. Mama Zuwena ana mapenzi ya dhati kwa binti yake, ndiyo maana hata anapokuwa Tanga anampigia simu Zuwena na kumuuliza anaendeleaje na masomo yake; na kumuuliza kama

mjomba wake bado yupo na Zuhura Chachandu na kumtaka Msafiri amuwekee msichana wa kazi ili akitoka shule apate muda wa kujisomea na siyo kufanya kazi za nyumbani.

"Shikamoo mama"
"Marahaba, haya vipi masomo"
"Masomo naendelea vizuri mama"
"Huyo mwanamke wa mjomba wako, sijui Zuhura……."
"Zuhura Chachandu……"
"Eeeee, bado anakuja hapo?"
"Bado mama hata leo alikuwepo akaondoka"
"Haya mwanangu, soma sasa, maisha ya siku hizi yapo hivyo, bila kusoma hakuna maisha bora."
"Nasoma mama, tena nasoma sana"

Zuwena Chachandu kwa Msafiri

Mapenzi mengine ya dhati yanaonekana katika Zuhura Chachandu kwa Msafiri. Zuhura anampenda kweli Msafiri, ndiyo maana yuko tayari kufanya lolote kwa ajili ya Msafiri. Pia hayuko tayari kuachana na Msafiri, ndiyo maana hata wanapogombana, yeye anazidi kumng'ang'ania tu, hata akimpiga bado anamfata.

"Nini kimetokea mpaka upo katika hali hiyo baby?"
"Sikia mama, ulipoingia ndani tu muda ule, sina mimi nikashuka. Ile nafunga mlango, nikashtuka nafungwa sharti kwa nyuma……."
"Na nani sweet,"nilidakia……..
"Zuhura……."
"Zuhura Chachandu?"
"Zuhura gani mwingine?"
"Kisa?"
"Kisa nini zaidi ya mapenzi!"

ii) Mapenzi ya Ulaghai

Msafiri kwa Zuwena

Mapenzi ya ulaghai yanajitokeza kati ya mjomba Msafiri na Zuwena. Tunaona jinsi Msafiri anavyomdanganya Zuwena ili tu ajihusishe naye katika mapenzi. Msafiri

anajua wazi, kuwa Zuwena ni mtoto wa dada yake, hivyo hapaswi kufanya aliyokuwa anayafanya. Lakini anaamua kutumia cheo chake, pesa zake na ukubwa wake kumlaghai Zuwena, na mwishowe anafanikiwa. Anamlaghai kwa maneno mazuri, vijizawadi na hata kumuahidi kumuoa ili waje waishi kama mume na mke hapo baadaye, wakati anajua kabisa swala la wao kuishi kama mke na mume lisingewezekana, maana wao ni ndugu.

"Anko," aliita
"Abee…."
"Unajua umekuwa sana."
"Kweli anko?" nilimuuliza kwa sauti yenye usingizi.
"Kweli kabisa, yani siku hizi unapendeza anko si kama zamani. Ukivaa nguo zako za kisasa hizi ndiyo kabisa, dah! Ankooo."
"Mjomba bwana! Sijui alikuwa anajua ninavyojisikia, alinikalisha kwenye kochi, akanilaza, akafungua pindo la khanga kidogo kisha kapeleka mkono wake kwenye nchi ya nido nikasisimka sana. Hapo macho yangu yote yalikuwa yamelegea."
"Anko."
"Abee"
"Twende chumbani kwako."

Baada ya kunogewa na mapenzi yao, hatimaye Msafiri anamfukuza Zuhura ili waendelee kupata nafasi nzuri zaidi ya kufurahia mapenzi yao yeye na Zuwena.

"Sikia, huyu mwanamke hawezi kurudi tena kwangu, nafasi yake utashika wewe."

Msafiri kwa Zuhura Chachandu

Msafiri hana mapenzi ya dhati kwa Zuhura Chachandu, ndiyo maana anaamua kumlaghai mjomba wake na kuwa naye kimapenzi. Pia anampiga, anamtukana na kumfukuza kwake. Pia hata anapokuwa naye nyumbani kwake anamtoroka usiku akiwa amelala na kumfuata Zuwena.

“Mara tukasikia milango inafunguliwa hovyohovyo tu, Zuhura Chachandu bwana, kaamka, kamkosa jamaa yake kitandani sasa anamtafuta.”
“Tulia kwanza.”
“Mlango wangu uligongwa na kuita kwa sauti……..
“We Shani, mjomba wako yuko wapi?”
“Nilinyamaza kimya kwa ujanja kwani nilijua nikimjibu haraka atajua
niko macho”
“Shani, mjomba wako yuko wapi?”
“Sijui mi nimelala”

Mwalimu Mnoko kwa Zuwena

Hakuna mapenzi ya dhati kati wa Mwalimu Mnoko na Zuwena. Mwalimu Mnoko anamtamani Zuwena tu na Zuwena anaingia kwenye mahusiano ya kimapenzi kwa kutaka kusaidiwa tu kimasomo na kujaribu mapenzi na watu tofauti ili aone ladha yake tu. Mwalimu Mnoko ana mazoea ya kuwalaghai wanafunzi wa kike na kufanya nao mapenzi, kisha kuwaacha.

“Eeee eti? Una nini Zuwena?” alinyoosha mkono wa kulia na kunishika kifuani. Alikuwa kama amenitonesha hisia zangu. Mwili mzima ulinisisimka kwa kushikwa kifua tu, nikamkumbuka mjomba…….”
“Mwalimu Mnoko mi sitaki.”

Baada ya mazungumzo, Mwalimu Mnoko anamwambia Zuwena baada ya kutoka shule aende nyumbani kwake wakamalizane, maana pale ofisini wameshindwa. Na Zuwena baada ya kuhisi kusisimka kwa mwili anatamani kufanya mapenzi na Mwalimu Mnoko; hivyo anakubali kwenda kwake.

“Nilimvisha ile zana tayari kwa vita ya kitandani. Vita ilianza mwalimu alikwenda sehemu yake na mimi sehemu yangu, risasi zikaanza kurushwa pande zote. Lakini yeye mwalimu alikuwa akizirusha kwa utaalam zaidi ndo maana nikasema moyoni kumbe ndiyo maana aliweza kulala na Ponde kwa mara saba zote.”

Pia katika jamii yetu kuna aina zote hizi za mapenzi, yaani mapenzi ya dhati na mapenzi ya udanganyifu. Mapenzi ya udanganyifu ndiyo yanaonekana kushamiri

sana kuliko mapenzi ya dhati, watu wamekuwa wakigombana, wakiachana, wakinuniana, na kupigana vita kali, na wakati mwingine hata kuuwana kwa kuwa hakuna upendo kati yao. Jambo ambalo ni hatari sana katika jamii yetu ni kuwa, kila mtu anakosa imani na mtu mwingine kwakuwa hakuna upendo wa dhati kati ya watu, na watu na jamii na jamii.

a) Nafasi ya mwanamke katika jamii

Hii ni dhamira nyingine inayojitokeza katika kitabu hiki. Mwanamke anaonekana kama mlezi, kama mpishi na kama mama anayetunza familia. Katika kitabu hiki, tunaona kuwa mama yake Zuwena ameonekana kama mlezi, amemlea Zuwena toka amezaliwa na mpaka amemaliza darasa la Saba, na hata anapokwenda kwa mjomba wake anaendelea kumlea kwa kwa njia ya simu na hata kwa kumtembelea.

> *"Za masomo mwanangu?"*
> *"Nzuri mama, magumu kidogo lakini tunapambana."*
> *"Mungu atakusaidia"*
> *"Amina mama."*

Nafasi nyingine imejitokeza kwa Zuwena, ambapo anaonekana akifanya kazi za ndani zinazopaswa kufanywa na mwanamke kama vile kufua, kupiga deki na kupika.

> *"Shikamoo mama."*
> *"Marahaba. Haya siku hizi mjomba wako ndiye anayekupokelea simu siyo.....?"*
> *"Mimi napika mama, yeye amekaa sebuleni na simu yangu iko sebuleni."*

Hata katika jamii yetu, kina mama wanachukua jukumu kubwa na zito katika kuwalea watoto wao wakue katika misingi iliyo bora ya kidini ili kuwaepusha na watu laghai. Huwafunza kuishi na watu vema, pia huwahimiza kusoma kwa bidii ili

hapo baadaye wasitetereke katika maisha yao. Pia huwafunza kujifunza kazi za nyumbani na shambani na kuishi na watu vema katika jamii inayowazunguka.

b) Unyanyasaji wa Kijinsia

Hii ni moja ya dhamira katika kitabu hiki. Unyanyasaji wa kijinsia unajitokeza pale ambapo mjomba Msafiri anachukua nafasi yake kama mjomba, mlezi, mtu mwenye pesa kumshawishi binti mdogo ambaye pia ni mjomba wake na ni mwanafunzi kuwa mpenzi wake. Mjomba Msafiri anatumia nafasi yake kumlaghai Zuwena ili awe mpenzi wake na hatimaye anafanikiwa kwa kuwa Zuwena anaishi katika nyumba yake na anamtegemea kwa kila kitu.

> *"Kichwani kengele iligonga, nilianza kuhisi maneno ya anko ni zaidi ya sifa. Mbaya zaidi wakati ananisifia alikuwa bado amenishika mkono na kuniangalia kwa kunikaguakagua. Ilifika mahali mjomba alishindwa kujizuia, akanikumbatia bwana, akaniweka kifuani kwake. Nilijikuta na mimi namkumbatia kwa kuzungusha mikono yangu kiunoni mwake. Nilihisi kuishiwa nguvu, joto lake zuri likanifanya nipungukiwe akili ya kuwaza mabaya na mazuri."*
> *"Anko, mjomba aliniita kwa sauti ya mchoko"*
> *"Abee"*
> *"Twende chumbani kwako."*
> *"Nilishtuka sana kupata maumivu makali, nikapiga kelele huku nikimsukuma kwa nguvu zangu zote, mjomba akashtuka sana akatoka kitandanina kusimama. Nilikaa kitandani huku nikihema sana na kilio juu."*

Unyanyasaji mwingine wa kijinsia unaonekana kwa Mwalimu Mnoko. Mwalimu Mmoko amezoea kunyanyasa watoto wa kike kwa kuwalaghai kuwa atawasaidia kimasomo au kutokuwapa adhabu pale wafanyapo makosa ili wawe nao kimapenzi. Tunaona anamlaghai Pode kuwa mpenzi wake na baada ya kumchoka anamwacha; lakini Pode hayuko tayari tena kukosa penzi la Mwalimu Mnoko. Pia tunaona wakati mwalimu Mnoko anapokuwa

chumbani na Zuwena, Pode anafuatilia ndipo Zuwena anataka kujua ukweli juu ya Mwalimu Mnoko na Pode.

"Niambie ukweli kwanza, Pode ni nani wako?"
"Nikikwambia ukweli ndio utanikubalia mambo?"
"Eee"
"Nimewahi kutembea naye siku za nyuma lakini tuliachana."
"Kwanini mliachana?"
"Hajatulia"
"Kivipi?"
"Ameshatembea na mwalimu Siasa Mageuzi"
"Mhhhh wewe umetembea nae mara ngapi?"
"Mhhhhhh…….kama mara saba tu"

Pia unyanyasaji mwingine unajitokeza pale Mwalimu Mnoko anapotumia nafasi yake kama Mwalimu kumtaka Zuwena kimapenzi ili asimpe adhabu. Mwalimu Mnoko baada ya kuona maendeleo ya Zuwena darasani yanashuka ndipo anapoamua kumteka kwa lengo la kujidai atamsaidia kimasomo. Anamwita Zuwena ofisini na kutaka kufanya naye mapenzi huko.

"Mwalimu Mnoko mi sitaki"

"Hutaki nini?"

"Sitaki hivyo unavyonishika we sema ulichoniitia"

"Unanifanyia ukali Zuwena, huogopi kama mi ni mwalimu wako!Eee?"

"Hata kama ni mwalimu ndo unishike kifuani, si useme tu"

Unyanyasaji wa kijinsia unajitokeza sana pia katika jamii zetu. Watu wamekuwa wakatili kuliko wanyama. Ndiyo, maana kila kukicha tunasikia matukio ya kutisha na ya kuogopesha. Watu wanaua albino bila huruma, wanabaka watoto bila huruma, wanawanyanyasa watoto kwa kuwapiga sana, kuwachoma moto, kuwalaza bila chakula na kuwalaghai kwa kutumia pesa zao na kuwaaribia maisha wakiwa bado wadogo, pamoja na wanafunzi pia. Kitendo kinachosababisha, kuwakatisha masomo yao na kuwaacha wakiteseka siku zote za maisha yao na kubaki na kovu la majuto na mateso.

c) Kutojitambua

Dhamira hii inajitokeza pale tunapoona Zuwena anadanganywa na mjomba wake awe mpenzi wake. Anakubali kujihusisha na mapenzi kwa kuwa anajiona amekuwa na anaonekana mrembo. Pia baada ya kuingia kwenye mapenzi anaahidiwa na mjomba Msafiri kuwa watafunga ndoa na kuishi kama mume na mke, wakati anajua wazi wao ni ndugu, Zuwena anashindwa pia kujitambua kwa kutoenda shule na kuzingatia masomo na kushawishika kwenda hotelini wakale raha maana nyumbani mama anawabana sana. Wanashindwa kujiachia na kukosa uhuru wa mapenzi yao. Amesahau kuwa elimu ndiyo mkombozi wa maisha yake na siyo mapenzi.

> *"Basi usiende kazini leo"*
> *"Ili?"*
> *"Tushinde wote"*
> *"Tushinde wote kivipi?"*
> *"Si kuwa pamoja jamani sweet"*
> *"Wapi, hapa nyumbani?"*
> *"Tutoke, wewe toka utafute hoteli mimi nitatoka kama nakwenda shuleni halafu nakufuata ulipo"*
> *"Oke, basi ngoja niende lakini usichelewe kuja"*

Tatizo lingine la kutokujitambua linaonekana pale Zuwena anapokosa adabu na busara kwa kunogewa na mapenzi ya mjomba wake, mpaka kufikia hatua ya kuhamia chumbani kwa mjomba wake. Na hata mama yake alivyokuja kuwasalimia, Zuwena alishindwa kujizuia na kumtoroka mama yake usiku akiwa amelala na kwenda chumbani kwa mjomba wake.

> *"We mama, nilirudia huku nikiendelea kujishika sehemu mbalimbali, hasa kwenye kifua"*
>
> *"Nilipoona hajaitika, nikamshika kwa mbali, pia hakushtuka, nikainuka na kukaa kwa sekunde kadhaa. Halafu nilinyoosha miguu kuelekea upande wa miguuni mwa kitanda na kushusha miguu. Nilisimama na kutembea hadi mlangoni, huku*

nikigeuka kumwangalia mama kwa machale. Nikafanikiwa kufungua mlango na kutoka”
“Haa! Huogopi baby?”
“Shiii, usiseme kwa sauti mama atasikia”

Pia tatizo hili linaonekana kwa Msafiri. Msafiri anashindwa kujitambua kwa kumlaghai mtoto wa dada yake kwa mapenzi ya uongo, na kumshawishi atoroke hata usiku ili wawe wote. Pia anamdanganya dada yake mambo mengi ili asijue wao na Zuwena ni wapenzi. Hakujua anajidanganya na kuvunja uaminifu wake kwa dada yake na ndugu zake kwa jumla. Hawakujua ipo siku mambo yote yatakuwa hadharani.

“Sasa sikia, itabidi wewe nikupeleke polisi halafu mimi nitakuwa nimesafiri Morogoro. Nitampigia simu mama yako na kumwambia nimepigiwa simu kutoka polisi kwamba wewe uliwekwa ndani jana wakati unatoka shuleni.”

Katika jamii yetu kuna watu wengi sana ambao hushindwa kujitambua, hasa vijana. Hufanya mambo bila kufikiri nini madhara yake hapo baadaye, au nini kitatokea hapo baadaye. Ndiyo maana wanafunzi wengi hushindwa kuendelea na masomo kwa kupata ujauzito au kwa kujiingiza katika madawa ya kulevya, au kujiingiza katika makundi yasiyofaa na kupoteza mwelekeo wa maisha yao. Pia, wapo watu wazima ambao hawajitambui kwa kufanya mambo ya aibu katika jamii, kama ata kubaka, kufanya mapenzi na binti wa kumzaa au na watoto wao wa kuwazaa, kurubuni wanafunzi, kuua albino. Hii yote ni kutojitambua na kumkosea Mungu.

d) Migogoro

Katika kitabu hiki kuna migogoro ya kinafsi na migogoro kati ya mtu na mtu.

i) Migogoro ya kinafsi

Mama Zuwena

Tunaona mama yake Zuwena anavyohangaika kutaka kupata ukweli juu ya mwanae Zuwena na mdogo wake Msafiri baada ya kuhisi kuwa kuna kitu kinaendelea kati yao. Halali wala kushinda kwa raha akitaka kujua ukweli wa jambo, ndiyo maana anaamka usiku kutaka kujua mwanae Zuwena ameenda wapi. Ijapokuwa anadanganywa mara nyingi, hakati tamaa mpaka ukweli unapopatikana.

> *"Moyo ulifanya paa! Mama alisimama mbele yetu……"*
> *"My God, alisema mjomba"*
> *"Mamaa, niliita kwa kilio, nikatoka kwa mjomba na kukaa pembeni nikiwa tayari nimeshaanza kulia."*
> *"Hili ndilo nilikuwa nalitegemea na nilijua lipo, ila nilikuwa napata tabu ya namna ya kupata ushahidi kama huu sasa hivi, alisema mama akiwa amekasirika balaa"*

Msafiri na Zuwena

Mgogoro mwingine unaonekana kati ya Zuwena na Msafiri, baada ya kufumaniwa kila mtu anawaza chake. Zuwena anapata mawazo na kukumbuka siku ya kwanza wakati Msafiri anaanza kumtongoza kwa kumsifia mambo mengi na kujiona mwenye hatia sana.

> *"Niliona nyumba haitoshi, kila upande nilioangalia ulikuwa mzito kwangu. Nilihisi mimi ni binadamu mmbaya kuliko mwingine yeyote aliyewai kuishi katika dunia hii"*

iii) Migogoro kati ya Mtu na Mtu

Zuwena na Pode

Zuwena na Pode wanaingia katika mgogoro baada ya Pode kumuona Zuwena yupo nyumbani kwa Mwalimu Mnoko. Ndipo anapoanza kufuatilia na kutaka kujua nini kinaendelea kati ya Zuwena na Mwalimu Mnoko.

“Nikiwa naendelea kuwaza, mara akapita Pode……”
“Hee! Zuwena wewe, huku kwa Mwalimu Mnoko umefuata nini?”

Zuwena na Mwalimu Mnoko

Zuwena na Mwalimu Mnoko wanaingia katika mgogoro baada ya Mwalimu Mnoko kumwita ofisini na kutaka kufanya naye mapenzi. Pia baada ya kukubaliana wakutane nyumbani kwa Mwalimu wanaingia katika mgogoro mwingine baada ya kuona Pode anawafuatilia, kutaka kujua ukweli wa kipi kinaendelea kati ya Mwalimu Mnoko na Pode.

“Una uhusiano gani na Pode? Nilimuuliza swali zito”
“Nani, Pode?”
“Utamuweza Yule”
“Hujanijibu swali lakini”
“Zuwena, yaache bwana, tuangalie yetu, alisema mwalimu huku akinivutia chumbani kwake”
“Pleese Mwalimu naomba niache” Nilimwambia kwa lugha iliyojaa ujasiri. Nilimwonyesha kwamba akileta za kuleta naweza kupiga kelele.”

Mwalimu Mnoko na Pode

Mgogoro kati ya Mwalimu Mnoko na Pode unakuja baada ya Mwalimu mnoko kukata mahusiano na Pode wakati Pode bado anamuhitaji. Pia baada ya kugundua kuwa kuna uhusiano unaendelea kati ya rafiki yake Zuwena na Mwalimu Mnoko, ndipo anapoamua kufuatilia kwa kwenda kwa Mwalimu Mnoko kila wakati ili apate ukweli.

“Haya unataka nini?”
“Nina hamu na penzi lako”
“We si tumeachana?”
“Wewe ndiyo uliniacha”
“Sasa si nilikuacha kutokana na tabia yako ya uhuni”
“Kwani wewe si muhuni?”
“Uhuni wangu nini?”
“Unataka kunambia Zuwena hayumo chumbani kwako?”

Msafiri na Zuhura Chachandu

Msafiri na Zuhura Chachandu wanaingia katika mgogoro baada ya Msafiri kuanza mahusiano ya kimapenzi na mjomba wake Zuwena, hivyo anatumia muda mwingi na Zuwena na kumsahau Zuhura. Ndiyo maana unapotokea ugomvi kidogo tu anaamua kumuacha kabisa Zuhura na kumwambia Zuwena awe huru kuanzia wakati ule, yeye ndiyo atashika nafasi ya Zuhura Chachandu, akimaanisha ashaachana na Zuhura kabisa. Zuhura hayuko tayari kuachika, hivyo anahakikisha anafanya fujo kila anapokutana na Msafiri na kufuata nyendo zake hadi anapogundua anatembea na mjomba wake Zuwena.

> *"He! Yule mwanamke analaana nini? Sasa madai yake yalikuwa nini?"*
> *"Sikiliza kwanza. Aliponishika shati, nikageuka na nilipogundua ni yeye nikamchapa makofina yeye akataka kunirudishia, wee! Nimempiga mabuti hadi amechakaa. Hili shati huku kufunguka vifungo na huu mkanda kuwa hivi ni kwa sababu alikuwa akining'ang'ania huku akiomba msaada, ndiyo mlinzi akaja……*

Msafiri, Zuwena na Mama Zuwena

Mgogoro kati ya Msafiri, Zuwena na mama Zuwena unaingia baada ya mama Zuwena kuwafumania mdogo wake Msafiri na binti yake Zuwena. Anasikitishwa sana na kitendo kile na hakufurahi hata kidogo na anaamua kutoa maneno mabaya juu yao.

> *"Mama aliniangalia kwa jicho baya sana, akamgeukia mjomba….."*
> *"Msafiri"*
> *"Naam dada"*
> *"Mimi si dada yako tena na hata Zuwena si mpwa wako tena, mimi ni mama mkwe wako na Zuwena ni mkeo kuanzia leo"*
> *"Dada usiseme hivyo"*
> *"Lazima niseme, nisiposema nitakuwa mama wa ajabu sana, mtoto anachezewa naangalia hivihivi……"*

Katika jamii migogoro mingi sana ya kimapenzi hutokea, kwa wapenzi kusalitiana, kudanganyana, kuachana. Pia kuna migogoro mingi ya kutokuelewana kutokana na sababu mbali mbali, kama vile kudharauliana, kukashifiana, kutapeliana, na mtu kutokuwa na imani na mtu mwingine. Dhamira zote hizi zipo katika jamii yetu na huleta madhara sana katika jamii.

4.2.3.2b) Dhamira Zinazojitokeza katika Kitabu cha Kutoka Uchungaji Mpaka Mkuu wa Wachawi na Ally Mbetu

Katika kitabu hiki tunapata dhamira nyingi, ila dhamira kubwa inayojitokeza katika kitabu hiki ni uchawi. Zikifuatiwa na dhamira nyingine ndogo ndogo kama vile usaliti, ushawishi, imani, migogoro, mapenzi ya dhati, nafasi ya mwanamke katika jamii, umasikini na matabaka.

a) Uchawi

Uchawi ni dhamira kubwa sana inayojitokeza katika kitabu hiki, na karibu vipengele vyote vimebebwa na dhana ya uchawi. Dhana ya uchawi inajitokeza pale ambapo Mchungaji Joshua anatokwa na imani kwa Mungu kutokana na maombi kutokumponya mke wake na anaamua kuingia kwenye imani za kishirikina ili mke wake apone.

> *"Niliona ngoja nifanye vile ili nione uongo wa wazee wale kama wataweza kumponesha mke wangu, baada ya kukubaliana nao walinipa masharti ya kutafuta mbuzi mweusi, sanda pamoja na maji aliooshewa maiti vipatikane kabla ya usiku. Kwa vile walikuwa wamekuja kwa ajili yangu nilimtuma mtu akawatafutie nyumba ya wageni wapumzike kabla ya kuanza kazi ile usiku"*

Baada ya kumuagua mke wa Mchungaji usiku ule, wale waganga wanasema:

> *"Ooh, sawa tatizo ni lile lile, mgonjwa amezikwa kivuli chake hivyo tutamuosha kwa maji ya maiti kisha tutamuacha hapa sisi na wewe tutakwenda makaburini kumfukua na kumzika mbuzi mweusi"*

Baada ya kutoka makaburini wanazindika nyumba na kuwachanja familia nzima eti wanawawekea kinga na wanamchagua kuwa mkuu wao wa wachawi na kumtaka aende kuzimu akasimikwe ukuu huu na mkuu wa kuzimu.

> *"Sauti ya mkuu wa kuzimu kama alivyojiita mwenyewe ambaye hakuonekana zaidi ya sauti yake." Baba Mchungaji kundi langu lilifanya mambo mengi katika uponyaji wako, hii tumeifanya sehemu nyingi kwa kuua nguvu za kanisa. Kwa kweli asilimia nyingi wachungaji si wavumilivu kwani hawawezi misukosuko ya kidunia. Na tukiifanya basi lazima wasalimu amri".*
>
> *"Kundi letu linaviongozi wengi wa dini mbalimbali ambao walijifanya wanamjua Mungu na mwisho wake huwatega kwa mitego mizito kama yako ambayo huibomoa imani yao na kufanikiwa kuwavuta kwetu. Kampeni yetu baada ya miaka mitano tutahakikisha kila kiongozi wa dini mwenye nguvu ya karama anakuwa mfuasi wetu."*

Mchungaji Joshua anakubali kuwa mkuu wa wachawi na kuifanya kazi yake vizuri kama anavyoagizwa na mkuu wa kuzimu na kufanya upendo uongezeke kutoka kwa mkuu wa wachawi na wachawi wenzie. Hayo yanajidhihirisha mkuu wa kuzimu anapomwambia;

> *"Joshua umekuwa mwanafunzi mwema mwenye kufuata mafunzo kwa ufasaha na hakika, sasa hivi umeweza kuyavunja makanisa yote kuanzia kitendo kizito ulichokitenda hata waliokuwa wamepoteza imani kwako wote watarudi. Umeweza kuwateka kwa kulitanguliza neno la Mungu mbele bila kujua kile kilikuwa kivuli cha kujificha wasikujue wewe ni nani. Hakikia umemsambaratisha nabii muongo na leo nitampumzisha milele kuzimu na kumpa adhabu kali siku zote za maisha yake ya kuzimu……Joshua endelea……Endelea Endelea……"*

Haya ni mambo yanayojitokeza katika jamii nyingi zinazotuzunguka. Viongozi wa dini na makanisa na misikiti wamekuwa wakiongezeka kila kukicha na baadhi yao

wakiwa ni manabii wa uongo. Wanahubiri kwa kutumia nguvu za giza na kutenda miujiza kwa kutumia nguvu za giza ama kwa kununua watu ili watoe ushuhuda wa uongo kanisani na kuwapatia fedha ili kuvuta waumini wengi zaidi katika makanisa yao.

Dhamira ndogo ndogo

a) Usaliti

Katika kitabu hiki tunaona ni jinsi gani Mchungaji Joshua amemsaliti Mungu kwa kushindwa kumtumikia yeye na kuamua kutumikia uchawi na mizimu:

> *"Katika maisha yangu baada ya kumpokea Kristo sikuwaza kuwa, kuna siku moja nitakunywa damu za watu au hata kula nyama zao, tendo ambalo ni chukizo mbele ya Mungu. Lakini kufa katika imani yangu ya kiroho ndiko kulikosababisha kufanya yoye haya, niliweza kuyakemea mapepo yakakimbia, niliweza kuwaponya wagonjwa kwa jina la Yesu nao wakapata afya, niliweza kuwatua mizigo mizito ya matatizo waumini wa kanisa langu. Nilipanda cheo toka uchungaji mpaka uaskofu kutokana na karama niliyopewa na Mungu, kutatua matatizo na kanisa langu kuwa kimbilio la wenye uhitaji"*

Mchungaji Joshua anawasaliti pia wachungaji wenzake wanakuja kumtembelea na kumfanyia maombi wakati anaumwa na kukataa kuonana nao kwa madai ameshapona na baada ya kuonana nao anakataa kufanya maombi na kuwaacha na kwenda kuwasikiliza wale wazee wa kichawi waliokuja nyumbani kwake.

> *"Sasa wakuu nafikiri tutaonana kanisani nina kazi moja muhimu, samahani sana."*
> *"Hakuna tatizo mkuu basi tufanye maombi."*
> *"Maombi si muhimu sana, mengine tutayafanya hukohuko kanisani, ilibidi niwe kauzu kukataa maombi yao ambayo kwangu sikuona umuhimu wake."*

Usaliti mwingine unaonekana kwa Mchungaji Joshua kwa mwanae ambaye anaamua kumtoa kafara ili aendelee kuwa na jina kubwa nje na ndani ya nchi:

> *"Baba……baba"*
> *"Naam mwanangu"*
> *"Nakufa baba….. nakufa baba"*
> *"Huwezi kufa mwanangu"*
> *"Hapana ushanitoa kafara"*
> *"Ha…ha…kuna"*
> *"Unabisha nini nawe usiku ulikuwa unanitoa kafara, sikulaumu baba najua ni shinikizo, angalia baba…. angalia tena ….tunakwisha"*

Usaliti mwingine unaonekana Mchungaji Joshua anapowasaliti wachawi wenzake na mkuu wao wa kuzimu kwa kukataa kumchinja mtoto wake kwa mikono yake mwenyewe na kuendelea kumtumikia mkuu wa kuzimu na wale wachawi.

Hivi ni vitu vinavyotokea sana katika jamii zetu. Watu wanasalitiana kwa mambo mengi sana ili kukidhi matakwa yao. Watu wengine hutoa watoto kafara kwa ajili ya mali, wengine husaliti ndoa zao kwa kuwa na vimada nje, wengine hutoa siri nzito za wenzao, wengine huvunja ahadi walizopeana na ndugu, jamaa, mafafiki hata wapenzi.

b) Mapenzi ya dhati

Pia katika kitabu hiki tunaona mapenzi ya dhati yaliyoko kwa Mchungaji Joshua na waumini wake, Mchungaji anapewa karama na Mungu naye anatumia kwa waumini wake kwa kuwafundisha neno la Mungu na kuwaponya magonjwa, pamoja na kuwatatulia shida zao. Kutokana na mapenzi walioonyeshwa na Mchungaji Joshua na wanamuonyesha mapenzi yao kwa kuungana na kujenga kanisa ili waweze kupata huduma nzuri na bora zaidi.

> *"Waumini waliweza kujenga nyumba ya kisasa pale kijijini na kuhakikisha wananinunulia pikipiki ya*

> *kunisaidia kufika kila kona kutoa huduma za kiroho. Kanisa lilibadilishwa toka la magunia hadi la matofali na bati juu. Mmoja wa watu waliojitolea ni mzee mmoja ambaye alikuwa na binti yake aliyepatwa na matatizo akiwa na miaka kumi wakati akitoka shuleni"*

Mapenzi mengine ya dhati yanaonekana pale watoto wa Mchungaji Joshua wanapofariki, Mchungaji na mke wake wanahuzunika sana na kuona kama Mungu amewaacha na kuwapa adhabu kubwa mno wasiyostahili.

> *"Mke wangu aliuweka uchungaji pembeni na kusahau kuwa ile ni kazi ya Mungu tuliyotakiwa kuipokea na kushukuru kwa kila alichotuahidi. Niliingia kazi ya kumbembeleza mke wangu huku watumishi wa kanisa hata sikujua walipata taarifa zile saa ngapi walifika kutufariji"*

Mapenzi mengine ya dhati yanaonekana kwa Mchungaji Joshua kwa mke wake kipenzi, ambaye anampenda sana mke wake; na hapo ndipo imani yake inapolegea na kutekwa na wachawi. Baada ya mke wake kuugua kwa muda na kumuombea bila mafanikio na kumpeleka hospitali bila nafuu, ndipo anapokubaliana kuungana na wachawi akiamini kuwa watamponya mke wake, kumbe anajitumbukiza kwenye matatizo makubwa zaidi:

> *"Niliamini ninapoelekea nilikuwa naingia kwenye shimo lisilo na mwisho lenye kiza kinene. Lakini sikuwa na jinsi hali ya mke wangu ilikuwa ikitia huruma kiasi cha kunifanya moyo wangu ukose amani. Kama watoto wangu karama yangu haikuwasaidia kitu niliamini hata mke wangu vilevile karama haitasaidia kitu"*

Katika jamii zetu pia tunaona kuwa kuna watu wenyemapenzi ya dhati na familia zao, ndugu zao, jirani zao na wengine, hata hufikia hatua ya kujitoa muhanga kwa jamii zao, nchi zao, na vyama vyao, ili mradi tu kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

c) Matabaka

Katika kitabu hiki tumeona kuwa kuna matabaka ya walichonacho na wasionacho. Mchungaji Joshua anatekwa na watu walionacho, watu wenye pesa kama vile wanasiasa na matajiri wakubwa na kusahau watu wa chini. Hivyo, kuwafanya watu wa chini kukosa huduma yake. Watu wa chini wanafukuzwa na walinzi wake na kudai kuwa hana nafasi ya kuonana nao, ila wenye pesa wanaruhusiwa kupita na kumuona Mchungaji na kutatuliwa matatizo yao. Na walionacho wengine wanataka waombewe peke yao nje ya kanisa au ofisini, kukwepa kuombewa katika kundi la watu wengi kanisani:

> *"Nilikwenda kwenye ofisi yangu kuonana na watu wenye shida ambao wana pesa, lakini hawakupenda kuombewa kwenye kundi la watu. Kwa kweli njia ile iliniwezesha kupata pesa nyingi za ahsante kwa muujiza niliokuwa nawafanyia"*

Tabaka lingine linaonekana pale Mchungaji Joshua anapopata msiba wa kufiwa na mtoto. Mkuu wa nchi anahudhuria mazishi na kumpa pole. Inaonekana siku zote ndege wanaofanana ndiyo wanaoruka pamoja. Hivyo, wote wanafedha ndiyo maana mkuu wa nchi ameweza kufika pale na kuhudhuria mazishi. Angekuwa mtu wa chini, asingeenda.

> *"Nilifarijika zaidi baada ya kumuona mkuu wa nchi kuja kunifariji na kunipa moyo kwa msiba ule mzito wa mtoto wangu"*

Pia katika jamii zetu swala la matabaka ni tatizo kubwa sana, ambao wenye nacho ndio huthaminiana na kusaidiana katika shughuli mbalimbali na kuwatenga wasionacho.

d) Migogoro

Mgogoro unaonekana kati ya Mchungaji Joshua na Mchungaji mwingine ambaye wanavutana kutokana na waumini. Mchungaji huyo anahubiri kweli kwa waumini wake na mitaani na kutoa siri za Mchungaji Joshua kuwa anatumia uchawi kuponya watu na kuvuta waumini kanisani kwake. Hilo, linaleta mgogoro kati ya Mchungaji Joshua na mwenzake. Hivyo, Mchungaji Joshua anamua kutumia uchawi wake kumwangamiza Mchungaji mwenzake, ila nguvu za Mungu zinamlinda Mchungaji yule:

> *"Tulikubaliana kwa kuwatuma vijana wetu kwenda kumchukua kwake ili kumgeuza ndondocha na kumpoteza kwenye himaya ya ardhi ile. Usiku tuliwatuma vijana wetu ambao walikutana na upinzani mkubwa wa kuona moto mkubwa kila walipokaribia ile nyumba ya nabii"*

Mgogoro mwingine unaonekana kati ya Mchungaji Joshua na mke wake, pale mtoto wao anapokuwa anaumwa na mke wa Mchungaji Joshua kumtaka Mchungaji afike nyumbani haraka sana ili kuokoa hali ya mwanao. Lakini Mchungaji hafiki kutokana na kumgonga mtu njiani na ku kucheleweshwa:

> *"Upo wapi mume wangu?"*
> *"Mke wangu mbona mkosi, nimegonga mtuna sasa hivi namuombea"*
> *"Mama yangu, muache huyo mwanao hali inazidi kuwa mbaya"*
> *"Nitamuachaje wakati nimeshaanza kumuombea, watu hawatanielewa hasa nikiwa mimi ndiye niliyemgonga"*
> *"Basi jiandae kuja kuona maiti ya mwanao"*

Mgogoro mwingine unaonekana kati ya mkuu wa kuzimu, wazee wachawi na Mchungaji Joshua, ambao unakuja kabla ya Mchungaji kujiingiza katika uchawi baada ya mkuu wa kuzimu kuona Mchungaji anawamalizia waumini wao, hivyo anaamua kuua watoto wawili wa Mchungaji ili wamteke Mchungaji, wawe kitu

kimoja. Na wa pili unakuja baada ya Mchungaji kukataa kumwua mtoto wake wa tatu kwa mkono wake mwenyewe na kuamua kumrudia Mungu.

Mgogoro mwingine ni wa nafsi. Mchungaji Joshua ana mgogoro na nafsi yake baada ya kumkana Mungu na kuingia katika mambo ya uchawi. Pia anasababisha kushindana na mambo mengi yanayomsumbua nafsi na kushindwa kumshirikisha hata mke wake:

> *"Kwakweli nilikuwa kwenye wakati mgumu sana kumueleza mke wangu juu ya uamuzi wa kumtoa kafara mwanetu wa pekee"*

Katika maisha yetu ya kila siku tunaona watu wengi wakiingia katika migogoro ya kinafsi na kijamii, au kindugu, au kimapenzi. Na hii inatokana na kutokuelewana kati yao, na kusababisha madhara makubwa katika familia na jamii kwa jumla. Migogoro hii pia husababisha ulemavu wa kudumu, au hata kifo, kwa sababu wakati mwingine inashindikana kutatulika na hatimaye kuleta madhara makubwa katika jamii.

e) Nafasi ya mwanamke katika jamii

Mwanamke huwa ana nafasi kubwa sana katika jamii inayomzunguka, na katika kitabu hiki tunaona mwanamke ameonekana katika nyanja mbalimbali kama mlezi, mshauri na muwajibikaji.

Kama mlezi, Mama Mchungaji (mke wa Mchungaji Joshua) anaonekana kama mlezi wa watoto wake watatu na mume wake. Yeye ndiye aliyeshika jukumu zima la kulea watoto na kuhakikisha wanakua katika misingi bora ya kimwili na kiroho:

> *"Mume wangu hali ya Samson siyo nzuri"*
>
> *"Mpe dawa na maombi, niache nilale kidogo nimechoka sana"*

Mwanamke amechorwa kama mshauri. Tunaona Mama Mchungaji akimshauri Mchungaji mambo mengi sana ya kifamilia na ya kiroho. Hata watoto wanapokuwa wanaumwa na kushindwa kupona kutokana na maombi, anamshauri mume wake wawapeleke hospitali. Pia alikuwa akimshauri mume wake na kumuonya juu ya kujiunga na wachawi. Hata wanapoona mambo yamezidi kuharibika na huko kwenye uchawi hakuna msaada wowote, anamshauri mume wake watubu na kumrudia Mungu:

> *"Mume wangu ni kweli tumemkosea Mungu na bado tunazidi kumkosea, kuna faida gani kubeba dhambi na bado kizazi chetu kinakwisha?"*
> *"Sasa tufanyaje"*
> *"La muhimu tumrudie bwana kwani alituahidi milango yake ipo wazi muda wote kuwapokea waliopotea"*

Mwanamke kama muwajibikaji, katika kitabu hiki tunaona jinsi Mama Mchungaji anavyowajibika na kujituma katika kazi mbalimbali za nyumbani na hata kanisani. Tunaona pindi mume wake anaposhindwa kwenda kutoa huduma za kiroho kanisani kwa sababu ya safari au maradhi, yeye anakwenda na kutoa huduma hiyo kanisani.

Katika jamii yetu ya Kitanzania mwanamke anaonekana akikabiliwa na majukumu mengi, kama vile malezi, ushauri, uwajibikaji wa kazi za ndani na nje na mtunza familia. Kwa kweli mwanamke ni nguzo muhimu sana katika familia na jamii kwa jumla.

4.3 Ulinganishaji wa Kidhamira katika Nyimbo za Bongo Fleva na Hadidhi Fupi za Magazeti ya Udaku

4.3.1 Mwongozo wa Usaili kwa Watu wa Makamo, Viongozi wa Dini na Wanasiasa

Kundi hili asilimia kubwa wanauelewa muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku, ijapokuwa wengi wao siyo wapenzi wa muziki huu, wala Magazeti ya Udaku. Wanadai kuwa vitu hivi vinapendwa zaidi na vijana na kwa asilimia kubwa vinahusu vijana na kugusia maisha yao ya kila siku. Kundi hili halina tabia ya kusikiliza sana nyimbo za Bongo Fleva, bali hutokea mara moja moja sana katika sehemu walizopo, au wanaposafiri ndani ya mabasi ambapo hulazimika kuusikiliza au kwenye sherehe mbalimbali pindi wanapoalikwa hulazimika kusikiliza muziki huu. Na wakati mwingine, kupitia Magazeti ya Udaku kutokana na yanayojitokeza juu ya kichwa cha habari, ijapokuwa siyo mara nyingi.

Wanasema kuwa jamii inaweza kujifunza jambo juu ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi za magazetini kutokana na kilichoimbwa au kuandikwa katika muziki huo na magazeti hayo. Ijapokuwa wanadai siyo nyimbo zote zina maudhui mazuri katika jamii na nyingine huwa zinaimbwa tu, ila ukichunguza huwezi kupata uchanya wa maudhui ya nyimbo hizo wala hadithi hizo. Jamii huweza kujifunza mambo mengi juu ya muziki wa Bongo Fleva kutokana na maudhui yaliyopo katika muziki huo na magazeti hayo, kama kuelimisha jamii, kuburudisha, kutoa mwongozo na kujifunza juu ya matukio mbalimbali kama vile masuala ya siasa, dini, mapenzi, elimu, maisha kwa jumla na mengineyo.

Dhamira zilizopo katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana kwa asilimia kubwa, maana wote huzungumzia mambo

yanayogusa jamii inayotuzunguka. Kwa mfano, umasikini, mapenzi, imani, malezi, matabaka, uchawi, usaliti, unyanyasaji wa kijinsia, migogoro na nafasi ya mwanamke katika jamii. Mambo yote haya ni mambo yanayotokea katika jamii zinazotuzunguka na huwa yapo kila siku. Hivyo, ukisikiliza nyimbo zilizotungwa na watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva zinagusa maisha ya kila siku katika jamii, na hadithi zinazotungwa na waandishi wa vitabu au hadithi fupi zinahusu mambo yaliyoko katika jamii. Hivyo, dhamira zao zinafanana kutokana na maudhui yaliyoko katika nyimbo zao na hadithi zao, vyote vinagusa maisha ya wanadamu ya kila siku.

4.3.2 Mwongozo wa Usaili kwa Wanafunzi na Wanachuo

Wanafunzi na wanachuo wengi wanauelewa muziki wa Bongo Fleva, na wanasema kuwa ni muziki wa Kitanzania, unaopigwa na kuimbwa na wanamuziki wa kitanzania, hujulikana pia kama muziki wa kizazi kipya, ikimaanisha wa rika la kati lenye kuwahusu zaidi vijana wa kike na wa kiume. Magazeti ya Udaku ni aina ya vipashio vya habari kwa njia ya chapa yenye kuelezea visa na matukio yanayotokea katika jamii. Wanamuziki wa Bongo Fleva ni wengi mno lakini baadhi yao ni **Diamond, Lady Jay Dee, Fid Q, Mwana Fa, Juma Nature, Linex, Barnaba, AY, Mwasiti, Lina, Nick wa Pili,Professa J, H- Baba, Ney wa Mitego, Recho** na wengine. Waandishi wa hadithi fupi ni kama vile **Irene Mwamfumpe Ndauka, Ally Mbetu, Osca Ndauka, Faki .A. Faki** na wengine.

Misukumo inayowapata watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku ni pesa, kujulikana katika jamii, matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii, kama vile mapenzi, siasa, imani, umasikini, ukosefu wa ajira, majanga na mengineyo. Dhamira zinazojitokeza katika muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku zinatoka katika changamoto za jamii husika, dhamira zilizopo katika

muziki wa Bongo Fleva na hadithi za magazetini kwa asilimia tisini zinafanana kwa kuwa mambo yanayozungumziwa ni yale yale yanayogusa jamii au yaliyomo ndani ya jamii. Siyo kweli kwamba muziki wa Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku havina mchango wowote katika jamii, vina mchango sana, ila dhamira zao nyingi zimekuwa zikijikita zaidi katika mapenzi, ambapo nyimbo nyingi huimbwa bila ufundi mkubwa, wala ubunifu na kushindwa kujikita zaidi katika vipengele vingine. Maoni ya kundi hili juu ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku wanatakiwa kufanya utafiti kwenye jamii kabla ya kutoa kazi zao, hasa hasa wanamuziki. Jamii ina mambo mengi yanayoikumba zaidi ya wanavyofikiria, kama vile rushwa, ufisadi, uvivu, na kadhalika, yanatakiwa kuangaliwa pia kwa wingi na siyo kujikita zaidi katika suala la mapenzi tu.

4.3.3 Mwongozo wa Mjadala wa Vikundi kwa Washabiki wa Muziki wa Bongo Fleva na Wasomaji wa Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku.

Kundi hili lina ufahamu vema muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku. Vile vile ni wafuatiliaji wazuri wa nyimbo za Bongo Fleva na mtiririko wa hadithi zilizopo katika Magazeti ya Udaku. Wanawafahamu vema wanamuziki hawa, **Lady Jay Dee, Diamond, Linex, Nick wa Pili na Profesa J** na baadhi ya nyimbo zao pia kama vile **Ndiyo Mzee, Sitaki kazi, Moyo wa subira, Mama Halima, Nasimama, Ngekewa, My number one, Historia** na nyingine nyingi. Pia wanawafahamu waandishi wa hadithi fupi kama vile **Irene M Ndauka, Ally Mbetu, Oscar Ndauka, na Faki A Faki** na hadithi zao kama vile, **Godoro la Mtumba, Utamu wa lifti ya Bodaboda, Familia ya kichawi, Niliolewa na Wanaume Watatu, Kutoka Uchungaji Mpaka Mkuu wa Wachawi, Nusu Siku Ndani ya Jeneza, Mimba ya Jini** na nyinginezo.

Wanamuziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku, wengi wao, ni watunzi wazuri sana ila kuna baadhi wanatakiwa kujirekebisha kwa kuwa nyimbo nyingine na hadithi nyingine zina maudhui mepesi mno. Pia wengi wao wanajikita sana katika swala la mapenzi na kusahau maswala mengine ambayo ni ya muhimu pia katika jamii wanayoizunguka. Vile vile, waimbaji wa muziki wa Bongo Fleva wengine hawana maadili katika mavazi, kwakuwa wanavaa nusu uchi na kuacha sehemu za miili yao nje bila kujali jamii inayowazunguka. Hivyo, yawapasa kuvaa vizuri na kufuata taratibu za Kitanzania na siyo kuiga mambo ya watu wa nje yasiyokuwa na maadili na kusahau utamaduni wetu.

Katika muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku, kuna dhamira nyingi zinazoelimisha jamii kwa jumla, kama vile kuelimisha, kuburudisha, kuonya, kukosoa, kutoa mwongozo na nyinginezo. Dhamira zilizopo ndani ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana kwa kiwango kikubwa kwa kuwa vitu ni vile vile vinavyozungumzwa katika jamii. Muziki huu na magazeti haya vina maana sana katika jamii zetu, kwani hutoa maonyo, mafunzo na miongozo katika jamii. Kinachotoa sifa mbaya kwa muziki huu ni jinsi ya baadhi ya wanamuzikii wanavyovaaa nusu uchi na kuharibu maadili ya Kitanzania. Pia katika magazeti kuweka picha za kihuni na kwa asilimia kubwa kutupiana maneno yasiyokuwa na maadili ya Kitanzania.

Watu ambao hawasikilizi muziki wa Bongo Fleva, wala kusoma Magazeti ya Udaku, wajitahidi kusikiliza kwani kuna baadhi ya nyimbo zinatoa mambo mazuri na kujifunza mengi katika maisha kama vile nyimbo za **Sitaki kazi, wa Nick wa pili; Starehe wa feruz; Nasimama wa Lady Jay Dee** na nyingine nyingi. Pia hadithi nyingi zinafundisha jinsi ya kuepukana na mambo mengine katika jamii, au jinsi ya

kumkimbilia Mungu katika shida zako na kuachana na mambo mengine kama vile, **Kutoka Uchungaji Hadi Mkuu wa Wachawi, Godoro la mtumba, Lifti ya Bodaboda**, na nyingine nyingi. Ukisoma hadithi hizi unajifunza mambo mengi katika maisha na kujua jinsi ya kuepuka misukosuko unayokumbana nayo katika maisha ya kila siku.

4.4 Jinsi Dhamira za Muziki wa Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku Zinavyofanana

4.4.1 Dhamira za Muziki wa Bongo Fleva Zilizojitokeza, Kutoka kwa Wanamuziki Teule

Namba	Dhamira	Nasimama - Lady Jay Dee	Mama Halima - Linex	Safari - Diamond	Sitaki Kazi -Nikki wa Pili	Ndiyo Mzee –Profesa J
1	Imani	✓	✓	✓	✓	-
2	Unafiki	✓	✓	-	-	✓
3	Elimu	✓	✓	✓	✓	✓
4	Usaliti	✓	✓	-	-	✓
5	Mapenz	✓	✓	✓	-	✓
6	Migogoro	✓	✓	-	✓	✓
7	Nafasi ya Mwanamke katika Jamii	-	✓	✓	-	-
8	Umasikini	-	✓	✓	✓	✓
9	Ajira na kujitegemea	✓	✓	✓	✓	-
10	Siasa	-	-	-	✓	✓
11	Ndoa	-	✓	✓	-	-
12	Malezi	-	✓	✓	-	-

4.4.2 Dhamira za Hadithi Fupi Zilizojitokeza, katika Magazeti ya Udaku za Waandishi Teule

Namba	Dhamira	Godoro la Mtumba - Irene Ndauka	Toka Uchungaji Mpaka Mkuu wa Wachawi – Ally Mbetu
1	Mapenzi	✓	✓
2	Nafasi ya Mwanamke Katika Jamii	✓	✓
3	Kutojitambua	✓	✓
4	Migogoro	✓	✓
5	Uchawi	-	✓
6	Usaliti	✓	✓
7	Matabaka	-	✓
8	Imani	✓	✓
9	Malezi	✓	✓
10	Umasikini	✓	✓
11	Elimu	✓	✓
12	Ndoa	-	✓
13	Ajira	✓	✓
14	Unyanyasaji wa Kijinsia	✓	-

Namba	Dhamira	Nasimama –Lady Jay Dee	Mama Halima – Linex	Safari - Diamond	Sitaki Kazi – Nikki wa Pili	Ndiyo Mzee – Profesor J	Godoro la Mtumba – Irene Ndauka	Toka Uchungaji Mpaka Ukuu wa Wachawi – Ally Mbetu
1	Imani	✓	✓	✓	✓		✓	✓
2	Unafiki	✓	✓	-	-	✓	✓	✓
3	Elimu	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
4	Usaliti	✓	-	-	-	-	✓	✓
5	Mapenzi	✓	✓	✓	-	✓	✓	✓
6	Migogoro	✓	✓	-	✓	-	✓	✓
7	Nafasi ya Mwanamke	-	✓	✓	-	✓	✓	✓
8	Umasikini	-	✓	✓	✓	-	✓	✓
9	Ajira na kujitegemea	✓	✓	✓	-	✓	✓	✓
10	Siasa	-	-	-	✓	✓	-	-
11	Ndoa	-	✓	✓	-	-	-	✓
12	Malezi	-	✓	✓	-	-	✓	✓
13	Unyanyasaji wa Kijinsia	-	✓	-	-	-	✓	-
14	Kutojitambua	✓	✓	-	-	✓	✓	✓
15	Uchawi	-	-	-	-	-	-	✓
16	Matabaka	-	-	-	✓	✓	✓	✓

4.4.3 Ulinganishi wa Kidhamira wa Nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi Fupi za Magazeti ya Udaku

Kwa asilimia kubwa dhamira zilizopo ndani ya muziki za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana sana, na hii inatokana na kuchunguza baadhi ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, kama zinavyojionyesha katika majedwali hapo juu. Vitu hivi viwili vina malengo sawa katika jamii na vyote vinalenga kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, kutoa muongozo katika jamii, kufichua uovu katika jamii na kutoa muelekeo wa mambo mazuri katika jamii. Nyimbo zilizotumika katika utafiti huu na vitabu vilivyotumika vina dhamira zinazofanana kwa asilimia kubwa kama tuonavyo katika uchambuzi wa nyimbo hizi na vitabu hivi hapo juu.

4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imeangalia mambo mbalimbali yanayohusiana na utafiti wetu. Nayo ni msukumo wa watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, kubainisha dhamira zinazopatikana katika kazi hizo na kulinganisha dhamira zilizopo katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Sura inayofuata ni ya mwisho, itatoa utangulizi kwa ufupi na muhtasari wa kazi hii, kuhusu sura zilizopo katika kazi na zinahusiana na nini, utoshelevu wa nadharia iliyotumika, mchango mpya wa utafiti huu na maoni na mapendekezo kuhusu utafiti huu na tafiti zijazo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa ufafanuzi wa mchakato mzima kwa muhtasari. Kuangalia kuna sura ngapi katika kazi na kila sura inahusiana na nini. Pia, sura hii inaangalia utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika utafiti huu na mchango mpya wa utafiti huu. Mwisho kabisa sura hii, inatoa maoni na mapendekezo kuhusu utafiti huu na tafiti zijazo.

5.1 Muhtasari

Ripoti ya utafiti huu ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inatambulisha usuli wa tatizo la utafiti. Sura ya pili inajumuisha mapitio ya maandiko na nadharia zilizotumika kama mwega wa utafiti. Sura ya tatu inafafanua mbinu za utafiti, pamoja na uwasilishaji na zana mbalimbali zilizotumika katika utafiti; ukusanyaji pamoja na uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyojumuishwa ni mpango wa utafiti, eneo la utafiti, taarifa za walengwa wa utafiti, vifaa vya kukusanyia data pamoja na udhibiti wa data. Sura ya nne inajumuisha suala la uchanganuzi wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti ambapo kila lengo mahsusi litabeba maudhui katika utafiti huu. Sura ya tano inajumuisha utangulizi, muhtasari, utoshelevu wa nadharia iliyotumika, mchango mpya wa utafiti na maoni ya mapendekezo kuhusu utafiti huu na tafiti zijazo. Pia kuna viambatanisho mbalimbali kama vile picha na vielelezo vihusianavyo na na utafiti huu.

5.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Nadharia iliyotumika ni ya upokezi/ mwitikio wa msomaji katika kuchunguza dhamira zilizopo ndani ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya

Udaku. Nadharia hii imelinganishwa na hali ya kijamii na jinsi kazi hizi zinavyoashiria uhalisia katika jamii kutokana na dhamira zake. Vile vile nadharia hii imefanya kazi kubwa ya kutuongoza kuangalia nyimbo na hadithi kama njia maalum ya kuchanganua dhamira. Nadharia hii inatuonyesha kuwa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, zinafanana kutokana na kuwa na sifa zinazofanana. Hivyo, nadharia hii imetosheleza utafiti huu kwa kuwa jamii hujifunza kwa upokezi na usomaji wa kazi za namna hii, ili kupata ujumbe au maudhui kutoka kwenye kazi hizi au kwa wasanii hawa.

5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Utafiti umebaini kuwa kuna ulingano wa kidhamira katika nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Jambo linalosababisha dhamira zao kulingana au kufanana, tunadhani kuwa ni malengo yanayofanana ya wasanii hawa katika kuelimisha jamii. Na hili limebainishwa vizuri kwa kutumia nadharia ya upokezi/mwitikio wa msomaji katika kuchunguza dhamira zilizopo ndani ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Yaani, kwa ufupi, zote zina malengo ya kuelimisha jamii, kuburudisha jamii, kutoa muongozo katika jamii, kukosoa jamii na kukemea maovu katika jamii. Hivyo, tunaona lengo la nyimbo na hadithi ni moja katika jamii na dhamira zake zinafanana.

5.4 Maoni na Mapendekezo Kuhusu Utafiti Huu na Tafiti Zijazo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu maoni yetu ni kwamba:

Kuna tafiti nyingi ambazo zimewahi kufanywa kuhusiana na muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku kama tulivyogusia hapo nyuma. Miongoni mwa tafiti

hizo ni, matatizo yanayowakumba wanamuziki wa Bongo Fleva katika harakati zao za kujikwamua kutoka katika tatizo la ukosefu wa ajira, uchunguzi wa lugha unaofanywa na wanamuziki wa hip hop, matumizi ya misimu katika muziki wa Bongo Fleva, tasnifu ya hadithi kwa kuchunguza athari ya dhamira katika uteuzi katika hadithi fupi teule za Kiswahili na utafiti katika hadithi fupi za Kiswahili, pamoja na utafiti huu ambao ulikuwa unaangalia ulinganishi wa kidhamira katika nyimbo za Bongo Fleva na hadidhi fupi za Magazeti ya Udaku. Utafiti wa namna hii ni tukio mahususi ambalo limeangalia na kulinganisha dhamira zilizopo ndani ya muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Licha ya kuwa utafiti wa namna hii umeziba pengo lililokusudiwa kuzibwa, lakini bado kuna maeneo mengi ya kuzamia kuchunguza zaidi. Maeneo hayo ni pamoja na:

a) Athari za muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku katika kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili fasaha.
b) Muonekano wa waimbaji wa muziki wa Bongo Fleva na uchapishaji wa picha katika Magazeti ya Udaku katika kumomonyoa maadili ya Kiafrika.
c) Matumizi ya lugha katika muziki wa Bongo Fleva na uandishi wa hadithi fupi za Magazeti ya Udaku katika kupotosha lugha.

5.5 Hitimisho

Kwa jumla, utafiti huu umeibua eneo jingine la kujifunza dhamira zilizopo ndani ya nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, na kuziona zinafanana na zina lengo moja katika jamii. Pia utafiti huu utasaidia kubadili mitazamo ya baadhi ya watu, hasa wale wa makamo na viongozi wa dini kuona kuwa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku vina mchango mkubwa wa kujenga jamii mpya isiyo na malumbano, vita, wala chuki, na watu

kuishi kwa raha mustarehe. Maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika sura hii yakipewa umuhimu na wasomi wengine, ni imani ya utafiti huu kuwa yatatoa mchango mkubwa katika kuijenga na kuipanua Fasihi ya Kiswahili.

MAREJELEO

Askew, K (2002), 'Perfoming the nation', Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania, Chicago & London, The University of Chicago.

Balisidia, M. L. (Matteru) (1987), Tanzu na Fasihi Simulizi, Mulika Na. 19.TUKI. Dar es Salaam.

Chachage, SL (2002), 'Ndani ya Bongo', Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni', Idara ya Sosholojia, chuo kikuu cha Dar es salaam.

Englert B (2003), Bongo Flava Still Hidden Underground Rap From Morogoro, Tanzania, Strichproben, Winer Zeitchrift fur Kritische Afikastudien. 3, 73-93.

Fenn J& Perrullo A (2000), A language choice and hip hop in Tanzania in popular Music and Society, University of Bowlinn, Green city.

Finnegan, R (1970), *Oral literature in Africa*, *clarendon Press*,Oxford, Part II. Kimani Njogu & Richard M. Wafula (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Sai Industries ltd, Nairobi.

Kahigi K.K (1995), *Lugha Katika Vitabu vya Watoto*. In Kahigi KK (Ed) Kioo cha Lugha , Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi, Idara ya Kiswahili, Chuo cha Dar es salaam, uk 145-166.

Kimani Njogu & Richard M. Wafula (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Sai Industries ltd, Nairobi.

Kirumbi, P (1977), *Misingi ya fasihi simulizi*, Shungwaya, Nairobi.

Kothari, C.R (2009), Research Methodology: Method and Techniques (2nd Revised Edt.), New Age International Publishers Ltd, New Delhi.

Kraidy MM (1990), The Local, The Global and the Hybrid: A Native Ethnography of Globalization. Critical Studies in Media Communication, 16(4), 456-477.

Kuhenga, C. (1980), *Nahau za Kiswahili, Jendwali la Misemo ya Lugha*. Arusha, Tanzania: Eastern Afrca Publications.

Madumulla, J (2009), *Riwaya ya Kiswahili*, Nadharia, Historia na Misingi ya Kiswahili, Mture Educational Publishers Limited, Dar es salaam.

Mangesho, P (2003), Global cultural trends, the case of hip-hop music in Dar es salaam, MA Dissertation, University of Dar es salaam.

Matteru, M. (1993), *Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili*. FASIHI. Makala za Semina ya kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili iii.TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mazigwa, S A (1990), *Fasihi ya Kiswahili* , BPN,Peramiho.

Msokile, M (1992), *Kunga za fasihi na lugha*, Education Publishers and Distributors Ltd, Dar es Salaam.

Msokile, M (1992), *Kunga za Fasihi na Lugha*, EPD, Kibaha.

Msokile, M (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Saalam University Press Dar es Salaam.

Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. EAEP ltd, Nairobi.

Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. EAEP ltd, Nairobi.

Msuya,S. K (1979), *Yatokanayo na fasihi simulizi*, TPH, DSM.

Muhando, P & Balisidya, N (1976), *fasihi na sanaa za maonyesho*, TPH, Dar es salaam.

Mulokozi, M. M (1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Mulika Na. 21: 1-24.

Mulokozi, M. M (1990), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Njogu, K & Chimerah, R (1999), *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omari, C K & Mvungi, M (1981), *Urithi wa utamadumi wetu*, TPH. DSM.

Omari, S (2006), *Mitindo na Matumizi ya Lugha Katika Muziki wa Kizazi Kipya*, katika Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 69:73-93.

Omari, S (2009), *Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature*, Unpublished Phd Thesis, University of Dar es salaam.

Perrullo A (2003), '*The life that live'*, popular urban practice and agency in Dar es salaam, Tanzania, Phd, dissertation, India Unversity.

Perrullo A (2005), 'Hooligans and heroes',Youth identity and Hip hop in Dar es salaam, Tanzania, Africa today, vol 51, no4, pp 74-101.

Perullo A (2007), *Heres a Little Something Local An Early History of Hip hop* in Dar es salaam, Tanzania 1984-1997. Dar es Salaam: The History of Emeging East Africa Metropolis, ed by Andrew Burton, James Brennan & Yusuf Lawi. London: British Institute and James currey. Uk 250 – 273.

Remes, PW (1998), Karibu Geto Langu/Welcome in my Ghetto "Urban Youth Popular Culture and Language in 1990s Tanzania Phd dissertation, Howard University (University Microfilms No. 9832973)

Reuster-Jahn, (2007), lets Go Party! Discourse and Self- Potrayal in Bongo Fleva Song Mikasi ('Sex'-Ngwair) Swahili Forum, 14,225-244.

Robert, S (1992), *Kielelezo cha fasihi. Mkuki na Nyota*, Dar es salaam.

Sengo, I S Y (1978), *Taaluma ya fasihi nadharia ,mitazamo na mbinu katika fasihi simulizi*, TUKI, University of Dar es Salaam.

Senkoro FEMK Rethinking Popular Arts & Culture in the 21st Century East Africa, Celebrating 30yrs CODESRIA. 2003.

Senkoro, F E M K (1987), *fasihi na jamii*, PPC, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K (1982: 8), *Fasihi*. Dar es Salaam: Press Publicity Center.

Syambo, B & Mazrui, A (1992), *Uchambuzi wa fasihi*, EAEP, Nairobi

VIAMBATANISHO

NYIMBO TEULE ZA MUZIKI WA BONGO FLEVA NA WAANDISHI TEULE WA HADITHI FUPI ZA MAGAZETI YA UDAKU KWA WASANII TEULE NA WAANDISHI TEULE.

NYIMBO TEULE ZA MUZIKI WA BONGO FLEVA

LADY JAY DEE, NASIMAMA

Kiitikio- Aliyepanga ni manani shida na riziki zangu, aliyezitupa gizani shida na tabu zangu.

1. Nasima na Mola kwa kila jambo lile nitendalo, maneno ya watu bakora yalinichapa nikaumia; lakini machozi machozi nilolia zamani yashafutikaa. Japo simanzi machozi yalojaa moyoni nikikumbukaa, nilishaambiwa zamani kinyago ukichongacho hakikutishi ng'oo, ndiyo maana nasimama nalia kwako.
2. Ukitazama kwa macho yako huwezi kumjua mwema, mateso yako furaha yao tena mengi watasema. Moyo wa mtu kichakaa mengi yalofichikaa, naye mdhania mwema kumbe mchawi kwako. Nilishaambiwa zamani kinyago uchongacho hakikutishi ng'oo ndiyo maana nasimama nalia kwako.

   Shida zangu ohhh

   Shida zako ohhh

LINEX, MAMA HALIMA

Kanchuti kuna maaa x3

1. Nilivyokuacha na nilivyokukuta ni tofauti tofauti kabisa, sitaki kugombana na wewe niambie nini kilikukuta inaonyesha na iko wazi unamimba ya miezi sita. Kama unavyojua sijawahi kutembea na wewe, kama unavyoelewa lakini mpaka nikuoe. Mi kwako ulinidanganya utanipenda kwa moyo wote, maisha hayataki haraka Mungu amekuponza weee. Mama Halima weee, Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima wee umesahau ahadi ni deni. Umevunja ahadi yetu tulopanga mimi na wewe kwamba mimi nikatafute hata nikikosa nije nikuoe.

Kiitikio - Mama Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima weee umesahau ahadi ni deni.

2. Nyumbani kwenu wanataka kujua baba wa mtoto, yule bwana uliyempenda kageuka moto x2. Natamani nisahau yalopita ili tugange yajayo, jicho lako linanishawishi nisahau salamu zao, wanasema ukipenda boga upende na ua lake. Wanasema unifai tena bora mi nikuache, Mama Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima weee umesahau ahadi ni deni. Umevunja ahadi yetu tulopanga mimi na weee, kwamba mimi nikatafute hata nikikosa nije nikuoe; Mama Halima eee umesahau ahadi ni deni, Halima wee umesahau ahadi ni deni.

3. Maisha ni safari wote tupo safarini, ndoto zangu zimeyeyuka bado sijakata tamaa najua yote mitihani ya dunia nakuombea maisha mema Halima wee. Umevunja ahadi yetu tulopanga mimi na wewe mimi nilipanga nikatafute

hata nikikosa nije nikuoe. Halima weee umesahau ahadi ni deni, Halima weee umesahau ahadi ni deni. Jua yote mitihani ya dunia nakuombea maisha mema, mi nakuombea, inatokea inawakuta watu, inatokea na inawakuta watu.

DIAMOND, SAFARI

1. Ahhh vipi mizigo umeshaweka tayari, nisije chelewa nikajaachwa na gari, basi jikaze usilie mpenzi, mi nitarudi niombee kwa Mwenyezi. Zile taabu na njaa msimu mzima, mavuno hakuna huwa nakosa raha pale mkikosa cha kutafuna. Roho yangu inauma sema nitafanya nini na pesa sina, na kuonea na huruma, bora niende mjini kusaka Tumaa.

   Kiitikio- Kama watoto wakinililia waambie kesho nitarejea, wadanganye kwa vibagia waambie pipi nitawaletea. Kama watoto wakinililia waambie kesho nitarejea, usichoke kuvumilia na kila siku kuniombea, nirudi salama.

2. We unajua kwamba na sina roho nitakuwa na wasi wasi iii ubaki na moyo utajaa wasi wasi iii. Napokuwa nakwenda shambani halafu nipo peke yangu honey, napokuja kuona majirani nitaumia, pale napotoka kisimani ama nipo na kuni kichwani sina wa kunitua nyumbani nitaliaa.

   Maneno yako yanafanya nakosa raha na mawazo, hata mwenzio sijawai kufika dar huu ndo mwanzo ooo, pili nakwenda nasijui pakukaa wala mavazi ohhh; we niombee niepushwe na balaa na maradhi ooo eee.

3. Unapoenda kama ukifika salama utukumbuke na sisi, usisahau kama mkeo na wana umetuacha na dhiki.

Hilo usijali ila naomba chunga sana ogopa na marafiki, wakikulaghahi hata kwa mbegu za mtama waambie sidanganyiki x2.

NIKKI WA PILI FIT BEN POL, SITAKI KAZI

Kiitikio - Utamaduni wangu nikuuliza why why why why why why x2

Nimekataa kuwa mtumwa najituma eee eee eee

Kataa kuwa mtumwa jitume eee eee eee

Form six degree hadi masters sitaki kazi, wana vyeti mtaani vijana, hawana kazi. Natengeneza ajira, mtaa niupe kazi.

1. Uko na wasi wasi mtu bila nafsi umeajiriwa shirika la mtu binafsi, sina wasiwasi mtu mwenye nafsi sijaajiriwa nimeajiri yangu nafsi. Mishaara imejaa makato biashara mjini ndo zimejaa mapato, ajira itakulinda toa vyeti, siitaji kulindwa mimi sio mtoto wa geti kali. Kazi ni mpaka wa akili yako, mpaka ufukuzwe kazi ndiyo ugundue kipaji chako, ajira ya mkeo chini ya boss we ni house girl pekee ndiyo anakuita boss. Sivai tai sikatai utamaduni wangu mi nikuuliza why, elimu bongo imekosa plani ya pili, ahufundishwi kuwa tajiri.

2. Wanasema eti singo na jingo mzee naelekea kuwa boss kiroho zee, Nick na binti mzuri nikuozee, mi bado sipo vizuri nipozee. Nakuza network najuana na watu nauza network naungana na watu, nakuza yangu keki napunguza za watu, keki baada ya Mungu ni mzungu alafu mimi. Oviously unataka mtoto mwenye akili serious fanyafanya uzae na Nick wa pili genious. Sitafuti kazi nataka nitafutwe na wanaotafuta kazi,

kuimba mziki kazi ya Mungu sitaki kazi ya mtu haki ya Mungu aaa kazi ni kipimo cha mtu, amka umekunja sura kipimo cha mtu.

PROFESSOR JAY FIT JUMA NATURE, PROFESSA J

Naam ndugu wananchi mc wenu babu Ayubu nawaleeteeni habari japo kwa ufupi, kuhuusiana na huyu ndugu yetu Joseph Haule mpeni kura zenu za ndio kwasababu yeye ni mpenda watu, mpenda amani na mtu mwenye huruma kwa wananchi wote. Kwahiyo basi ninawaomba wananchi mumpe kura yake ya ndiyo, hivyo basi wananchi tafadhali namkaribisha mgombea mtu, ndugu Joseph Haule ili aweze kuzungumza na wananchi.

1 Ok ok naitwa Joseph Haule nadhani nimeletwa niokoo hiki kizazi, mimi ni mwana siasa niliyebarikiwa na Mungu nadhani nimeletwa niokoe hiki kizazi. Nimeletwa kwenu ili niwapunguzie machungu mimi ni mteule tangu enzi za sahara, ndiyo maana nimetunukiwa hii zawadi na hekima kuliko Mfalme Suleimani. Msiwe na wasi na hii itafahamika pindi mtakaponipa nafasi, actually nimedhamiria kuwasaidia Taifa lenye nguvu liwe Tanzania, jamani makofi basi tafadhali. Ni mambo madogo tu nadhani nitarekebisha mkinipa visiku vichache, uchumi utapanda ghafla bin vuu, nataka mpaka matonya afundishe Chuo Kikuu nchi ya Tanzania itang'ara kishenzi. Na nitahakikisha kila baamedi anamiliki benzi, mtafurai dada zangu jamani "ndiyo" basi endeleeni kunisifu kwa nyimbo na mapambio "ndiyo" nipeni basi jamani hiyo nafasi, hamuoni hali ni mbaya, nataka kuigeuza Tanzania kama Ulaya. Cha kwanza nitafuta umasikini, wanafunzi mtafanyia practical mwezini, kwenye mahospitali nitamwaga maji kama mchanga. Nitafungua akaunti kwa watoto wachanga, mabomba yatatoa maji na maziwa nchi nzima, watu

watasahau habari za visima. Nina wafadhili hatari waweza kutengeneza ndege, kila mtu awe na yake makonda na wapiga debe.

Kiitikio- Si mtafurai Watanzania jamani "Ndiyo mzee"

Si kweli inakubalika jamani "Ndiyo mzee"

Basi mie mkombozi wenu jamani "Ndiyo mzee"

Na nitafuta shida zenu zote "Ndiyo mzee"

Hivi ni nani ni vijimambo tu "Ndiyo mzee"

Na vinanikera kweli kweli "Ndiyo mzee"

Basi hali itabadilika sawa "Ndiyo mzee"

Na hatamu tutaishika ok "Ndiyo mzee"

2) Wafanyakazi wa serikalini nashangaa hamna magari, yani hata mikweche hahaaa hii ni hatari. Nina mpango wa kuongeza mishahara iliyo minono mara mia moja ya ile ya kwanza, iliyowafanya mfanye migomo. Nitawapa nyumba nzuri na magari ya kifahari watu watashangaa mtakapopita kila mahali, wakulima kila mmoja nitampatia trekta nafikiri hii itasaidia kuinua sekta, tauza na mboga zenu bilioni kwa bilioni. Watu watabaki midomo wazi kama wamekamatwa ugoni, walimu hizi zawadi zenu nimezificha moyoni nadhani mtazimia siku mkizitia machoni, we acha tu mtafurai ninyi ila hapo hapafai mkimuweka mtu mwingine niwekeni mimi. Polisi wote mi nawasifu jinsi mnavyokwenda sahani moja na waalifu, sasa kila mmoja nitampatia helkopta nadhani hiyo hata mmoja hajawai kuota. Hivyo, Watanzania mtalala milango wazi infact na uhakika wa kuzuia waizi. Nitajenga barabara tano tano juu na chini, nitajenga nyumba za starehe baharini, nitapenda kuiga mshumaa kumulikia wenzangu, mtakao yumba kiuchumi tutagawana vya kwangu.

2 Ndugu wana nchi kuna mtu anaswali kutoka kwa mgombea? Nauliza hivi kuna mtu anaswali, basi ajitokeze ili aweze kuuliza swali.

Nyie ndugu zangu huyu msimpe uongozi siyo mzuri muongo tu, mnafiki na kiburi si mzuri anaongopea sana, sijui kazaliwa muda gani alfajiri au alasiri au wakati wa mvua zile za kipindi kile. Amepitapita skuli lakini mambo yake si mazuri wala tusimtetee atatuangamiza, kwanza kasubirii weee uchaguzi, tumemfuma kwa kalimanzira anakatisha, kalimanzira akamwambia shida yako elezea fasta kabla jini ajapanda. Ajakaa vizuri mashetani si yakamuanza kimbunga akajichanja, tulisikia akisema kwa sauti kubwa ya kukaripia waungwana mnisaidie ndio. Mtamueleza uongo mtupu ameliwa waungwana wamempeleka chau mpaka kaibiwa hamna tafu na babu kawehuka.

Hajatulia huyu mpepeeni, huhuhuu ni sauti iliyosikika kutoka kwa mzee wa pembeni sijui msaidizi mganga au mpelelezi, na kwa taarifa yako uongozi upati ng'o labda urudi kwenu urudi ukavunje tunguri na hao waganga wako waeleze upati kitu hapa ata utoe chapaa.

Kiitikio- Wananchi mmesikia Ndiyo Mzee

Kuwa jamaa hatufahi Ndiyo Mzee

Na inafaa kumchukia Ndiyo Mzee

Hatumtaki aondoke zake Ndiyo Mzee

Tusifuate maneno yake Ndiyo Mzee

Tunahakikisha hatumchagui Ndiyo Mzee

Kwasababu jamaa ni mnafiki Ndiyo Mzee

Asitufanye tuwe na dhiki Ndiyo Mzee

KIAMBATANISHO 2

GODORO LA MTUMBA

1a) Hadithi ya Godoro la Mtumba, iliyotungwa na kuandikwa na Irene Mwamfupe Ndauka.

Hii ni hadithi fupi inayogusa maisha ya wanadamu au ya jamii kwa jumla, ni vitu ambavyo vinatokea katika jamii tunazoishi. Hadithi hii inaitwa **"Godoro la Mtumba"**. Ni hadithi yenye kusisimua na yenye mafundisho ndani yake, kuhusu mapenzi. Mapenzi ni dhamira kubwa sana iliyojitokeza katika kitabu hiki, na ni kitu kizuri katika maisha ya binadamu, ila kikitumika vibaya kinaweza kuleta madhara makubwa sana kwa wapenzi, rafiki, ndugu, jamaa na jamii kwa jumla.

Hadithi hii inahusu ndugu wawili waliojikuta wakiingia katika swala la mahusiano ya kimapenzi na kusahau kuwa wao ni ndugu wa karibu sana. Mjomba msafiri aliamua kumshawishi na kumlaghai mjomba wake Zuwena ili wawe wote kimapenzi baada ya kumuona Zuwena amekua na anavutia kimapenzi. Pia aliamua kumuacha mpenzi wake Zuhura Chachandu ili wapate muda wa kuwa pamoja na Zuwena. Zuwena ni mtoto wa dada yake Msafiri. Zuwena baada ya kumaliza darasa la Saba katika Shule ya Msingi Usagara alikosa nafasi ya kuendelea na masomo, ndipo mjomba wake alipomchukua kwa nia ya kumuendeleza. Alimchukua mwaka mmoja mbele baada ya kutengana na mke wake. Alimtafutia sekondari ya binafsi iliyopo maeneo ya Ubungo Kibangu na kuanza masomo. Mjomba wake alikuwa na kazi nzuri yenye maslahi makubwa, hivyo aliajiri msichana wa kazi na mlinzi, lakini baada ya muda aliwaondoa watu hao na kujikuta wakiishi yeye na Zuwena tu katika nyumba hiyo.

Zuwena alipofika Kidato cha Tatu, ndipo mjomba Msafiri alipoamua kuvunja ukimya na kumshawishi Zuwena kuingia katika mahusiano ya kimapenzi.

Alifanikiwa kumteka kiakili kwa kuwa alikuwa ni binti mdogo na hakuwahi kukutana na mwanaume yeyote kimwili toka atoke tumboni mwa mama yake. Zuwena alipoingia katika mchezo huo, akajikuta ananogewa. Jina la mjomba likafa, na kujikuta akimuita mjomba wake majina ya kimapenzi kama vile mpenzi, honey, baby, sweet, na mengineyo. Uwezo wake darasani ulipungua na kujikuta akiingia tena katika mahusiano na walimu wa kiume na wanafunzi kwa lengo la kusaidiwa kimasomo na kuwafahamu wanaume wengine zaidi. Walinogewa na mapenzi na kujikuta wakati mwingine Zuwena haendi shule, wala Msafiri haendi kazini.

Mama yake Zuwena alikuwa akiota ndoto mbaya juu ya Zuwena na mdogo wake Msafiri. Hivyo, aliamua kufunga safari kutoka Tanga kwenda Dar es Salaam kuwatembelea. Baada ya kufika huko, aligundua kuwa kuna mchezo unaoendelea kati ya Zuwena na Msafiri. Aliamua kuendelea kukaa na kufuatilia kwa kina nyendo zao, na baada ya muda alipata ukweli. Zuwena na Msafiri walinogewa na mapenzi na kutojali kuwa mama Zuwena yupo. Zuwena alikuwa akitoroka usiku kutoka chumba alicholala na mama yake na kwenda kwa mjomba wake. Mama alimtafuta mara kadhaa, lakini walimdanganya kwa maneno mengi. Waswahili wanasema, za mwizi ni arobaini. Hatimaye, siku hiyo mama Zuwena aliwakuta wakiwa kitandani kwa Msafiri, tena watupu kama walivyozaliwa.

Baada ya fumanizi hilo walikosa cha kujitetea tena. Mama baada ya kupata ukweli, aliamua kuondoka na kuwaachia maneno makali ya laana juu yao na pia akaenda kuwaambia ndugu. Huku nyuma, Zuwena na Msafiri waliendelea na mapenzi, huku Zuwena akitaka wafunge ndoa ili wawe mke na mume kama Msafiri alivyomuahidi siku za nyuma. Dakika za mwisho, waligundua walichokifanya siyo kizuri kwa ndugu na hata kwa jamii kwa jumla. Waliamua waende Tanga kuomba msamaha.

Lakini kutokana na mawazo na mwendo kasi wa Msafiri, walijikuta wakipata ajali na Msafiri kupoteza maisha papo hapo, na Zuwena kujikuta hospitali na mama yake akiwa pembeni.

1b) Hadithi ya Kutoka Uchungaji Mpaka Ukuu wa Wachawi, iliyotungwa na kuandikwa na Ally Mbetu

Hii ni hadithi fupi inayogusa maisha ya wanadamu au ya jamii kwa jumla, ni vitu ambavyo vinatokea katika jamii tunazoishi. Hadithi hii inaitwa "**Kutoka Uchungaji Mpaka Mkuu wa Wachawi"**. Ni hadithi yenye kusisimua na yenye mafundisho ndani yake, na inahusu imani katika dini ya Kikristo. Inaonyesha jinsi baadhi ya viongozi wa dini wasivyokuwa na imani au wana imani haba na vitu wavifanyavyo, na kukosa imani na Mungu na kuamua kujiingiza katika imani za kishirikina ili kupata sifa zaidi ya kile wanachokifanya.

Hadithi hii inamuhusu Mchungaji anayeitwa Joshua, aliyepewa karama kubwa na Mungu ya kuhubiri na kuombea wenye matatizo mbalimbali katika maisha, au katika jamii inayomzunguka na jamii nyingine. Mchungaji Joshua aliifanya kazi yake kwa moyo, akiamini ni kipawa alichopewa na Mungu. Alianza katika mazingira magumu ya kutokuwa na kanisa na waumini wachache. Lakini kutokana na kipawa chake cha kuombea watu wakapona magonjwa na mapepo kutoka, jina lake lilikuwa kwa kasi na kusababisha kila kukicha waumini wazidi kuongezeka kwenye Kanisa Lake. Ongezeko hilo lilisababisha ongezeko la pesa na zawadi nyingi kutoka kwa waumini wake. Kitendo hicho kilisababisha kununua kiwanja na kujenga kanisa kubwa sana litakalopokea waumini wengi zaidi, ila katika huduma yake ya kiroho hakukosa majaribu ila kwa uwezo wa Mungu aliyashinda.

Mchungaji Joshua aliwaombea wagonjwa, na wakapona, wenye shida wakafanikiwa. Hivyo, akafahamika kila kona ya nchi, maana alifanya huduma ndani na nje ya nchi. Siku moja, mwanawe aliumwa akiwa safarini na aliporudi alimfanyia maombi ili apone kwa masaa kadhaa lakini haikusaidia. Aliamua kumpeleka hospitali, lakini kwa bahati mbaya alifariki dunia. Kitendo kile kilihuzunisha sana familia. Baada ya miezi michache mwanawe wa kiume tena aliugua ghafla. Yeye na wachungaji wenziwe wakamfanyia maombi, lakini ilishindikana. Walipompeleka hospitali, alifariki dunia. Alipoteza imani kwa Mungu na kujiuliza kwanini kwake kunabomoka kila siku na kwingine kukizidi kuimarika, wakati ni yeye ndiye anayefanya kuimarike. Hivyo akaona Mungu amemuacha na ameamua kumpa mapigo makali sana. Baadhi ya watu walisema kuwa anatoa watoto kafara ili aweze kuonekana Mchungaji mwenye kipaji cha kuombea, kuponya na kutatua matatizo ya watu. Baada ya siku chache, mkewe aliugua na kupoteza fahamu. Alimuombea, lakini haikusaidia. Alimpeleka hospitali, hakiwa hali ikawa mbaya zaidi.

Siku moja akiwa ofisini kwake, alitembelewa na wazee wawili wakidai wamekuja kumponya mke wake kwa dawa za kienyeji. Alikataa, lakini baadaye ushawishi wa wazee ulimshinda nguvu Mchungaji Joshua na kujikuta akikubaliana nao. Wazee wale walikuwa wachawi na walitumwa na mkuu wao kuja kumshawishi ili aingie katika nguvu hizo maana anamaliza watu wao kwa kuokoka, na wao ndiyo waliohusika na vifo vya wanawe na ugonjwa wa mkewe. Walimwagiza vitu vya kichawi vya kumponya mke wake na hatimaye alipona, na yeye wakafanikiwa kumuingiza kwenye kundi lao la uchawi na kumpa cheo kikubwa kuwa mkuu wao wa wachawi. Pia walimpa masharti ya kutoa vitu vyote vinavyohusiana na dini nyumbani kwake na kumuamuru yeye na familia yake waache kusali. Walimpatia vitu vya kichawi vitakavyomuwezesha kutenda miujiza zaidi atakapokuwa kanisani,

hadi kufufua watu. Pia walihitaji sadaka ya damu. Hivyo, Mchungaji alikuwa anaua watu na kupata damu na vichwa vyao kuviweka mbele ya madhabahu (mahali ambapo Mchungaji anasimama kuhubiri). Jina la Mchungaji likazidi kukua, na miujiza yake kuzidi kutokana na uchawi. Na aliye mkashifu tu kwa njia yoyote ile alipoteza uhai wake.

Maisha yaliendelea na mke wake akashiriki katika ushirikina huo na vifo vya watoto wake vikaisha. Siku moja alitakiwa kumtoa mtoto wake sadaka kwa kiongozi wao wa kichawi ambaye haonekani. Mchungaji Joshua alipata wakati mgumu sana kumtoa mtoto sadaka, na cha kusikitisha mtoto alimlalamikia baba yake kwa kumtoa sadaka. Alitakiwa amchinje kwa mkono wake, ila alishindwa na mwisho, mtoto alifariki. Hapo Mchungaji na familia yake walilia sana na kuona kumbe hata huko kwa shetani hakuna msaada. Ndipo mke wake alipomshawishi wapige magoti chini na kumrudia Mungu. Walitubu kwa Mungu na kwa waumini wote na kuanza maisha mapya ya kiroho tena, ijapokuwa mwishowe alipelekwa polisi kujibu tuhuma za mauaji. Kutokana na kutubu kwake na kesi kukosa ushahidi, aliachiwa huru na kuhama sehemu ile na kwenda sehemu nyingine kufanya huduma ya kiroho.

KIAMBATANISHO 3

MIONGOZO YA UDODOSAJI NA USAILI

1 a) Mwongozo wa Usaili kwa Watu wa makamo, viongozi wa dini na wanasiasa.

Utafiti huu unahusu ulinganishi wa kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku. Vilevile utafiti huu unalenga kubaini msukumo wa watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi katika Magazeti ya Udaku. Pia utafiti huu unalenga kubainisha dhamira zinazopatikana katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi na kulinganisha dhamira za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku.

1. a) Je, unaelewa nini kuhusu muziki wa Bongo Fleva?
   b) Je, unaelewa nini kuhusu Magazeti ya Udaku?
   c) Je, unadhani mambo hayo ni kundi gani la watu: watoto, vijana au watu wazima? Kwanini?

2. Je, umewahi kusikiliza muziki wa Bongo Fleva na kusoma Magazeti ya Udaku?

   Kama ndiyo/ hapana, ni nini kilikusukuma au kukuvutia ?

3. Je, unadhani kwa kupitia muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku jamii

   inaweza kujifunza jambo lolote? Kama ndiyo, ni lipi na kama hapana kwa nini?

4. Unafahamu nini kuhusu dhamira katika jamii ya Kitanzania?

5. Je kuna dhamira zipi katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya

   udaku?

6. Je, wafikiria dhamira katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za magazeti ya

udaku zinafanana au kutofautiana katika jamii?

7. Unaweza kuwaelezeaje wanamuziki wa Bongo Fleva wa sasa na waandishi wa

hadithi fupi za Magazeti ya Udaku wa sasa?

Ahsante kwa Ushirikiano Wako

KIAMBATANISHO 4

1b) Mwongozo wa usaili kwa Wanafunzi na Wanachuo

1. Unaelewa nini kuhusu muziki wa Bongo Fleva na Magazeti ya Udaku?

2. Unawafahamu wanamuziki wa Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi za Magazeti ya Udaku? Wataje kwa majina yao.

3. Ni msukumo upi unaowapata watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku, hadi kutunga au kuandika kazi zao?

4. Unadhani dhamira zinazopatikana katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinatoka wapi?

5. Je, dhamira zilizomo katika nyimbo za Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku zinafanana au kutofautiana? Kama ndiyo/hapana toa sababu.

6. Je, ni kweli kuwa muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku ni vya kihuni na vinawahusu wahuni au vijana tu na havina mchango wowote katika jamii? Kama ndiyo/hapana toa sababu.

7. Una maoni gani kuhusu wanamuziki wa Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi za Magazeti ya Udaku?

Ahsante kwa Ushirikiano Wako

KIAMBATANISHO 5

1 c) Mwongozo wa Mjadala wa vikundi kwa Washabiki wa Muziki wa Bongo Fleva na Wasomaji wa Hadithi fupi za Magazeti ya Udaku.

1. Unaujua muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku?

2. Umewahi kusikiliza nyimbo zozote za Lady Jay Dee, Diamond, Linex, Nick wa Pili na Profesa J? Na umewahi kusoma hadithi zozote za Irene Ndauka? Unadhani zina ujumbe wowote?

3. Unasema nini kuhusu wanamuziki wa Bongo Fleva na waandishi wa hadithi fupi?

4. Je, kuna dhamira katika muziki wa Bongo Fleva na hadithi fupi za Magazeti ya Udaku? Kama zipo zitaje, na kama hakuna kwanini?

5. Je, unadhani dhamira zilizopo ndani ya Bongo Fleva na hadithi fupi zinafanana au kutofautiana katika jamii?

6. Je, muziki wa Bongo Fleva na hadithi za Magazeti ya Udaku ni vitu visivyokuwa na maana wala maadili mema katika jamii ya Kitanzania? Toa sababu.

7. Unawashauri nini watu ambao hawasikilizi muziki wa Bongo Fleva, wala hawasomi Magazeti ya Udaku?

Ahsante kwa Ushirikiano Wako